

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA ISHIRINI

Kikao cha Thelathini – Tarehe 14 Julai, 2010

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:

Sera ya Taifa ya Ajira ya Mwaka 2008 [*The National Bill Employment Policy for the year 2008*].

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUPH MZEE):

Majibu ya Hazina Kuhusu Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali kwa Hesabu za Serikali zilizoishia Tarehe 30 Juni, 2008.

Na. 221

Ugawaji wa Majimbo, Tarafa na Kata Nchini

MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA (K.n.y. PROF. FEETHHAM FILIPO BANYIKWA) aliuliza:-

Kwa kuwa sensa ya mwaka 2003 ilionyesha ongezeko kubwa la watu Vijijini na kuonyesha umuhimu wa Serikali kuangalia jinsi ya kupeleka huduma za kutosha kwa wananchi:-

- (a) Je, ni lini Serikali itatumia sensa hiyo kugawa maeneo ya majimbo, Tarafa na Kata ili kurahisisha Utawala kwa Wananchi Vijijini?
- (b) Je, ni lini vitongoji vya Mozi, Tunyi, Teweta, Mwanya, Jengeni, Nondo na Kachele ambavyo vina shule za msingi na idadi kubwa ya watu vitafanywa kuwa vijiji kamili?

(c) Je, Serikali inakamilisha vipi maandalizi ili vitongoji hivyo viwe na vituo vya kupigia kura katika Uchaguzi wa mwaka 2010, tofauti na miaka ya nyuma ambapo kumekuwa hakuna vituo hivyo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI MISTAA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Mbunge, naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ugawaji wa maeneo ya Utawala nchini kwetu huzingatia matakwa ya Kisheria na Kanuni zinazoongoza zoezi hilo. Kwa mfano ugawaji wa maeneo ya Mkoa na Wilaya hufanywa na Mheshimiwa Rais kwa mujibu Mamlaka anayopewa ndani ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ugawaji wa maeneo ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa hufanywa na Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa kwa mujibu wa Sheria sura 287 na 288 ya mwaka 1982. Isipokuwa upandishaji hadhi Halmashauri kuwa Jiji ambako Waziri mwenye dhamana hupendelekeza kwa Mheshimiwa Rais naye akiridhia hutamka Halmashauri hiyo kuwa Jiji.

Aidha, ugawaji wa Majimbo ya Uchaguzi kwa ajili ya Uchaguzi wa Wabunge hufanywa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi, kwa kuzingatia matakwa ya Sheria. Ugawaji wa Kata, Vijiji, na Mitaa uko kwenye Mamlaka ya Waziri mwenye dhamana na Serikali za Mitaa ugawaji wa vitongoji hufanywa na Halmashauri husika na baadaye kutoa taarifa kwa Waziri mwenye dhamana na Serikali za Mitaa kwa ajili ya kumbukumbu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ludovic John Mwananzila Mbunge wa Kalambo, lenye sehemu (a), (b), na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi la ugawaji wa Tarafa, Kata, Vijiji, Mitaa na vitongoji huzingatia vigezo maalum ambavyo vimewekwa.

Aidha, naomba kumfahamisha Mbunge pamoja na Bunge lako Tukufu pamoja na kigezo cha idadi ya watu kuna vigezo vingine ambavyo hutumika kama vile ukuaji wa uchumi, hali ya kijiografia ya eneo husika, idadi ya kaya, na hali ya mawasiliano.

Hivyo Serikali hugawa maeneo mara kwa mara ili kurahisisha Utawala kwa wananchi katika maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu tayari imeandaa orodha ya majina ya Kata, Mitaa, Vijiji na Vitongoji ambayo yamechapishwa katika gazeti la Serikali tangazo Na. 205 la tarehe 26/6/2009 na tangazo Na.173/174 la tarehe 7/5/2010. Maeneo hayo ya

utawala yalitumika katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka 2009 na pia yatatumika katika Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika mwezi oktoba mwaka huu 2010.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria na Kanuni zilizopo, Kitongoji huundwa na Kaya zisizopungua 50. Kwa mujibu wa Sheria sura 287 ya mwaka 1982 kifungu 30 (3) kijiji huundwa na vitongoji visivyozidi vitano (5) yaani kaya 250 na kuendelea. Hivyo, naomba nitoe angalizo kwamba kuwepo kwa shule ya msingi siyo kigezo pekee cha kupandisha hadhi ya kitongoji.

Wakurugenzi wa Halmashauri wameelezwa kuzingatia vigezo kabla ya kuwasilisha maombi ya kupandisha hadhi maeneo ya utawala. Ni matumaini yangu kwamba vitongoji vya Mozi, Tunyi, Teweta, Mwaya, Jengeni, Nondo na Kachele vilivyomo katika Jimbo la Mheshimiwa Mwananzila vitashughulikiwa baada ya kukidhi vigezo muhimu ili viwe viwe vijiji kamili.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu upi utumike katika kuainisha vituo vya kupigia kura katika Uchaguzi Mkuu mwaka 2010, suala hili hufanywa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa mujibu wa taratibu watakazojiwekea pale Uchaguzi utakapokaribia.

Na. 222

Hitaji la Magari ya Shule- Sengerema

MHE. SAMUEL M. CHITALILO(K.n.y. MHE. JACOB D. SHIBILITI)
aliuliza:-

Kwa kuwa Wilaya ya Sengerema ina shule mbili za sekondari kwa kila Kata lakini hazina huduma ya usafiri ikizingatiwa kuwa Kata ya Nyakasasa, Lugata, Komewo na Maisome zipo visiwani na zingine ziko mbali na Makao Makuu ya Wilaya.

Je, Serikali itatoa gari kwa kila Kata ili walimu wetu wapate huduma.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA
NA SERIKALI MISTAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Samuel Mchele Chitalilo, Mbunge wa Buchosa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua uwepo wa tatizo la uhaba wa vyombo nya usafiri katika shule za sekondari hapa nchini hususan magari. Hali hii inatokana na ufinyu wa Bajeti na fedha kidogo zinazotengwa kwa ajili ya maendeleo na usimamizi na uendeshaji wa shule za sekondari. Aidha, ni nia ya Serikali kulitafutia ufumbuzi tatizo hili la usafiri katika shule za sekondari kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema ina jumla ya shule za sekondari 40 na ina Kata 25. Kulingana na mahitaji halisi ya gari kwa kila shule jumla ya shilingi bilioni 3.2 zitahitajika ikiwa kila shule itanunuliwa gari. Kwa kuzingatia Bajeti inayotolewa ya shilingi milioni 200 za maendeleo kwa mwaka ni dhahiri kuwa fedha zinazotengwa ni kidogo ukilinganisha na mahitaji halisi ya fedha kwa ajili ya shughuli za maendeleo, kutokana na hali hiyo Halmashauri ikipanga kununua gari moja kwa ajili ya shule itahitaji kutenga shilingi milioni 80 kutoka katika Bajeti hiyo. Aidha, kwa kuwa mahitaji ya fedha kwa shughuli za maendeleo ni makubwa ikiwa ni pamoja na kununua magari kwa ajili ya shule ni jukumu la Halmashauri kuweka mipango ya utekelezaji ikiwa ni pamoja na kutafuta fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tatizo hili la usafiri uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema unashauriwa kuandaa maandiko (*Project Proposals*) yatakayowasilishwa kwa wadau mbalimbali ili kusaidia ununuzi wa magari.

Hata hivyo, suala la kuzipatia shule usafiri wa uhakika yakiwemo magari ni jukumu la Halmashauri yenye kuweka katika vipaumbele vyake wakati wa maandalizi ya Bajeti.

MHE. JACOB D. SHIBILITI: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri napenda niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Waziri anafahamu kabisa kuwa Halmashauri zetu zina mzigo mkubwa zaidi katika shughuli mbalimbali za maendeleo ukizipa mzigo huu mwingine wa kutafuta gari bado inakuwa ni kazi nzito sana kwa nini Serikali isifanye mkakati maalum kwa ajili ya kuzisaidia Halmashauri hasa shule zetu za sekondari ambazo ni nyingi na ziko kwenye matatizo makubwa mno. Mfano Wilaya ya Misungwi shule ya Sekondari Mbarika, Ilujamate, Nhunduzizina matatizo kama hayohayo ya Wilaya ya Sengerema. (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOAA NA SERIKALI MISTAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, analolisema Mheshimiwa Shibili tunalionna na tunalifahamu. Mimi nataka kusema kuwa hapa kuwa sasa hivi baada ya kujenga hizi shule za Kata na kuhakikisha kwamba sasa hawa watoto wanakwenda shuleni na nyinyi mmemsikia Waziri wa Elimu amesimama akizungumza suala la kipaumbele kwamba sasa tutakwenda kwenye nyumba za Walimuna maabara na

sisi sote tulielezwa hapa na ninavyofahamu mimi Bajeti ni mpango wa Serikli unaoonyesha namna hela zitakavyopatikana na namna zitakavyotumika na Bajeti ilishapita hapa na sisi sote tukaitikia tukasema ndiyo tukasema kuwa ipite.

Sasa nikiambiwa kuwa hapa nibadilishe niweke matumizi ya magari labda itabidi nipaye maelekezo mapya hapa kwa sababu sijui kwamba tunafanyaje sasa kwa sababu Bajeti imeshapita na kila kitu kimeshapita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana katika jibu hili sasa unaona tunesogea kidogo tukaseka kwamba tuandike *Project write ups*. Sisi Wizara ya TAMISEMI tuko tayari kushirikiana na Halmashauri hizi zinazozungumziwa katika maana ya kuagiza wataalam wetu wasaidie katika kuandika hizi *project write ups* ili tuweze kupata hizo fedha ndivyo ninavyoelewa mimi vinginevyo itakuwa ni vigumu mimi kutamka hapa na jamani hapa tulipofika tena tukianza kuhojiana na jana nimemaliza kila kitu jamani si nitaonekana wa ajabu? Kwa hiyo, Mheshimiwa Shibili ninaiona *point* yako lakini hali ndiyo hiyo kama mnaona kuwa ni muhimu kufanya hivyo basi muweke katika vipaumbele vya Bajeti yenu.

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kuna shule zilizoko katika maeneo magumu. Je, Serikali itakumbuka kuweka kipaumbele kwamba wakati wa kugawa magari zikumbukwe shule hizo zilizoko katika maeneo yenye mazingira magumu. Ambayo walimu ni shida kusafiri na wanafunzi wakiugua hakuna namna ya kuwapeleka hospitalini. Je, hilo lisingekwa kigezo cha kuwasaidia katika shule za sekondari zilizoko katika maeneo haya kama shule zilizoko katika Jimbo la Longido?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUIU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaOmba kujibu swali la Mheshimiwa Lekule kaka yangu na Jirani yangu na ninasema haya yote kwasababu mimi na ye ye tunatoka mahali pamoja ni majirani na sitaki mimi nikifika kule tena nioneckane nimejibu mambo ya ajabuajabu hapa. Kwanza kabisa nataka niliambie Bunge lako Tukufu na nyinyi wote mnakumbuka kwamba Wilaya ya Longido ni miiongoni mwa Wilaya ambazo tumeziweka katika Wilaya ambazo zinaonekana kuwa zina mazingira magumu kwamba sasa tutapeleka gari kwa maana hii inayozungumzwa hapo itategemea na vipaumbele ambavyo vimewekwa pale kwa kweli tunachoangalia kikubwa pale ni nyumba za walimu, masuala ya watumishi, maabara na madarasa tunaangali tunaagalia namna ya kuweka *solar system* na vitu vingine ndivyo vitu ambayo tumevipitisha, Kwa hiyo, nataka kumwambia Mheshimiwa Lekule Laizer kuwa hata hili la magari kuwa sasa tutawa- *consider* litategemeana na fedha kama tutakuwa tumepata kwa maana hii inayozungumzwa wako watu wengine wanaotoka Ludewa tunapeleka maboti. Sasa tukiona kwamba hilo ni jambo ambalo ni kipaumbele kama anavypendekeza hapa na hela zikawa zimepatikana basi tutafanya hivyo kama Mheshimiwa Mbunge anavyoelekeza. (*Makofi*)

Na. 223

Ahadi ya Rais ya Ajira Milioni Moja

MHE. HALIMA J. MDEE aliuliza:-

Kwa kuwa moja kati ya ahadi za Rais, Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete wakati akiomba kura kwa wananchi kama mgombea Urais wa Chama cha Mapinduzi (CCM) mwaka 2005 ni kutengeneza ajira mpya milioni moja, na kwa kuwa, hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana (2009/2010) ilionyesha kwamba ahadi hiyo imetekelizwa kwa kuwepo kwa ajira mpya zaidi ya milioni moja:-

- (a) Je, ni ajira za aina gani zilizotengenezwa na Sekta gani iliyoongoza kwa kutoa ajira hizo?
- (b) Je, ni wanawake wangapi waliofaidika na ajira hizo mpya na wako kwenye sekta gani?

NAIBU WAZIRI WA KAZI,AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA
alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 iliahidi Serikali ya Awamu ya nne itawezesha upatikanaji wa ajira milioni moja kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2005/2006 mpaka 2010.

Hata hivyo ndani ya miaka mitatu ya mwanzo kufikia Desemba 2008, tayari jumla ya ajira mpya 1,271,923 zilizalishwa ambapo wanawake 613,459 (sawa na asilimia 48.2) na wanaume 658,464 (sawa na asilimia 51.8 ambapo sekta ya binafsi imeongoza kwa kutoa ajira 1,185,387 (wanawake 572 ,829 na wanaume 612,558) ikifuatiwa na Serikali kwa kutoa ajira mpya 86,536 ambapo wanawake ni 40,631 na wanaume 45,905.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, uchanganuzi zaidi unaonyesha baadhi ya sekta muhimu ambazo zimezalisha ajira nyingi ni pamoja na:-

- (i) Afya: 36,776 9 wanawake 25,949, wanaume 10,827).
- (ii) Elimu: 37,740 (wanawake 13458, wanaume 24,282).
- (iii) Usafirishaji na Mawasiliano: 15,536 (wanawake 997, wanaume 14,539).
- (iv) Huduma ya Fedha: 7,788 (wanawake 3,908, wanaume 14,539).
- (v) Ujenzi: 118,378 (wanawake 9688, wanaume 108,690).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Aidha takwimu za ajira mpya kuhusu, uvuvi na ufugaji zinatarajiwu kutolewa mara baada ya zoezi la uchambuzi wa sensa ya kilimo iliyofanyika mwaka jana kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hizi zilipatikana kutoptana na utafiti wa watu wenye uwezo wa kufanya kazi (*Intergrated Labour Force Survey – 2006*), utafiti wa mapato na matumizi ya kaya binafsi (*Household Budget Survey – 2007*) pamoja na taarifa za kiutawala

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru katika swal语 langu la msingi niliuliza ni ajira za aina gani na ngapi zilizotengenezwa na nikataka nichambuliwe.

Katika jibu la Naibu Waziri, kwa mujibu wa uchambuzi ajira ambazo zinaonekana zimetengenezwa ni laki mbili na kumi na sita tu tofauti na maelezo ya Waziri na vitabu vyao kuwa wametengeneza ajira milioni 1.271 hali kadhalika katika jibu lake anaonyesha kwamba takwimu za ajira mpya kuhusu kilimo, uvuvi na ufugaji zina tarajiwa kutolewa mara baada ya zoezi la uchambuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swal语 langu kwa Mheshimiwa Naibu Waziri hizi takwimu za ajira milioni 1.2 zimetoka wapi wakati hakuna uchambuzi wowote uliofanyika kuhusiana na hizi ajira? Swal语 langu la pili kwa mujibu wa taarifa ya vitabu vya Serikali sekta binafsi ambayo tulitaraja kwamba ingesaidia kuongeza ajira zilizo rasmi imepunguza kwa *negative* 48,000. Sasa nilitaka Mheshimiwa Naibu Waziri atusaidie tatizo ni nini? Sekta binafsi Tanzania imefeli ama Serikali imeshindwa kuratibu ili kuweza kutengeneza ajira?

NAIBU WAZIRI WA KAZI AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, napenda kujibu maswali ya Mheshimiwa Mdee kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kwamba takwimu zinatofautiana mimi naona siyo kweli kwa sababu nimesema nilipokuwa najibu kipengele a kwamba ajira zilizozalishwa jumla ni milioni moja na laki mbili sabini na moja kufikia Disemba 2008. na nikasema wanawake kati ya hao ni laki sita kumi na tatu elfu mia nne na hamsini na tisa na wanaume laki sita hamsini na nane. Kwa hiyo bado takwimu ndiyo hizo hizo. Isipokuwa uchambuzi kwa maana ya vipengele gani au ni sekta gani tumechambua kwa upande wa sekta rasmi kwa maana ya ile sekta ya Umma, afya, elimu, usafirishaji na mawasiliano huduma za fedha na ujenzi. Lakini kwa upande wa jumla ya ajira zilizozalishwa nimesema ni milioni moja na laki mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kilimo na ufugaji kwamba hizi zitafanyika baada ya sensa kukamilika, ndivyo nilivyojibu, kwamba sensa ilifanyika mwaka jana na tutafanya uchambuzi ili tuweze kuona. Na tunaamini kabisa kwamba tukifanya uchambuzi katika sekta hizi, ajira ambazo zimezalishwa zitakuwa ni nyingi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sekta rasmi binafsi kupunguza, huu ulikuwa ni wakati ule ambapo makampuni yalikuwa yamepunguza watu, mimi ninahakika kwamba baada ya hali ya uchumi kuanza kuimarika na baada ya takwimu sasa kuja kukusanywa mpya kifikia mwaka 2010, naamini sasa ajira zimeanza kupanda katika hizi sekta rasmi, binafsi na nina hakika kwamba hiki kiasi cha ajira 48,000 haitakuwepo tutakapofanya takwimu mara nyininge. (*Makati*)

Na. 224

Ukaguzi wa Mizigo Katika Bandari ya DSM

MHE. MWADINI ABBAS JECHA aliuliza:-

Sehemu ya ukaguzi wa mizigo ya Bandari ya Dar es Salaam kwa abiria wanaotumia boti ndogo na zile ziendazo kasi wanapata usumbufu mkubwa kupanda juu kupitia vipandio vingi (ngazi) ambapo abiria na kuli hulazimika kubeba mizigo kichwani:-

Je, Serikali inachukua hatua gani kulitatua tatizo hili?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Miundombinu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mbunge wa Wete kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kupunguza tatizo la kupanda ngazi nyangi zinazowaletea usumbufu abiria bandarini, Serikali kupatia Mamlaka ya Bandari (*TPA*) inao mpango wa kufanya marekebisho ya dharura ya ngazi hizo ili kuboresha usalama wa abiria na mizigo yao wanapopanda melini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa kudumu ni kujenga gati la kisasa la kuhudumia abiria lenye hadhi sawa na vituo vya Kimataifa vya kuhudumia abiria(*International Passenger Terminal*). Mchakato wa utekelezaji wa mradi huu umeanza kwa kumteua mtaalam mshauri na kazi ya kutayarisha mchoro itakamilika hivi karibuni. Kazi ya ujenzi inatarajiwa kufanyika katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa gati hili utaiwezesha Bandari ya Dar es Salaam kutoa huduma katika kiwango cha Kimataifa kwa meli za abiria na abiria wenywewe.

MHE. MWADINI ABBAS JECHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali imekubali kufanya marekebisho ya gati Dar es Salaam wanapoteremka abiria ili

kuboresha usalama wa abiria na mizigo, na kwa kuwa Serikali ipo tayari kwa mpango wa baadaye kujenga gati ya kisasa ya kimataifa kwa madhumuni hayo hayo:-

(i) Je, Serikali katika hatua zote mbili za ujenzi iko tayari kuzingatia mahitaji ya walemovu hasa walemovu wa miguu na wa macho?

(ii) Kwa kuwa, katika gati iliyopo sasa hivi hakuna vifaa vyta upekuzi wa mizigo na utaratibu uliopo ni kupekua mizigo ya watu kadarnasi na hii ni kinyume na haki za binadamu. Je, Serikali iko tayari sasa kufunga mitambo ya upekuzi wa mizigo kukwepa adha hiyo?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUDOMBINU: Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la kwanza la kuzingatia hali ya walemovu wa aina mbalimbali katika ujenzi wa hizi gati ambazo tunatarajia kuzijenga, napenda nikubaliane naye Mbunge kwamba tutakapokuwa tunaandaa mpango huu suala hilo litazingatiwa kwa sababu kwa kila hali Serikali inawajali sana wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili la kuangalia uwezekano wa kufanya marekebisho ili kuweza kupekua mizigo katika hali ya faragha kidogo, nimesema hapa katika jibu la msingi kwamba ipo mipango ya kufanya marekebisho ya dharura, na katika marekebisho hayo tutaelekeza suala hili nalo liweze kuzingatiwa.

MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD: Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri nina swali moja la nyongeza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru kwamba anakiri ujenzi wa pale labda ni wa karne ya kumi na nane au kumi na saba nyuma zaidi. Je, Waziri anaonaje kuwa na mpango wa dharura kwa sababu hili ni tatizo na linasumbua; ni mpango gani wa dharura kwa sasa hivi ya kuwasaidia walemovu pamoja na mizigo ili ipitishwe kwa usalama?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUDOMBINU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi ya kwamba ufumbuzi wa kudumu wa tatizo hili ni kujenga gati lenye hadhi ya kimataifa, ambapo nimesema kwamba tutazingatia hali ya walemovu ili isiwaletee usumbufu.

Lakini kwa mipango ya dharura ambayo sasa hivi tunairekebisha pengine itakuwa si rahisi sana kuzingatia hali ya walemovu kutokana na miundombinu iliyokuwepo kwa sababu ni ya muda mrefu.

Lakini naomba tuwe na uvumilivu kwamba tutakapokuwa tunaandaa mpango wa muda mrefu na wa kudumu, walemaavu watazingatiwa kama nilivyoeleza awali.

Na. 225

Mpango wa Kupeleka Umeme Mji Mdogo wa Tunduma

MHE. DR. LUKA JELAS SIYAME aliuliza:-

Kwa kuwa, hapo awali wananchi wa Mji mdogo wa Tunduma walikuwa na matarajio ya kupatiwa umeme wa uhakika kutokana na mipango ya kupeleka umeme wa *grid* ya Taifa Sumbawanga katika kipindi kifupi kijacho, lakini kwa utaratibu wa mpango Kabambe wa Taifa wa usambazaji Umeme wa *TANESCO*, umeme huo hautegemewi kabla ya mwaka 2018.

Je, Serikali ina mpango gani wa dharura wa kuupatia Mji wa Tunduma unaokua kwa kasi kubwa umeme wa uhakika?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, kabla ya kujibu swalii la Mheshimiwa Dr. Luka Jelas Siyame, Mbunge wa Mbozi Magharibi, naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa swalii la Mheshimiwa Mbunge, umeme wa *grid* ndiyo umeme wa uhakika. Lakini hata umeme usiotokana na *grid* mathalani kwenye maeneo ambayo kuna upopo wa kutosha au gesi asilia au makaa ya mawe ya kuhakikisha uzalishaji endelevu usiosimama wa umeme utakaokidhi mahitaji ya umeme nje ya *grid* iliyopo, umeme huo utakuwa wa uhakika na huenda hata ukawa nafuu kuliko kusafirisha umeme kutoka *grid* ambayo katika mazingira hayo inaweza ikawa iko mbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo ya utangulizi naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji mdogo wa Tunduma ulikuwa ukipata umeme kutoka *grid* za Zambia kabla ya mwezi Desemba 2007 lakini sasa Mji huo umeunganishwa kwenye *grid* ya Taifa kwa njia ya umeme wa msongo wa kv 33 inayoanzia katika kituo cha Mwakibete Jijini Mbeya. Hii ilifanyika bada ya ya umeme wa Zambia kutokuwa wa uhakika. Umeme unaopatikana sasa hivi wa uhakika na endapo kuna matatizo ni mambo ya kiufundi na juhudii na hatua madhubuti ya kurekebisha hufanywa na mafundi wa *TANESCO* kulingana na tatizo lililopo.

Mheshimiwa Spika, napenda kukiri kwamba kasi ya ukuaji wa Mji huu ni kubwa hivyo, maombi ya umeme nayo ni mengi. Serikali inaendelea kuhimizi Shirika la Umeme

TANESCO kuhakikisha wateja wengi zaidi katika Mji wa Tunduma wanapatiwa huduma hii muhimu.

MHE. DR. LUKA J. SIYAME: Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Kwa vile hili ni swali langu la msingi la mwisho kwa Bunge hili la tisa naomba kwa uchache tu unipe nafasi niwashukuru sana wananchi wa Mbozi Magharibi ambao sasa hivi ni Wilaya mpya na Halmashauri mpya ya Mombasa kwa ushirikiano mkubwa walionipa kwa miaka mitano hii iliyopita na napenda niwahakikishie kwamba Jumatatu ijayo tarehe 21 nitakuwa nachukua fomu kwa ajili ya kugombea kwenye Uchaguzi Mkuu ujao. Kwa hiyo, naomba wanipe ushirikiano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo naomba niulize swali langu la nyongeza. Kwa vile katika jibu lake la msingi kuhusu umeme wa upepo na nguvu ya jua katika Jimbo hili la Mbozi Magharibi Waziri mara ya mwisho alinijibu kwamba umeme utokanao na nguvu hiyo katika Jimbo langu huenda ukawa haiwezekani kwa sababu upepo unavuma kwa utaratibu usiokuwa na mwendo maalum.

Je, sasa hivi Waziri anataka kuniambia ameshafanya utafiti ili kujuua kama upepo huu unavuma kwa uhakika?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipojibu swali hilo kwa wakati huo anaoukumbushia Mbunge nilisema kwamba hata kwenye eneo ambalo upepo unaonekana upo mwingi, bado kuna mahitaji ya kuupima ili kujuua kasi yake, mwendo wake na kadhalika na ukishaupima na kujuua mwendo wake ndiyo utajua upepo ule utazalisha umeme kiasi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mbunge kwamba kwa kuwa tulitoa agizo kwamba upepo huo ufanyiwe tafiti, ni vema basi anipe muda ili niwasiliane na watu wa Wakala wa Nishati Vijijini ambao tuliwapa kazi hiyo waniambie kwamba katika kuupima huo upepo kama wamepata matokeo ya namna gani na kama upepo huo unatosha kuzalisha umeme wa kiasi hicho ambacho maeneo ya karibu ya Mbozi Magharibi wanahitaji na huenda ikawa nafuu kuliko kupeleka *grid* kwenye maeneo hayo.

MHE. MOHAMMED SAID SINANI: Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti wananchi wa Mikoa ya Kusini ya Mtwara na Lindi walipata matumaini makubwa pale Serikali yao ilipofanya jitihada za kuwapatia umeme wa uhakika wa gesi asilia ya Mnazi Bay, tulifurahi na sisi wengine tukaanza kupiga ndogo ndogo kwa wawekezaji kuja kuwekeza. Lakini kinachotokea hivi sasa katika maeneo haya ni kwamba kuna mgao ambao haujapata kutokea katika historia ya Mikoa hii miwili. Hili ni jambo la kusikitisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Waziri atuhakikishie kwamba tatizo hili litaisha lini na kwamba halitatokea tena?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba tulipokamilisha mradi wa umeme kwa ajili ya Mikoa ya Lindi na Mtwara na kwa matarajio ya baadaye kufika mpaka Mangaka na Tunduru umeme ule unatarajiwa uwe wa uhakika zaidi kwa sababu kile chanzo kilichopo cha gesi asilia hakiishi kesho na keshokutwa. Kwa hiyo ni chanzo cha uhakika zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichotokea sasa hivi ni kwamba pale pale mashine sita ambazo kwa ujumla zinatakiwa zizalishe megawati 12, mahitaji ya umeme kwa Mtwara leo ni megawati 8, kwa hiyo ukiwa na megawati 12 ni umeme mwingu na mashine zile zinafanya kazi kwa kupokezana ili kutokuzipa mzigo mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti kwa hiyo kilichotokea ni kwamba katika zile mashine mbili zimeharibika, zimebaki mashine 4, zile mashine zinafanya kazi kwa kupokezana.

Jana Mheshimiwa Sinani na Mheshimiwa Kumchaya na wengine walinifikia na nikawaahidi kwamba nimeongea na watu wa *ARTIMUS* na wanaoendesha ile mitambo sasa watupatie maelezo kwa nini mitambo ambayo ina miaka miwili tu kwa sasa hivi imeanza kuharibika wakati wao wenyewe walitarajia kwamba mitambo ile ingekuwa na uwezekano wa kukaa bila kuhitaji matengenezo makubwa kwa miaka kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti naomba niseme kwamba Serikali inalifanya kazi jambo hili na tujue haraka iwezekanavyo mashine zile mbili zingine zitaingia kwenye mfumo wa uzalishaji lini na ninaomba nikuhakikishie kwamba mafundi wa *MANTRA* wamekwenda na wamekuja mafundi wa Uingereza tunatarajia kwamba watapata ufumbuzi wa tatizo hili haraka iwezekanavyo.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Katika swali la msingi swali la Tunduma linafafana kabisa na suala la Kagunga katika mpaka kati ya Tanzania na Burundi ambapo Mamlaka ya Bandari Tanzania inajenga Bandari pale na Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma imejenga soko. Waziri aliwahi kuahidi hapa Bungeni kwamba atazungumza na watu wa *TANESCO* kwa ajili ya kuhakikisha kwamba shirika la umeme la Burundi linapeleka umeme katika Mji ule wa Kagunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupata maelezo kutoka kwa Naibu Waziri kwamba hali hiyo imefikia wapi na anawaeleza nini wananchi wa mpaka wa Kagunga? (*Makati*)

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimhakikishie tu kwamba kwa sababu ya asili ya Kagunga ni kweli vinafanana kidogo na Tunduma ile hali ya kuwa mpakani na kuhitaji umeme, na kwa sababu ya uzito wa pale kwamba kuna matarajio ya kuwa na soko, bandari na kadhalika yote kama tulivyomwahidi, mimi binafsi nimekutana na Moise Bukumbi Waziri wa Burundi wa Masuala ya umeme mwezi wa tatu, nikamusia hilo suala akaniahidi atalifanya kazi. Nimekutana naye Misri baada ya hapo kwenye *Africans Energy Ministers* akanihakikishia kwamba analifanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Zitto atupe muda ili tuliongee na turejee kwa watu wa Burundi tuone uwezekano kwa sababu na wao kidogo upande ule pia wapo taabani kidogo.

Lakini tuongee nao kama wana uwezo wa kutupa kama megawati moja kiasi kinachohitajika Kagunga au itabidi tufanye utaratibu wa kutoa umeme ambao kwa sasa hivi Kigoma kidogo umeme ni mwinci. (*Makati*)

Na. 226

Kufikisha Umeme Wilayani Lushoto kwa njia Mbadala

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO (K.n.y. MHE. BALOZI ABDI H. MSHANGAMA aliuliza:-

- (a) Je, ni maeneo gani ya Wilaya ya Lushoto ikiwemo Tarafa ya Mlola yanafaa kuendeleza miradi ya Mini-hydro, umeme –jua, au umeme upepo?
- (b) Je, Serikali ina mipango gani ya kufikisha umeme Tarafa ya Mlola kwa kutumika *Grid* ya njia hizo?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Balozi Abdi Mshangama, Mbunge wa Lushoto, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Mwenyekiti, mionganii mwa taarifa tulizo nazo ni za Mto Vuruni unaopita vijiji vya Kwamuhafa na Nkamai ambavyo viro umbali wa kilomita 6 toka kwenye kiwanda cha chai cha Mponde ambapo tayari kuna umeme.

Mto huo huwa na maporomoko ya kina cha meta 80 na mtiririko wa maji wa lita 25 kwa sekunde mwanzoni mwa miezi ya Machi.

Pia Mto India unaopita vijiji vya Langoni na Kishanga, huwa na maporomoko ya kina cha meta 160 na mtiririko wa maji wa lita 11 kwa sekunde mwanzoni mwa miezi ya Machi. Hata hivyo kwa kuwa utafiti wa kina wa mfumo wa maji haujafanyika, hakuna taarifa kama mito hiyo hukauka wakati wa kiangazi. Hivyo haiwezekani kukisia kiasi cha umeme kinachowenza kuzalishwa kwenye mito hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa tulizo nazo ni kuwa Wilaya ya Lushoto inafaa kwa kuendeleza Nishati ya Umeme Jua kwa yale maeneo yaliyo mbali na umeme kutoka gridi ya Taifa. maeneo ya bondeni yakiwa bora zaidi kuliko yale ya milimani.

Aidha uchunguzi wa awali wa Nishati ya Umeme-Upepo uliofanywa na watalaaam wa Wizara ya yangu umeonyesha kuwa maeneo ya Mkumbara yanaweza kuendelezwa kwani yana upepo wa wastani wa kasi ya mita 5 kwa sekunde mwaka mzima.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama za kufikisha umeme wa *grid* katika vijiji vya tarafa ya Mlola zinakadiriwa kuwa shilingi bilioni 1.634. Fedha hizi ni kwa ajili ya ujenzi wa kilomita 25 za njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 33, uwekaji wa *transisfoma* tatu zenyenye ukubwa wa jumla ya kVA 100, pamoja na njia ndogo za umeme za kilovoti 0.4 zenye urefu wa kilomita 4.5. maeneo yatakayohusika ni pamoja na Hemtoe, Msale na Makole. (*Makati*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyoelezwa hapa Bungeni wakati wa kujibu swali la Mbunge tarehe 1 Februari 2010. Mradi wa umeme wa Tarafa ya Mlola ni mionganoni mwa miradi iliopendekezwa na TANESCO kuingiza katika Bajeti ya mwaka 2010/2011 ya mfuko wa Wakala wa Nishati Vijijini *REA/REF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba nitawahimiza Viongozi wa *REA* na Idara ya Nishati Mbadala ya Wizara yangu wafanye tathmini linganishi *comparative analysis* ya uwezekano wa matumizi ya umeme kwa kutumia vyanzo vya Nishati Mbadala vilivyotajwa.

Vilevile wafanye tathimini ya gharama zake kiwango cha uzalishaji na manufaa ya kiuchumi na kijamii ya uwekezaji huo ikilinganishwa na gharama za kuunganisha umeme kutoka kwenye *grid*. Namhakikishia Mbunge kwamba kazi hiyo itafanywa haraka iwezekanavyo na wananchi wa Lushoto watataarifiwa matokeo ya kazi hiyo. (*Makati*)

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kuna mradi wa umeme unaopelekwa katika tarafa ya Mgwasho ambao unaendelea na kwa kuwa tarafa ya Mgwasho inapakana na Mlola:-

(a) Je, Waziri atakubaliana na mimi kwamba wale wanaofanya utafiti wahusise mradi huo wa Mgwasho kwa sababu unaweza kuwa karibu zaidi kuliko upande mwengine?

(b) Kwa kuwa katika mradi wa Mgwasho kulikuwa na timu ya TANESCO lakini ikaondolewa kwenda Kilindi kutekeleza ahadi ya Rais na Rais mwenyewe alitamka juzi kwamba umeme umeshafika Songe Kilindi. Je, ile timu imesharudi ili iendelee na kazi kule Mgwasho?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakubali kwamba utafiti huu ulioko Mlola unaweza kwenda mpaka Mgwasho kwa sababu naamini kwanza kwa yale mazingira yanafanana na kama alivyosema inawezekana kwamba ikawezekana kwamba kuna vyanzo vya Nishati Mbadala upande wa Mlola na vikatumika kukidhi umeme hata wa tarafa zote mbili. Kwa hiyo, naomba

nimwambie kwamba nimelipokea na kwa sababu ni maeneo ya karibu tu sioni sababu kwa nini wanaokwenda Mlola kufanya utafiti wa Nishati mbadala wasiweze kufanya na Mgwash. Kwa hiyo, hili naomba kumhakikisha kwamba litatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nafahamu kwamba kulikuwa na nia ya kukamilisha utekelezaji wa kukamilisha umeme unaokwenda Kilindi kama ilivyokuwa kwenye ahadi ya kuhakikisha kwamba Makao Makuu ya Wilaya zote zinapata umeme. Hii tulifanya pia siyo kwa Kilindi tu lakini pia kwa Uyui na maeneo mengine.

Kwa hiyo, naomba anipe muda niwasiliane na *TANESCO* Mkoa wa Tanga ili niwaaulize kama wale waliokwenda Kilindi wamemaliza kazi na kama sasa wamerudia Mgwash wataendelea na hii kazi ya Mgwash ambayo walikuwa wanaendelea nayo. Nitampa majibu.

MHE. VITA RASHID KAWAWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa wananchi wa Wilaya ya Namtumbo wamekuwa wakitegemea umeme walioahidiwa na Serikali wa *Grid* utakaounaganishwa kutoka Makambako na ni muda mrefu sana na inategemea mradi huu utachelewa kuanza na nimekuwa nikizungumza na Wizara kuhusu kuomba kama wanaweza kutupatia kwa kuanzia umeme wa *Generator* kwa mji wa Namtumbo.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza kuwaeleza Wananchi wa Namtumbo utaratibu huo umefikia wapi wa kupatiwa umeme wa *Generator* ya kuanzia na Wilaya ya Namtumbo?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimtoe wasiwasi kwamba kweli mradi wa Makambako Songea umechelewa kidogo.

Lakini yale mambo yaliyokuwa yanafanya ule mradi uchelewe yameshamalizika, kulikuwa na masuala ndani ya Wizara ya Fedha na Wizara yetu na wale wafadhili wakuu wa Sweden lakini jambo lile limeshakwisha na kusema kweli sasa tunasubiri kuanza utekelezaji wa awali. Kwa hiyo, mradi huo umechelewa kidogo badala ya labda mwaka 2012/2013 kwa sababu ni mradi mkubwa unaweza ukafika mwaka 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kuzingatia hayo ndiyo tunaomba tunamhakikishie Mheshimiwa Vita Kawawa kwamba katika Bajeti ya mwaka huu tunafanya utaratibu hatuwezi tukaacha wananchi wa Namtumbo wanakaa miaka mitatu wakisubiri umeme huo wa grid unatoka Makambako.

Kwa hiyo, tumefanya utaratibu pamoja na maeneo ya Wilaya mpya kama Wilaya ya Nyasa na Wilaya ya Mbozi Magharibi na kadhalika, hizi Wilaya mpya ambazo hazina umeme pia tunatarajia kwamba tuziweke kwenye mfumo amba mwaka huu zitapatiwa umeme. Kwa hiyo, kwa sasa hivi tathimini imefanywa na kwamba kwa pale Mji wa Namtumbo pana Ofisi ya Serikali, pana Hospitali na kadhalika. Utawekwa umeme

ambao utakidhi mahitaji kwa muda wa miaka miwili kabla hatujafikisha umeme wa grid. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Vita Kawawa kwamba jambo hili linafanyiwa kazi tayari liko kwenye mpango wa Serikali na naamini kwamba mwaka huu wa fedha linaweza likakamilika *inshallah*. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Maswali ya Wizara ya Nishati na Madini ni mengi kwa kweli yamechukua karibu robo saa, Wizara moja. Tuendelee sasa na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Tusameheane Waheshimiwa Wabunge.

Na. 227

Kutotambulika kwa Leseni za Uvuvi Kutoka Tanzania – Zanzibar

MHE. AME PANDU AME aliuliza:-

Wavuvi wa Tanzania Zanzibar wanapokuja kwenye maeneo ya Tanzania Bara kama Bagamoyo, Somanga na kadhalika, wakiwa na leseni za kutoka Tanzania – Zanzibar hulazimika kukata leseni nyingine huku Tanzania Bara kwa sababu hawazitambui Leseni za Uvuvi waliozotoka nazo Tanzania - Zanzibar.

Je, kwa nini leseni za uvuvi kutoka Zanzibar hazitambuliwi na kwa kutozitambua leseni hizi si kuwanyanya wa uvuvi kutoka Tanzania - Zanzibar?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ame Pandu Ame, Mbunge wa Nungwi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uvuvi siyo la Muungano na hivyo shughuli za uvuvi Tanzania Bara zinasimamiwa na Sheria ya Uvuvi Namba 22 ya mwaka 2003 pamoja na Kanuni zake za mwaka 2009 na kwa upande wa Zanzibar Sheria ya Uvuvi Na. 8 ya mwaka 1988. Sheria hizi zinalenga katika matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu wavuvi kutoka Tanzania - Zanzibar wamekuwa wakija kuvua Tanzania Bara kwa utaratibu maalum unaofahamika kama Uvuvi wa Dago. Uvuvi wa dago ni utaratibu wa uvuvi wa kuhama hama na kuweka kambi eneo la uvuvi kwa vipindi viwili vya miezi mitatu mitatu kwa mwaka. (*Makofi*)

Kutokana na tabia ya kuhama kwa wavuvi hao na pia kuwepo kwa sheria mbili tofauti kumekuwepo na usumbufu katika kusimamia kikamilifu shughuli za uvuvi wa dago.

Kwa kuliona hilo, Wizara yangu na Wizara inayosimamia uvuvi Tanzania Zanzibar, yaani Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira zimekublaiana kuwahudumia wavuvi wa dago kwa utaratibu ambao wavuvi kutoka upande mmoja na Jamhuri wanapohitaji kufanya uvuvi kwenye maji ya upande mwingine wa Jamhuri hutakiwa

kuonesha leseni zao halali za uvuvi na barua ya utambulisho kutoka kwa Afisa Uvuvi wa Wilaya anapotoka na kuwasilisha kwa Afisa Uvuvi wa Halmashauri anakotarajia kuvua. Afisa Uvuvi wa eneo linalopokea wavuvi wa dago hukagua na kuhakiki nyaraka na zana zitakazotumika na kuwaelekeza wavuvi hao sehemu watakazovua. Aidha, kwa uvuvi mwingine ambao sio wa dago, mvuvi inabidi kutekeleza masharti yaliyoko kwenye sheria husika ambapo inamtaka kukata leseni kamili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mvuvi ye yeyote anayezingatia masharti ya kuvua kwa utaratibu wa dago hawajibiki kuwa na leseni mbili za uvuvi na hawezi kusumbuliwa wakati akifanya shughuli za uvuvi kwenye maeneo ya uvuvi nchini.

MHE. AME PANDU AME: Mheshimiwa Mwenyekiti, Je, Serikali zetu mbili hazzioni kuwa sasa ipo haja ya kuweka sheria hii kuwa ni moja ili kuwaondolea wananchi wetu usumbufu ikionekana inafaa?

Swali la pili, je, hayo masharti ya uvuvi ni yepi na hawa wavuvi wanayajua?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba tungelipenda kwamba sheria moja itumike lakini lazima tutambue kwamba suala la uvuvi siyo la Muungano. Kwa hiyo, nahitaji mpaka Katiba itakapobadilika na kulibadilisha suala hili kuwa la Muungano ndio hivyo inaweza kuwezekana kuwa na sheria moja ya uvuvi. Lakini kwa sasa sheria mbili itabidi ziendelee kutumika.

Kuhusu swalii la pili kwamba ni utaratibu gani unaotumika kuhusu uvuvi wa dago. Utaratibu huu uliwekwa mwaka 2001 mwezi wa Januari wakati Wizara mbili za uvuvi zilipokutana kule Zanzibar. Kwanza kabisa mvuvi anatakiwa kuwa na leseni ya uvuvi iliyo hai inayotolewa na Mamlaka inayotambulika kisheria kwenye eneo analotoka.

Pili, mvuvi anatakiwa kuwa na barua ya utambulisho kutoka kwenye eneo alilopewa leseni ya kuvua.

Tatu, mvuvi anapofika kwenye Wilaya anakusidia kuendesha uvuvi wa dogo anatakiwa kutoa taarifa kwa Afisa Uvuvi wa Wilaya husika na kuonyesha nyaraka zote, leseni na barua ya utambulisho pamoja na chombo, zana, wavuvi aliofuatana nao na kadhalika.

Nne, Afisa Uvuvi wa Wilaya wa mvuvi anayehamia wa dago anawajibika kukagua nyaraka, chombo pamoja na idadi ya wavuvi watakaohusika katika uvuvi huo.

Tano, Afisa Uvuvi akisharidhika anawajibika kuwaonyesha eneo watakaokuwa wanavua pamoja na kufuatilia kwa karibu mienendo ya wavuvi hao. Kwa hiyo, kinachotakiwa hapa ni kwamba kabla mtu hajatoka kule Zanzibar ama anayetoka Tanzania ahakikishe kwamba anapitia Ofisi za Uvuvi ambapo Afisa Uvuvi atamwelekeza masharti haya ili wakija hapa wasisumbuliwe. (*Makofî*)

NMB Kufungua Tawi la Benki Bumbuli – Lushoto

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wa Jimbo la Bumbuli hasa wale wanaolima chai wana kipato cha kila mwezi na kwamba kila mwezi wastani wa shilingi 100 milioni hulipwa na tawi lilopo Lushoto ambalo liko kilomita 40 kutoka Bumbuli mjini:-

Je, ni lini *NMB Plc* itafungua Tawi la Bumbuli ambako kuna fedha nyingi zilizoko majumbani?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa William H. Shellukindo, Mbunge wa Jimbo la Bumbuli, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba *NMB* haina Tawi la Bumbuli. Kutohana na kuwa huduma za kibenki zinahitajika katika maeneo mengi hapa nchini, *NMB* imepanga kupanua mtandao wa matawi yake kwa kufungua matawi zaidi katika maeneo ambayo hayajafikiwa na yana uwezo mkubwa kiuchumi ikiwa ni pamoja na Bumbuli.

Hata hivyo ufunguaji wa tawi la Benki Bumbuli kutategemea siyo tu kuwepo kwa uwezo wa kifedha bali pia miundombinu na wananchi kuwa tayari kulipia huduma za kibenki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya kuwa benki zinaendesha shughuli zake kwa kuzingatia ushindani, Serikali itaendelea kuishawishi *NMB* kufungua Tawi Bumbuli kama eneo hilo linakidhi vigezo.

Serikali pia itaendeleza juhudii zake za kuboresha mazingira ya uwekezaji kwa lengo la kuwashamasisha wananchi wa Bumbuli na maeneo mengine kuanzisha benki za wananchi ambazo zikiendeshwa kwa ufanisi zitawapatia wanahisa na wananchi mapato zaidi na huduma za kibenki kutolewa kwa gharama nafuu. Namwomba Mheshimiwa Mbunge wakati tunawasubiri *NMB* kufungua Tawi Bumbuli, tushirikiane katika kuwashamasisha wananchi ili waanzishe benki ya wananchi.

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini napenda kuonyesha masikitiko yangu kwamba nadhani swalii hili halikufanyiwa mchakato wa kutosha.

Nasema hivyo kwa sababu tulishafanya mawasiliano na *NMB*, nimewaeleza miundombinu iliyopo labda wanieleze kwamba kuna miundombinu mingine ukiacha umeme watu wenye uwezo, barabara inayopitika, majengo YA mahali hapo.

- (a) Je, haoni kwamba kwa kweli kuna haja benki hiyo kwenda kule?
- (b) Kwa kuwa wakati wa kampeni za Uchaguzi na wakati *NBC* inabinafsishwa, tuliwahakikishia wananchi kwamba kuna benki yao itafika mpaka kwao vijijini nayo ni *NMB* au sera hiyo imebadilika?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE): Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali yote mawili kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishie tu Mheshimiwa Shellukindo, kwamba licha ya kwamba Bumbuli ina miundombinu yote hiyo, lakini lazima kuwepo kwa utafiti wa kina siyo kwa mazungumzo ya ana kwa ana unaweza ukawa na miundombinu lakini mzunguko wa fedha nimesema zamani kwamba hali ya mzunguko wa fedha ndani ya Bumbuli au ndani ya eneo ndiyo inayoifanya benki kuweza kuanzisha tawi pale. (*Makati*)

Lakini siyo kwamba watu wana fedha inawezekana kama watu wana fedha lakini matumizi wanayafanya nje ya Bumbuli hiyo haitawafanya Benki kufungua tawi.

Kwa hiyo, namwambia Mheshimiwa Shellukindo kwamba sera yetu ni kufungua matawi katika maeneo yote ambayo yanahitaji matawi na tutajaribu kuwashamasisha *NMB* na benki nydingine waharakishe basi kwenda Bumbuli kufanya utafiti wa kina na hatimaye kuona kama kuna haja ya kufungua matawi ya benki. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, muda mdogo kweli kweli. Naomba tusogee Wizara ya Maji na Umwagiliaji.

Na. 229

Uhaba wa Maji Katika Kata ya Mikangaula

MHE. DUNSTAN DANIEL MKAPA aliuliza:-

Vijiji vilivyoko katika Kata ya Mikangaula vina uhaba mkubwa wa maji na hivyo kuwa kero kubwa kwa wananchi wa Kata hiyo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kudumu wa kuwapatia maji wananchi wa Kata hiyo ya Mikangaula ili waondokane na kero hii ya uhaba wa maji inayowakabili?

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dunstan Daniel Mkapa, Mbunge wa Nanyumbu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Julai, mwaka 2007 Wizara yangu kwa kushirikiana na TAMISEMI ilianza utekelezaji wa programu ya maji na usafi wa mazingira vijiji kwa kutekeleza miradi inayoleta matokeo ya haraka kulingana na mipango na vipaumbele vya kila Halmashauri.

Kati ya mwaka 2006/2007 na 2008/2009, Serikali ilitumia shilingi 610,402,400 kwa Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu pamoja na mambo mengine kukarabati visima vya maji katika vijiji vya Lowasa, Chang'ombe, Nangaramo na Nawaje katika Kata ya Mikangaula na ambayo ina vijiji 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na jithada za kuwapatia wananchi wote wanaoishi mijini na vijiji kwa kupitia katika utekelezaji wa programu na usafi wa mazingira ambayo itaendelea kutekelezwa kwa awamu ambapo awamu ya kwanza inaisha mwezi Juni, 2012.

Katika Halmashauri ya Nanyumbu kwa sasa, Serikali inatekeleza miradi katika vijiji 10 vya Sengenya, Mara, Holola, Chipuputa, Ndechela, Nandembo, Ndwika, Ulanga, Chivirikiti na Lukula ambavyo vilipewa Kipaumbele na Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu, katika awamu ya kwanza.

Pamoja na utekelezaji huu Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu inaendelea kutenga fedha kwa ajili ya miradi ya maji katika vijiji vingine. Kwa mfano katika mwaka 2010/2011, Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumba itachimba kisima kimoja katika kijiji cha Mkwajuni, kata ya Mkangaula. Juhudi za Serikali katika kuwapatia maji wananchi Nanyumbu inaendelea kusaidiwa na madhehebu ya dini na asasi zisizo za Serikali ikiwa ni pamoja na Kanisa la Kianglikana Dayosisi ya Masasi. Tunashukuru. (*Makati*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Dunstan Mkapa kwa ufuataliji wake wa makini na wa karibu kuhusu masuala yanayowahusu wananchi wa Wilaya ya Nanyumba hasa katika sekta ya maji. Nanyumbu ni moja ya Wilaya ambazo upatikanaji wa maji ni chini ya wastani. Hakika Serikali itazingatia hili kama moja ya vigezo katika kutenga fedha za kuendeleza sekta ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii ya kujibu swali hili kwa niaba ya wananchi wa Rungwe Mashariki na kwa niaba yangu kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa na Chama cha Mapinduzi (CCM) kuwa mgombea wa CCM katika Uchaguzi Mkuu ujao Oktoba, 2010.

Nampongeza vile vile Dr. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais kwa kuchaguliwa na CCM kuwa mgombea wa nafasi ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. (*Makofi*)

Nampongeza sana Mheshimiwa Dr. Mohamed Ghalib Bilal Waziri Kiongozi Mstaafu, Katibu Mkuu mwenzangu Mstaafu na Mwalimu mwenzangu na Mwalimu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa kuteuliwa kuwa mgombea Mwenza wa Mgombea wa Urais kwa Tiketi ya CCM, hakika hii ni timu ya ushindi. (*Makofi*)

MHE. DUSTAN D. MKAPA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri na hasa pale waliponitajia kwamba Kijiji cha Ukwanjuni kitapatiwa maji hivi karibuni lakini nina maswali mawili ya nyongeza, kwanza, maji ni uhai, bila maji uhai haupo. Sasa kwa kuwa maeneo mengi ya Kata hii ya Mikangaula hayana maji. Je, Wizara haioni kwamba inawapunguzia umri wa kuishi wananchi hawa wa Mikangaula?

Pili, kuna baadhi ya Vijiji ambavyo vina hali mbaya sana ya maji. Kwa mfano, Chitandi, Nkoromwana, Namatumbusi, Kamundi, Kilosa, Ngalinje, Nahimba na Mkambata. Je, Wizara haioni kwamba ni vyema kuwajengea hawa watu bwawa la maji ili waweze kuondokana na kero hii ya maji? Ahsante sana.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ni uhai na sisi tulio katika sekta ya maji tunalichukulia jukumu hilo kwa uzito na unyenyekevu kama suala lenyewe lilivyo. Kwa maana hiyo, tunajua kwamba, kutowapatia maji safi wananchi kunahatarisha hata uhai wao. Kwa maana hiyo jukumu letu kama nilivyosema ni kuendelea kwa kasi na nguvu zaidi katika kutekeleza programu yetu ya maji, hasa maji Vijijini. Namhakikishia Mheshimiwa Mkapa kwamba tutalizingatia hilo hasa ukizingatia kwamba Nanyumbu ni moja ya Wilaya ambazo ziko chini kiwastani kwa maana ya upatikanaji wa maji.

La pili, ni kuhusu Vjiji alivyovitaja ambavyo ni vingi. Ninachowea kusema ni kwamba pamoja na suala lile ambalo alilizungumza wakati wa kuchangia hoja yangu nilipokuwa nawasilisha mpango na bajeti kwa mwaka 2010/2011, nimeagiza na timu inakwenda Nanyumbu kufanya kazi na Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu kuangalia jinsi gani kwanza, kuwapatia maji wanakijiji wa Kijiji ambacho mwanamama mmoja aliuliwa na tembo wakati akienda kutafuta maji. Hilo lilitugusa sana. Kwa hiyo, timu hiyo itakwenda hivi karibuni, nitawaongezea hadidu za rejea ili waangalie hali ya maji katika Vijiji vingine alivyovitaja. Ahsante sana.

MHE. CHARLES N. MWERA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi hii ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, Kata ya Mikangaula iko karibu sana na Kata ya Namatutwe, Namajani, Chiwale pamoja na Mpanyani na katika Kata hizi, kuna matatizo yaliyolingana sana na yale ya Kata ya Mheshimiwa Mkapa. Je, Waziri anaweza

kuwahakikishia nini wananchi wa Kata hizi nilizozitaja wa Masasi Magharibi ili kuondoa uhaba mkubwa wa maji ambao unawakabili kwa hivi sasa?

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika moja ya maandiko matakatifu, Mwenyezi Mungu anasema tumefanya kila kitu kuwa hai kutokana na maji. Kwa hiyo, tunalichukulia suala hili la upatikanaji wa maji, sisi si kiutendaji tu lakini vile vile kiroho kwa sababu ni wajibu mkubwa sana. Kwa maana hiyo kwa Kata zote alizozitaja hizi, kama nilivyojibu swal la Mheshimiwa Mkapa, sisi tutaendelea kufanya kazi na Halmashauri ya Wilaya ya Masasi ili kuona jinsi gani tunaweza kuwafikishia maji safi, maji salama katika umbali ulio karibu, wananchi si wa Masasi Magharibi tu bali hata wa Rungwe Mashariki na wa nchi nzima.

Lakini Mheshimiwa Mrope alitaka tu, ameshindwa namna ya kuingia kuhusu Mbwinji, naomba kutangaza kwamba leo hii mkatuba wa ujenzi wa mradi wa Mbwinji, Masasi, Nachingwea utatiwa saini hapa Dodoma, hii ni kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais Dr. Jakaya Mrisho Kikwete kwa wananchi wa Masasi na wananchi wa Nachingwea. Waheshimiwa Wabunge wa Masasi na Nachingwea hakika wakiandamana na Waheshimiwa Wabunge wa Lindi na Mtwaru mnakaribishwa saa nane na nusu katika kushuhudia utiaji saini wa mradi huu muhimu. Ahsante sana.

Na. 230

Ahadi ya Viongozi wa Kitaifa Kupeleka Maji Mji wa Tarime

MHE. CHARLES N. MWERA aliuliza:-

Kwa kuwa, tatizo la maji katika Mji wa Tarime limedumu kwa muda mrefu na kwa kuwa Rais wa Awamu ya Tatu Mheshimiwa Benjamin William Mkapa na Rais wa Awamu ya Nne Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete walihidi upatikanaji wa Maji, je, ni lini ahadi hiyo ya viongozi wa Kitaifa itatekelezwa ili wananchi wa Tarime Mjini waondokane na kero hiyo ya maji?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swal la Mheshimiwa Charles Nyanguru Mwera, Mbunge wa Tarime kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu inatekeleza programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji katika maeneo ya Vijijini na Mjini nchini. Chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Musoma Mjini ambao ni kiongozi wa *cluster* ya Musoma tunaita Mji wa Tarime ni mionganoni mwa Miji iliyowekwa kwenye programu hiyo. Mhandisi Mshauri ambaye ataajiriwa na Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka, Musoma ndiye atakayefanya usanifu, uandaaji wa vitabu vyta zabuni na usimamizi wa ujenzi wa mradi wa maji katika Mji wa Tarime. Matarajio ni kwamba kazi ya usanifu itaanza kabla ya Septemba, 2010. Matarajio yetu ni kwamba atafanya kazi hiyo kwa

maana ya kuangalia upatikanaji wa maji katika Mji wa Tarime uwe wa uhakika mpaka ifikapo mwaka 2032.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni imani yangu kuwa mradi huu mkubwa ukikamilika, wananchi wa Tarime Mjini wataondokana kabisa na kero ya maji na sisi tutakuwa tumetekeleza kwa dhati ahadi za Viongozi wa Kitaifa za kuondoa tatizo la maji katika Mjini wa Tarime.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango wa muda mfupi mwaka 2008 Serikali ilituma shilingi milioni 225 kwenye Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Mjini Tarime. Fedha hizo zilitumika kwa :-

- (a) Kununua na kufunga mabomba 800 ya *PVC* yenye kipenyo cha inchi sita;
- (b) Ujenzi wa tanki lenye mita za ujazo 225;
- (c) Ununuzi wa mtambo wa kusukuma maji (*surface pump*); na
- (d) Ununuzi wa pikipiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa mabomba, mitambo ya kusukuma maji na pikipiki vimeshanunuliwa. Pia, ujenzi wa tanki lenye mita za ujazo 225 umekamilika. Aidha, kulikuwepo na ucheleweshaji wa utekelezaji wa mradi kutokana na suala la fidia kwa wananchi wenye mashamba ambapo mabomba ya maji yamepitishwa. Suala hili tayari limeshughulikiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Tarime na hivi sasa utekelezaji wa mradi unaendelea vizuri na kazi inatarajiwu kukamilika mwisho wa mwezi huu wa Julai, 2010 na niseme hii kwa upande wa Tarime ni utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa upatikanaji wa maji ni kiu sio tu ya Tarime bali ya nchi nzima ikiwa ni pamoja na Rungwe, nachukua fursa hii adimu kuwashukuru tena wananchi wa Rungwe Mashariki kwa umoja wao, mshikamano wao na maendeleo makubwa waliyofikia ikiwa ni pamoja na imani kubwa waliyoonesha kwangu, niko tayari na nitaendelea kuwatumikia kwa juhudhi na bidii kwa kadri Mwenyezi Mungu atakavyonisaidia. Nakushukuru.

MHE. CHARLES N. MWERA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza niwashukuru Halmashauri ya Wilaya ya Tarime chini ya uongozi wangu tulivyoshirikiana katika kuwalipa fidia wananchi wale wa Tarime pamoja na majibu mazuri ya Waziri yenye matumaini, nataka nipate sababu zippi zilizochelawesha huo mradi kuanza kwa wakati?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa miradi hii ni kwa mbinu shirikishi kwa maana kwamba tunategemea sana ushirikiano wa Halmashauri, pale ambapo tunatekeleza miradi hii. Kwa maana hiyo,

iwapo kumetokea na ucheleweshaji katika utekelezaji wa mradi wa Tarime, jukumu hilo analolibeba ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Pazuri hapo, asante sana Mheshimiwa Waziri. Waheshimiwa Wabunge wote, sasa ni wakati wa kuwatambulisha wageni wetu waliofika hapa Bungeni asubuhi ya leo. Naanza na wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa John Chiligati ambao ni wazee wa CCM kutoka Kata ya Sanza, Manyoni, wale wazee wa CCM hebu wasimame pale walipo, karibuni sana wazee, yupo mzee Mathias Mafande, kiongozi wa msafara, nyoosha mkono. Ahsante. Yuko Mzee Pius Chakutwanga, Mzee Mkoka, Mzee Ibiga, Mzee Vemwe, Mzee Maroda, Mzee Malende, yuko Mzee Malolo, Mzee Manyehe, Mzee Mazoho, Mzee Ndahani, Mzee Mabwahi, Mzee Matonya na Mzee Tarimo. Karibuni sana wazee wangu. (*Makofi*)

Wako wageni wa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundı, Mheshimiwa Mwantumu Mahiza nao ni kutoka Kituo cha Utafiti wa Zao la Mhogo Duniani ambao ni Dr. Peter Hatman, ni Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi hiyo, Makao Makuu yako Ibadan, Nigeria, huyu ni Mtanzania mwenyeji wa Tanga, tunyooshe mkono; hongera sana. Tupelekee salamu huko Ibadan. Pia yupo Dr. Victor Manyong, Mkurugenzi wa Taasisi hiyo Kanda ya Afrika ya Mashariki na Kati, ahsante sana. Dr. Edward Kanju, Mtafiti wa Zao hilo la Mhogo, karibu sana Daktari. Yuko Ndugu Catherine Njugune, Afisa Mawasiliano na pia yuko Bernadeta Majebèle, Mtafuta Masoko wa Zao la Mhogo Tanzania. Ahsante sana, karibuni sana. Wako wageni wa Mchungaji Luckson Mwanjale, ambao ni Ndugu Shukuru Mwakambanga, huyu ni mjomba wake na ni mfanyakishara Dar es Salaam, karibu sana. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Mkiwa Jecha na Mwadini Jecha ni Bwana Jafari Juma Yussuf, Mwenyekiti wa *CUF*, Kata ya Kirumba Mwanza na Mheshimiwa Abdul Kitogo, Mjumbe wa Baraza Kuu Vijana, *CUF* Taifa. Karibuni sana Dodoma. (*Makofi*)

Kuna pia wageni wa Mheshimiwa Charles Keenja ni Ndugu Loitina Fales, Katibu wa Mbunge pia ni Katibu wa Umoja wa Vijana, Kata ya Kimara, Loitina, ahsante sana, karibu sana, tunashukuru sana kwa kumsaidia kurahisisha kazi zake. Ndugu Geofrey Mshana, Katibu wa CCM Tawi la Kimara Bi. Faustin Mawanja, Katibu wa siasa na uenezi, Kimara Matangini; Aziza Muhenzi, Mjumbe wa Kamati ya Utekelezaji UWT, Kata ya Kimara, Mjumbe wa Serikali wa Mtaa na Johari Lugenge, Mjumbe wa Serikali ya Mtaa, Kimara Matangini ambae pia ni Mjumbe wa Halmashuri Kuu ya Kata ya Kimara. Karibuni sana. (*Makofi*)

Vile vile kuna wageni wa Mheshimiwa Felista Bura ambao ni watoto wake Gerald Bura, Yussuf Bura, Lilian Bura, Gerald Charles na Peter Anderson. Karibuni sana watoto wa Mheshimiwa Bura, mama anafanya kazi nzuri sana hapa Bungeni na kwa mara nyingine niwaombe akinamama wa UWT, Mkoa wa Dodoma msimsahau Mheshimiwa Bura. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Herbert James Mtangi ni walimu saba kutoka shule ya sekondari Misozwe, lakini vile vile shule ya msingi ya Misozwe na shule ya Msingi ya Manyoni, karibu sana walimu. Pia wako Wajumbe watatu wa umoja wa Vijana, Wilaya ya Muheza, wale watatu nyoosheni mikono, ahsanteni sana. Pia wapo Viongozi wa Serikali za Vijiji vya Kibanda na Masuguru, Wilaya ya Muheza. Mheshimiwa Mtangi anafanya kazi kubwa hapa Bungeni. (*Makofi*)

Pia kuna wageni wa Mheshimiwa Shally Raymond, ambaao ni Kambarage Julius Nyerere, huyu ni mtoto wa Mheshimiwa Makongoro Nyerere ni mjukuu wa Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, hebu simama tena Bwana, hujaonekana. Huyu ndio amechukua majina yote matatu ya Mzee, Kambarage Julius Nyerere, karibuni sana natumaini utafuata nyayo za Mzee wetu. (*Makofi*)

Vile vile kuna wageni wa Mheshimiwa Bakari Shamis Faki ni Amdan Rashid Mwinchande, Mwenyekiti wa *CUF*, Wilaya ya Mafia na Ndugu Moshi Muhunda, mke wa Mheshimiwa Adam Rashid, Mjumbe wa Serikali ya Kijiji cha Kilindoni Mafia, karibuni sana. (*Makofi*)

Wapo wageni wa Mheshimiwa Emmanuel Luhahula ni Joseph Wanka, kaka yake, karibu sana. Sara Salvatory mwanachuo, Chuo Kikuu cha Mzumbe na Ndugu Mkami Tumbu anasomea Ualimu Bunda, karibuni sana. Ninyi Wasukuma siku zote huwa nawaambia mkifika Dodoma magari ni mengi muwe makini kidogo. (*Makofi*)

Kuna maafisa kutoka Ubalozi wa Uingereza ambaao ni John Bradshow, yeye ni mwambata wa mambo ya siasa anayemaliza muda wake hapa nchini, karibu sana John, tunakushukuru kwa kazi njema uliyofanya katika nchi yetu; Ndugu Mike Polataiko, mwambata mpya wa siasa atakayechukua nafasi ya John Bradshow, karibu sana Mike na Ndugu Pascal Mayala, yeye ni Mshauri wa Mambo ya Siasa katika Ubalozi huo. Tunakikosa kipindi chako cha enzi zile cha Kiti Moto. Karibuni sana. (*Makofi*)

Wanafunzi 50 na walimu watano kutoka Shule ya Sekondari Makole Dodoma. Amekuja mwalimu tu. Watakuwa wako *Basement*. Wanafunzi 30, walimu wanne kutoka Shule ya Msingi, Kiwanja cha Ndege Dodoma. Wako *Basement* pia. Ooh, ahsanteni sana, karibuni sana. Wanafunzi 30 walimu wanne toka Shule ya Msingi Uhuru, karibuni sana sana wanafunzi na walimu Bunge hili ni la kwenu. (*Makofi*)

Wanafunzi 30 na walimu wawili toka Shule ya Msingi Azimio. Hili kundi la pili, jana walikuja kundi moja na sasa wamekuja kundi lingine. Karibuni sana wanafunzi. Tunao wanafunzi 35 toka *CBE* Chuo cha Elimu ya Biashara Dodoma. Karibuni, wako upande huu. Karibuni sana *CBE*. Yuko mgeni wangu Dr. Gerald Lenjima, ni Daktari huyu, ni mdogo wangu. Karibu sana. (*Makofi*)

Naendelea na matangazo. Kuna tangazo la kikao cha pamoja kati ya Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala na Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, leo saa 7 mchana. Inatoka kwa Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mwenyekiti Kamati ya

Kudumu, Katiba, Sheria na Utawala. Naomba Kamati hizo mbili, Katiba, Sheria na Utawala na Fedha na Uchumi mkutane kwa pamoja ili kuchambua Muswada wa Sheria ya Ubia kati ya Serikali na Mtu au Kampuni Binafsi wa mwaka 2010. Tunaotarajia kuushughulikia kesho.

Liko tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge linasema kwamba Mheshimiwa Profesa Mwandosya, Waziri wa Maji na Umwagiliaji anawaalika Waheshimiwa Wabunge kutoka Mikoa ya Lindi na Mtwara kwenye shughuli ya kutia saini Mkataba wa mradi wa maji wa Mbwinji, Masasi, Nachingwea. Sheria hiyo itafanyika saa 8.30 mchana katika Ofisi ya Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka, Mjini Dodoma *DUWASA* leo Jumatano tarehe 14 mwezi wa Saba, mwaka 2010. *DUWASA* iko karibu na makazi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu pale.

Pia naomba niwatangazie kwamba Mheshimiwa Hassan Rajab Khatib, Katibu Msaidizi wa Wabunge wetu wa Chama cha Mapinduzi anaomba niwatangazieni kwa heshima kubwa Wabunge wote wa CCM kuhudhuria kwenye kikao muhimu sana leo tarehe 14 mwezi wa Saba katika Ukumbi ule ule wa Pius Msekwa na nasema hapa Wabunge wote wa Upinzani mnaotaka kuhamia CCM mnakaribishwa pia. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Saa ngapi?

MWENYEKITI: Leo mchana maana yake baada tu ya kumaliza shughuli zetu za mchana huu. Baada tu ya kumaliza hapa.

Liko tangazo kutoka kwa Kamishna wa Maadili. Tumelirudia rudia sana hili tangazo kuhusiana na zile fomu za maadili ambazo tunapaswa kuzijaza kisheria, mpaka jana jioni ilikuwa Wabunge 190 hawajajaza fomu hizo. Sasa na mambo haya yanakaribia mwisho ni hatari kubwa. Ningesisitiza tena Waheshimiwa Wabunge pamoja na ratiba yenu ngumu, jambo hili mlipe kipaumbele tujaze, tuziridishe haraka ili liwe limepit. Tukizidi kuahirisha inaweza ikafika mahali ukajikuta umeondoka bila kurudisha hizi, jambo ambalo si zuri. Vile vile niwaambie Waheshimiwa Wabunge ambao hawako hapa Dodoma kujitahidi kurudi kwa wakati kujaza fomu hizi na kuzirudisha kwa wakati.

Kuna taarifa kwamba Profesa Mwaikusa wa Chuo Kikuu, Kitivo cha Sheria, Dar es Salaam amepigwa risasi na kupoteza maisha. Sasa kutoptera na jina lake kutaka kufanana na jina la Profesa Mwakyusa ningeomba tu kuwaambia wananchi wa Rungwe na Watanzania kwa ujumla kwamba Profesa Mwakyusa yupo pamoja nasi na anaomba kutoa pole sana kwa familia ya Profesa Mwaikusa lakini pia kuwashakikishia kabisa kwamba Profesa Mwakyusa yupo, mzima, hajambo na ni huyu hapa Bungeni. Ahsante sana. (*Makofi*)

Tangazo la mwisho, linatoka kwa Katibu wa Bunge. Anaomba niwatangazieni Waheshimiwa Wabunge kwamba tarehe 16 Julai, 2010 kesho kutwa Ijumaa baada ya hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutakuwa na tafrija na burudani

mbalimbali kwenye Uwanja wa tafrija wa Bunge kwa ajili ya Wabunge kupata nafasi ya kuagana.

Tafrija hii itakuwa ni ya kihistoria kutokana na mambo yaliyoandaliwa kuwa ya namna ya kipekee sana. Hivyo, Wabunge wote mnaombwa kuhudhuria bila kukosa, tarehe 16 Julai, 2010 mara tu baada ya Mheshimiwa Rais kutamka rasmi kufunga Bunge hili. Baada ya matangazo haya, sasa naomba nimwite Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid ili aendeleze gurudumu hili. (*Makofi*)

Hapa (Mhe. Zubeir Ali Maulid) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea. Katibu kwa shughuli inayofuata.

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2009
(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) No. 3 Bill, 2009)

(Kusomwa Mara ya Pili)

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima naomba kuungana na familia ya Profesa Mwaikusa, Profesa wa Sheria wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambaye amepoteza maisha yake usiku wa leo kutokana na matukio ya ujambazi. Vile vile nijiunge na familia ya Jaji Mnyera na kumpa pole sana Mheshimiwa Jaji Mkuu kwa kifo cha Mheshimiwa Jaji Mnyera ambaye amefariki usiku wa kuamkia leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, naomba kutoa hoja kwa heshima kwamba Bunge hili sasa lijadili na hatimaye kupitisha Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 3 wa Mwaka 2010 yaani (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) No. 3 Act 2010*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyo ada, napenda kushukuru sana Kiti cha Spika na kupitia kwako kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wa aina zote waliomo humu ndani, kwa ushirikiano nilioupata kutoka kwao kwa kipindi chote nilichokitumikia Bunge hili. Kwa hakika nimejifunza mambo mengi sana kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge ambayo nilikuwa sijajifunza kwa maisha yangu yaliyokuwa yametangulia. Nafahamu kwamba katika mchakato wa uteuzi katika vyama vyenu vya siasa kwa ajili ya uchaguzi mkuu umeanza na unaendelea. Nawatakia kila la kheri katika uchaguzi ujao na kubwa kuwaomba kwa heshima na kwa kuwapigia magoti kuwaomba muwe mfano wa viongozi bora, viongozi waungwana, viongozi waadilifu, wasiojihusisha na rushwa, matusi au kampeni za kuwagawa Watanzania wenzetu kwa mambo ya hovyo hovyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie pia nafasi hii kutambua michango ya Mawakili wa Serikali na watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali wakiongozwa na Naibu Mwanasheria Mkoo kwa kazi nzuri wanazozifanya ambazo zimeniwezesha kufanya kazi zangu kwa urahisi na kwa ufanisi. Namshukuru sana Mwandishi Mkoo wa Sheria na Maafisa Waandishi wote wa Sheria kwa kuandaa Miswada yote ya Sheria ukiwemo huu. Nawashukuru Wakurugenzi wote wa Ofisi yangu pamoja na Wakuu wote wa Vitengo na watumishi wote wanaoonekana mbele yenu na wasioonekana mbele yenu kwa kazi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nawatambua Wachapaji, Madereva na Wahudumu ambao michango yao imesaidia kukamilika kwa kazi zetu. Bado tunayo kazi ya kuhudumia umma wa Tanzania kwa umakini na unyenyekevu na kufanya kwa kutambua kwamba kufanya kazi katika Ofisi hii ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali na Serikalini kwa ujumla sasa liwe ni jambo la kujivunia. Nashawishika kuwapongeza sana Mawakili wa Serikali kwa kuendesha kwa umahiri mashauri Mahakamani na kuzisaidia Mahakama kutenda haki ama uendeshaji mzuri wa mashauri ya madai yameisaidia Serikali kuokoa fedha za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yale mashauri mengine ya kuwashtaki wale ambao wanahuksika na mauaji ya ndugu zetu wenye ulemavu wa ngozi. Rai ni ile ile ya kawaida, vitendo vyetu vya uadilifu vitatuzungumzia kabla hatujaanza kupaza sauti zetu. Kuhusu Muswada namshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Katiba na Utawala, Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa na kupitia kwake Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hiyo kwa ushauri wao wakati wa kupitia na kuujadili Muswada huu. Maoni na ushauri wao kwa kiasi kikubwa umesaidia kuboresha sana Muswada. Hii inathibitishwa na marekebisho katika Muswada kama yanavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho tulilowasilisha pamoja na Muswada hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewasilisha pia hotuba yangu ninayoisoma sasa na Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali ambao nausoma. Sheria zinazofanyiwa marekebisho kama zilivyo kwenye Muswada, naomba zionekane kwenye *Hansard* na kwa sababu kila Mbunge ana nakala ya hotuba yangu, nadhani sina haja ya kuzisoma. Sheria hizo ni *The Electronic and Postal Communication Act, No.3 of 2010, The Mining Act, No.14 of 2010, the Employment and Labour Relations Act, Cap.366, the Labour Institutions Act,Cap. 300, the Election Expenses Act, No.6 of 2010, the National Elections Act, Cap.343, the Local Authority (Elections) Act, Cap.292, the Road Traffic Act, Cap. 168, the Local Government (District Authorities) Act, Cap.287 and the Local Government (Urban Authorities) Act, Cap.288* .

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sheria ya Mawasiliano ya Elektroniki na Posta Na. 3 ya mwaka 2010 inapendekezwa kufutwa na kuandikwa upya kifungu cha 26, kama ilivyo kwenye kifungu cha (4) cha Muswada. Kwa mujibu wa mabadiliko haya Kampuni zinazohusika na masuala ya mawasiliano ya elektroniki na posta sasa yatatakiwa kuuza hisa kwa wananchi kupitia soko la hisa baada ya miaka mitatu kuanza kutumika kwa Sheria ya Mawasiliano ya Elektroniki na Posta ya mwaka 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa masharti haya inapendekezwa kumpatia Waziri mwenye dhamana mamlaka ya kutunga kanuni zitakazoweka ufanuzi kuhusu viwango vya chini vya hisa na utaratibu utakaotumika katika uuzaji wa hisa hizo kwa wananchi. Katika kufanya hivyo masharti ya Sheria ya Mamlaka ya Masoko ya hisa na Dhamana yaani *The Capital Markets and Securities Act*, Sura ya 79 ya Sheria zetu zitatumika. Katika Sheria ya Madini Na. 14 ya mwaka 2010 inapendekeza katika Vifungu vya 5 na 6 vya Muswada kufanya marekebisho katika kifungu cha 96(iii) ili kubainisha kwa uwazi aina ya malipo ya fidia ambayo mmiliki wa ardhi ambaye atahamishwa ili kupisha shughuli za uchimbaji wa madini atastahili. Malipo hayo yatahusu pia usumbu na uharibifu wa mali au upotevu wa haki ya matumizi ya mali yake kutokana na uhamisho huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vifungu vya 7 hadi 16 vya Muswada, mapendekezo ya marekebisho katika Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini yaani Sura 396 yanafanyika katika vifungu vya 38, 67, 69, 71, 88, 91 na 93. Marekebisho haya yanalenga kuboresha utaratibu wa kutatta migogoro kazini, kwa kufafanua mambo yafuatayo:-

Yako mambo manne ukurasa wa nane. La kwanza, mkachato wa usuluhishi kabla mwajiri hajachukua uamuzi wa kumwachisha kazi mwajiriwa kwa sababu ya kutokubaliana na masharti ya kazi yaliyotolewa na mwajiri. Pili, kuruhusu Chama cha Wafanyakazi chenyé wanachama wengi kuomba jukumu la chama cha wafanyakazi kilichopoteza haki ya uwakilishi kutokana na kuwa na idadi ndogo ya wanachama ndani ya Taasisi husika. Tatu, kuruhusu upande wowote katika majadiliano, kujiondoa katika majadiliano hayo baada ya kutoa sababu za kufanya hivyo. Nne, kuruhusu usuluhishi mgogoro wa kikazi, kuandaa makubaliano yaliyofikiwa katika utatuzi wa migogoro na ambayo yatawekwa saini pande zote mbili za mgogoro huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu cha 18, cha Muswada inapendekeza pia kurekebisha Sheria ya Taasisi za kazi Sura ya 300, *Labour Institutions*, kwa kuweka tafsiri ya neno Mahakama ambayo sasa katika Sheria itakuwa na maana ya Mahakama ya Kazi. Mahakama hiyo itakuwa ni sehemu ya Mahakama Kuu na itaongozwa na Jaji ambaye atakuwa ni Mwenyekiti.

Vile vile inapendekezwa kwenye kifungu cha 19 cha Muswada kuweka masharti ya kutotoza ada kwa mashauri yatakayofunguliwa katika Mahakama ya Kazi. Aidha, yapo masharti yanayoruhusu kупендеkeза kwa mwenye mamlaka ya uteuzi kuondolewa kuwa Mshauri wa Mahakama yaani *Assessor* ambaye atashindwa kufanya kazi zake ipasavyo. Mamlaka za Uteuzi za Ushauri wa Mahakama hiyo zimetajwa kwenye kifungu cha 53 cha Sheria ya Taasisi za kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 23 cha Muswada kinabeba mapendekezo katika Sheria ya Gharama za Uchaguzi Na. 6 ya 2010 yanayohusu kubadilisha masharti ya kifungu cha 9(i) ili kuwataka watu walioleuliwa kuwa wagombea wa nafasi ya Rais,

Ubunge au Udiwani kutoa tamko la gharama watakazotumia katika uchaguzi siku saba baada ya uteuzi wao, badala ya siku tano kabla ya siku ya uteuzi ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mgombea atafahamu kwamba haya yamefanyika kwa kura, mgombea atafahamu ameteuliwa baada ya siku ya uteuzi na italeta maana iliyokusudiwa kama atatoa tamko hilo baada ya kuteuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 20 cha Sheria hiyo kinafanyiwa marekebisheso kwa kuzingatia marekebisheso ya kifungu cha 9(i) kwa kuongeza neno linalomzuia mgombea anayepatikana na kosa la kutotaja matumizi kuendelea kushiriki katika uchaguzi kama inavyoonyeshwa katika kifungu cha 24 cha Muswada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rekebisheso la mwisho linalofanywa kwenye kifungu cha 24 ni kwa kukifuta kifungu kidogo cha kwanza na kuorodhesha upya vifungu vidogo vilivyobaki kama inavyoonyeshwa kwenye Jedwali lenye marekebisheso.

Marekebisheso haya yanaondoa sharti la Vyama vya Siasa kukamilisha zoezi la uteuzi angalau siku tano ili sasa zoezi hilo likamilishwe muda wowote kabla ya siku ya uteuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili marekebisheso haya yawiane na masharti yaliyomo katika Sheria ya Gharama za Uchaguzi, inapendekezwa kufanya marekebisheso katika Kifungu cha 38(4) (d) cha Sheria ya Uchaguzi, Sura ya 343 na Kifungu cha 42(4)(d) cha Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Sura ya 292. Kwa marekebisheso haya, vifungu hivyo sasa vinafutwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisheso mengine katika sheria hizi, yanafanyika kwa kufuta na kuandika upya Vifungu vya 50(a) katika Sheria ya Uchaguzi, Sura ya 343 na Kifungu cha 52(a) cha Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Sura ya 292, ili kumpatia Msajili wa Vyama Vya Siasa Mamlaka ya kuweka pingamizi kwenye Tume ya Uchaguzi kwa lengo la kumuondoa katika mchakato wa uchaguzi mgombea ambaye amekiuka Sheria ya Gharama za Uchaguzi, kufuatia pingamizi lililowekwa na Msajili wa Vyama vya Siasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisheso katika Sheria ya Serikali za Mitaa, Mamlaka za Wilaya, Sura ya 287, yanafanyika ili kuongeza Kifungu cha 178 (a) ambacho kinampa Waziri mwenye dhamana, Mamlaka ya kuvunja Mabaraza ya Halmashauri. Inapendekezwa kuwa Mabaraza hayo yavunjwe siku saba kabla ya tarehe ya kuvunja Bunge, ili kupisha kampeni kwa wagombea wa nafasi ya Udiwani katika Uchaguzi Mkuu kuanza. Kwa madhumuni hayo hayo, inapendekezwa kufanya marekebisheso katika Sheria ya Serikali za Mitaa, Mamlaka ya Miji, Sura ya 288, kwa kuongeza Kifungu cha 84(a). Marekebisheso haya yanabainisha kwamba katika kipindi ambacho Mabaraza ya Halmashauri yatakuwa yamevunjwa, Kamati zilizoundwa na Mabaraza hazitaruhusiwa kuanzisha au kubadilisha mradi wowote ulioanzishwa kabla Baraza halijavunjwa. Aidha, inapendekezwa kurekebisha Kifungu cha 16 kwa kuongeza kifungu kidogo cha sita na cha saba kwa lengo la kumpatia Msajili wa Vijiji, Mamlaka ya kutangaza orodha ya mitaa iliyosajiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa Mabaraza ya Madiwani yamevunja kwa mujibu wa masharti ya Kifungu cha 4(i)(a) na Kifungu cha 173(c) cha Sheria iitwayo *The Local Government District Authorities Act, Chapter 287 (as revised in 2002)*. Waziri mhusika amevunja Mabaraza hayo kwa kutumia vifungu hivyo na akatoa Tangazo la Serikali Na.241 la 2010, yaani *The Local Government Urban Authorities Suspension of Councils and Committee Meetings Order 2010*. Tangazo hilo ni la terehe 2 Julai, 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho katika Sheria ya Usalama Barabarani, Sura ya 168 yanafanyika ili kuongeza kiwango cha faini itakayotozwa kwa makosa yaliyomo kwenye Sheria ya Usalama Barabarani. Sababu zake ni kwamba, kutilia maanani thamani ya shilingi ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho mengine yako katika Sheria ya Pensheni ya Watumishi wa Umma, Sura ya 371. Haya yanafanyika ili kubainisha umri wa kustaafu kwa hiari na kustaafu kwa lazima kwa Askari wa ngazi za Konstebo, Koplo na Sajenti wa Jeshi la Polisi, Magereza, Uhamiaji na Zimamoto na Uokoaji. Inapendekezwa kwamba sasa umri huo uwe kama ilivyoainishwa kwenye jedwali la marekebisho ambalo Wabunge, wamegawiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho mengine yanafanyika katika Sheria ya Taifa ya Bima ya Afya, *The National Health Insurance Fund*, Sura ya 395 katika Kifungu cha 9, ili kuongeza vifungu vidogo vya tatu (3) na nne (4), kuweka utaratibu wa uchangiaji katika Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, kwa Askari Polisi, Magereza, Uhamiaji na Zimamoto na Uokoaji. Marekebisho haya yanaweka kiwango cha mchango ambapo Serikali itachangia kila mwezi katika Mfuko wa Bima, kwa ajili ya kuwawezesha Askari Polisi, Magereza, Uhamiaji na Zimamoto na Uokoaji, kutibiwa kama watumishi wengine wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho mengine yanafanyika katika Sheria ya Udhibiti wa Silaha, Sura ya 223 kwa kukifuta Kifungu cha 34(2) na kukiandika upya ili Sheria hiyo itoe adhabu kwa makosa ya kupatikana na silaha kinyume cha sheria, kufuatia kuondolewa kwa kosa hilo katika Sheria ya Uhujumu Uchumi, Sura ya 200 ambayo ilikuwa inatoa adhabu kwa makosa ya kupatikana na silaha kinyume cha sheria. Makosa haya sasa hayana adhabu. Marekebisho tunayoyawasilisha, yatawezesha Mahakama zetu kutoa adhabu pindi mtuhumiwa akipatikana na hatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho mengine yanayopendekezwa yanafanywa kwenye Sheria ya Umeme, *The Electricity Act. No.10, 2008*. Inapendekezwa kwamba vifungu vidogo vya (7), (8) na (9) vya Kifungu cha 41, vifutwe na kuweka kifungu kimoja kipyä kinachompa Waziri anayehusika na Sekta kuweka Kanuni zitakazosimamia utekelezaji wa masharti ya Kifungu cha 41(6).

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya, sasa ninapenda kupitia kwako, kuwaomba Waheshimiwa Wabunge, waujadili Muswada huu na kuupitisha katika hatua zinazofuata. Nina imani kwamba Bunge lako Tukufu litaridhia marekebisho yote

yanayopendekezwa na kukubali marekebisho haya yawe ni sehemu ya sheria ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima, ninaomba kutoa hoja.
(*Makofii*)

WAZIRI WA CHAKULA, KILIMO NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA – MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii, kukushukuru wewe binafsi, kwa kunipa nafasi hii adhimu ili nitoe maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, baada ya kukamilisha kazi ya kuchambua Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuipelekea Kamati yangu kazi ya kushughulikia Muswada huu kwa mujibu wa Kanuni ya 84(1) ya Kanuni za Bunge Toleo la 2010, tarehe 5 Julai, 2010, Kamati ilikutana Ofisi ya Bunge Dodoma na kupata maelezo ya Serikali kuhusu maudhui, madhumuni na sababu za Muswada huu, maelezo hayo yalitolewa na Mheshimiwa Jaji Frederick M. Werema, Mbunge, Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambaye alieleza kuwa marekebisho yanayopendekezwa yanalenga kuziboresha Sheria husika na kufanya utekelezaji wake uwiane na mabadiliko ya kisera na mfumo. Aidha, ili kuendana na mabadiliko hayo ya mfumo, Serikali ililazimika kuchukua uamuzi ambao utekelezaji wake unahitaji marekebisho ya sheria kama inavyopendekezwa. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Kamati iliafiki sababu zilizotolewa na Serikali na kuona umuhimu wa mabadiliko ya Sheria hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutohana na maelezo yaliyotolewa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Kamati ilipenda kujiridhisha kuhusu namna mapendekezo hayo yanavyoweza kuboresha utekelezaji wa Sheria husika. Baada ya kujadili na kutafakari kwa kina, Kamati yangu iliridhika kwamba mapendekezo hayo kwa ujumla yanakidhi vigezo vya msingi na kwamba yatasaidia kuweka sawa mambo mengi katika Sheria zitakazorekebishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maudhui na sehemu za Muswada. Kama alivyoeleza mtoa hoja muda mfupi uliopita, Muswada ulipowasilishwa kwenye Kamati baada ya Kusomwa Mara ya Kwanza, ultajwa kuwa na sehemu 13 na kwamba unapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria mbalimbali 13 kama zilivyotajwa na mtoa hoja. Mionganini mwa Sheria hizo ni Sheria ya Gharama za Uchaguzi (*The Election Expenses Act*) Na. 6 ya Mwaka 2010, Sheria ya Mawasiliano ya Electroniki na Posta (*The Electronic and Postal Communications Act*) Na. 3 ya Mwaka 2010 na Sheria ya Uchaguzi (*The National Election Act*) Sura ya 343. Katika kikao cha tarehe 5 Julai, 2010, mtoa hoja pia aliwaliwasilisha Jedwali la Marekebisho na kutoa ufanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mara ya pili sasa Serikali inaleta mapendekezo ya kurekebisha Sheria ya Gharama za Uchaguzi na Sheria ya Mawasiliano ya Electroniki na Posta tangu Bunge lilipopitisha Sheria hizi. Mara ya kwanza, ilikuwa ni tarehe 17 Aprili, 2010 ambapo katika Muswada wa Sheria ya Marekebisho, Serikali ilipendekeza kubadilisha Sheria hizi pamoja na Sheria nyingine. Jambo la msingi kuhusu mapendekezo haya, ni azma ya Serikali ya kuboresha Sheria hizo na kuweka sawa utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla, marekebisho ya Sheria zinazopendekezwa yanatokana na nia njema ya Serikali ya kusimamia Sheria za Bunge kwa ufanisi. Kamati imeridhika kuwa dhamira hii ni njema na inapaswa kuungwa mkono. Jambo muhimu la kuzingatia, ni jinsi marekebsiho yanayopendekezwa yanavyoweza kuondoa upungufu uliolengwa. Kwa maelezo haya, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali katika Muswada huu na Kamati ilitoa maoni na ushauri kwa jumla kuhusu sehemu mbalimbali za Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu matumizi ya lugha na sarufi, katika kikao cha Kamati, Wajumbe walitoa ushauri uliopokelewa na Serikali na kusababisha Muswada huu uwe katika hali hii kama ilivyowasilishwa pamoja na Jedwali la Marekebisho. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Jaji Frederick M. Werema, Mbunge, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa umakini mkubwa katika kufanyia kazi hoja zilizotolewa na Kamati yangu wakati wa kuchambua Muswada huu. Usikivu na ushirikiano wake umesaidia kuboresha mapendekezo ya Serikali kuhusu Marekebisho ya Sheria mbalimbali kama yalivyobainishwa muda mfupi uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maudhui ya Muswada, kwa ujumla Kamati ina maoni kuwa, Muswada huu utawezesha Sheria zinazorekeblishwa kuwa katika sura ya kutekelezeka kwa ufanisi zaidi kwa kuondoa upungufu uliojitekeza wakati wa utekelezaji wake. Aidha, mapendekezo ya Serikali yatawesha Sheria husika kusomeka kwa maana iliyokusudiwa na Bunge sambamba na kuendana na mabadliko ya fedha na ongezeko la uvunjifu wa Sheria. Kamati inashauri kuwa, marekebisho haya yaende sanjari na kuimarisha usimamizi wa Sheria hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na maoni hayo kwa ujumla, Kamati pia inatoa maoni yake katika maeneo mbalimbali ya Muswada wa Sheria uliowasilishwa. Mojawapo ya maeneo hayo, ni Sehemu ya Tatu ya Muswada huu hususan Ibara ya 6, inayopendekeza marekebisho ya Kifungu cha 96(3) cha Sheria ya Madini, Na 14 ya Mwaka 2010. Ni maoni ya Kamati kuwa mapendekezo haya yatazingatia ushauri uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge wakati Bunge lako Tukufu linapitisha Sheria Namba 14 ya Mwaka 2010. Aidha, mapendekezo ya Serikali yatasaidia kuboresha Sheria ya Madini na kuweka mazingira bora ya Kibiashara katika Sekta ya Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sehemu ya Nne ya Muswada huu, mapendekezo ya Serikali yanalenga kuifanyia Marekebisho Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, Sura ya 366, *The Employment and Labour Relation Act. Cap 366*. Kamati ina maoni kuwa

ufafanuzi unaofanywa wa Ibara ya 8 hadi 16 za Muswada wa Sheria tunaoujadili, unarahisisha Sheria husika pamoja na kuzingatia haki za msingi za Mwajiri na Mwajiriwa. Pamoja na hivyo, Kamati yangu inashauri kuwa, mara zote Serikali inapopendekeza marekebisho ya Sheria iongeze umakini katika kufanya hivyo ili kuepuka kasoro zinazoweza kusababishwa na marekebisho ya Sheria pale ambapo Bunge litapitisha mapendekezo hayo kuwa Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Sehemu ya Sita, Saba na Tisa, Kamati imeridhika kuwa marekebisho yanayopendekezwa kwa kuzingatia maoni kuhusu kuwianisha Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Sura ya 292, Sheria ya Uchaguzi, Sura ya 343 na Sheria ya Gharama za Uchaguzi ya mwaka 2010, ni jambo la msingi ambalo litawezesha utekelezaji na usimamizi wa Sheria kuwa rahisi na wenyе ufanisi. Aidha, kutokana na usikivu wa Serikali ya Awamu ya Nne, hoja nyingi zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge wakati wa majadiliano ya Mkutano wa Kumi na Nane wa Bunge na Mkutano wa Kumi na Tisa wa Bunge, kuhusu madaraka ya Msajili wa Vyama vyta Siasa zimezingatiwa katika mapendekezo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Ibara ya 23 inayopendekeza marekebisho katika Kifungu cha 9, kuhusu tamko la gharama watakazotumia Wagombea, kama sote tunavyofahamu, katika Mkutano wa Kumi na Tisa, Bunge hili lilifanya marekebisho yaliyolenga kuongeza siku kutoka Tano (5) hadi Saba (7), katika Muswada huu Serikali pia inapendekeza kurekebisha Kifungu kinachohusu muda wa kutoa tamko la gharama kutoka siku tano (5) kabla ya uchaguzi hadi siku saba (7). Ni maoni ya Kamati kuwa mapendekezo haya yamezingatia sana hali halisi na mazingira ya utekelezaji wa Sheria. Vilevile napenda kusema kuwa ni wazi mapendekezo haya yalizingatia majadiliano yalivyokuwa kila mara ndani na nje ya Bunge jambo ambalo linapaswa kupongezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sehemu ya Tisa na Kumi ya Muswada huu ambapo Serikali inapendekeza kuifanyia marekebisho Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura ya 287 na Sheria ya Serikali za Mitaa, (Mamlaka za Miji), Sura ya 288. Kamati ina maoni kuwa iwapo Bunge litapitisha Sheria inayopendekezwa, itasaidia sana kukabiliana na hali inayolalamikiwa. Uzoefu umeonyesha kuwa kuna malalamiko kuhusu Watendaji wachache wa baadhi ya Halmashauri nchini, kutekeleza au kubadilisha miradi mbalimbali pale Mabaraza ya Madiwani yanapokuwa yamevunjwa. Jambo hili si jema na ni kinyume na misingi ya kuwapa nguvu wananchi kujiamulia mambo yanayowahusu kwa kuitia Wawakilishi wao. Kamati yangu inaipongeza Serikali kwa mapendekezo haya. Ni matumaini yetu kuwa lengo la Serikali ni kudhibiti uanzishaji mradi mpya au ubadilishaji wa mradi wowote ulioanzishwa kabla ya Baraza kuvunjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Kumi na Mbili, kama ilivyowasilishwa kwenye kikao cha Kamati, inalenga kuongeza umri wa Askari kustaafu. Kamati ina maoni kuwa, mapendekezo haya yanaonyesha usikivu wa Serikali kuhusu maoni ya Wabunge katika Mikutano ya Bunge iliyopita. Ni kweli kuwa umri wa kustaafu kwa Mujibu wa Sheria za awali ulisababisha kuwapoteza Askari wazoefu na wenyе nguvu pale wanapostaafu. Napenda kuliomba Bunge lako Tukufu likubali mapendekezo haya ili

kuliwezesha Jeshi la Polisi, Magereza, Zimamoto na Uokoaji kuendelea kuwatumia Askari wenye uzoefu wa kutosha na nguvu katika kutekeleza majukumu yake ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuhitimisha maoni ya Kamati kuhusu Muswada huu, naomba nikushukuru tena kwa kunipa nafasi hii ili niwasilishe maoni ya Kamati yangu kuhusu Muswada huu. Aidha, namshukuru Mheshimiwa Jaji Frederick M. Werema, Mbunge, Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na wataalamu wa Ofisi yake, kwa ushirikiano na ufanuzi walioutoa kwa Kamati yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuwashukuru sana na kuwapongeza Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, kwa umakini na michango yao ya kina wakati Kamati ilipochambua Muswada huu. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kwa majina kama ifuatavyo. Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mwenyekiti, Mheshimiwa Ramadhani Athumanu Maneno, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Stephen J. Galinoma, Mheshimiwa Rajab H. Juma, Mheshimiwa Riziki O. Juma, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakari, Mheshimiwa John Paulo Lwanji, Mheshimiwa Fatma Mussa Maghimbiri, Mheshimiwa Yusuf Rajab Makamba, Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mheshimiwa Nimrod Mkono, Mheshimiwa Salim Yusuf Mohamed, Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro, Mheshimiwa Abbas Zuberi Mtemvu na Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kuwashukuru watumishi wa ofisi ya Bunge wakiwemo Makatibu wa Kamati hii, Ndugu Athumanu Hussein, Elihaika Mtui, chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge Dr. Thomas Kashililah, kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. (*Makofit*)

MHE. FATMA M. MAGHIMBI - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Napenda kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu, kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani, kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa mwaka 2010, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 86(6), Toleo la mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mie pia naomba niunge mkono wenzangu kwa kutoa pole katika familia ya Mheshimiwa Prof. Mwaikusa. Prof. Mwaikusa amenisomesha Sheria mwaka wa pili na bila ya mchango wake katika kupata Shahada ya Sheria, pengine nisingekuwa hapa mbele yenu kama Waziri Kivuli wa Katiba na Sheria. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa Sehemu ya Pili, ambayo ni *Amendment of the Electronic and Postal Communication Act, 2010*. Kifungu hiki cha 26

kinachorekeblishwa, kilishawahi kuletwa katika Bunge lako hili Tukufu lakini kilitolewa bila ya kujadiliwa, wala Bunge halikuarifiwa ni kwa nini kilitolewa. Sasa kimeletwa tena kama kilivyokuwa kimeondolewa katika *Miscellaneous* ili kufanya mabadiliko ambayo yalipendekezwa wakati ule. Kambi ya Upinzani inapenda kuelewa ni kwa nini unakuja dakika hii ya mwisho ili Waheshimiwa Wabunge wasipate muda wa kuujadili kwa kina maana asilimia kubwa ya Wabunge sasa wamekwishachoka kutokana na kufanya kazi bila ya kupumzika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yetu katika Sheria hii ilikuwa ni kwa nini wanahisa wa kizalendo (*local shareholders*) ndio walazimishwe kuuza hisa zao katika Soko la Hisa baada ya muda wa miaka mitatu tangu uanzishwaji wa kampuni na si wageni? Hisa ni sawa na mtu aliye na shamba la Kahawa, Chai Korosho, Karafuu na pia ni sawa na mfugaji anayemiliki ng'ombe, je, ni halali kuwaambia watu hao wauze mifugo yao au mashamba yao na wabakie na nusu au robo ya kile wanachomiliki? Kwa lugha yoyote itakayotumika kwa hili, bado Kambi ya Upinzani inaona kutakuwa na kasoro kubwa kwani mtu anapotafuta mbia toka nje, kuna makubaliano wanayoyafanya baina yao na hivyo kuingiza watu wengine katika biashara yao ni kinyume na hili linaweza kusababisha *local shareholders* wakafungwa na makubaliano na kujikuta wamepoteza uhalali wa kuwa wamiliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Tatu, *amendment of the Mining Act, 2010*, Kifungu cha 6 katika Muswada kinachorekebisha kifungu cha 96 cha Sheria ya Madini, maneno yanayoingizwa mwisho wa Kifungu kidogo cha 3, tunaomba neno “disturbance” litolewe, maana hawa *Investors* karibu wote ni wageni. Hivyo hata kupita karibu ya ukuta ambapo pengine pana njia ya miguu basi atasema kwanza ni *trespass* na pia ataita “disturbance” na wananchi wengi watasumbuliwa iwapo kifungu hiki hakitawekwa sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Nne, *amendment of the Employment and Labour Relations Act*, tunakubaliana na mabadiliko ya Sehemu hii ya Kifungu 38(3) isipokuwa pale inaposema “*The employer may proceed with their retrenchment*”. Kambi ya Upinzani, inapendekeza kuwa hadi pale *employer* anaposhinda ndio uachishwaji kazi uendelee. Kwa sababu wafanyakazi wakishinda basi Waajiri wanakuwa wagumu kuwalipa zile siku zao ambazo walizokuwa “*suspended*”.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Tano, *amendment of Labour Institutions Act*, Kambi ya Upinzani inakubaliana na Sehemu hii ya Tano lakini tunaona adhabu haina haja. Kulitupilia mbali shauri ni adhabu ya kutosha. Kwa sababu kisa cha mlalamikaji kuleta kesi hiyo Mahakamani basi yeche aliiona kuwa kesi hiyo ni ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Sita, *amendment of Election Expense Act, 2010*, Kambi ya Upinzani inakubaliana na mabadiliko yaliyofanywa. Lakini tuna wasiwasi na kujiuliza kwa nini Sheria hii imeshaingia katika Bunge lako Tukufu kwa mara ya tatu sasa. Je, tatizo liko kwa Wanasheria wenzetu wanaomshauri Rais?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Wanasheria wajitahidi kumshauri vizuri Rais ili Sheria muhimu kama hii isirudirudi kwa marekebishi maana wageni wanawenza

kufikiria kuwa tuna tatizo kwa Wanasheria wetu kiuwezo, jambo ambalo sio la kweli. Pia hii ni dalili ya ukosefu wa umakini wakati wa kupendekeza jambo linalosababishwa na kubana muda wa kutafakari mapendekezo kwa kina. (*Makofi*)

Mheshimwa Mwenyekiti, Mwanasheria Mkuu ni mtu makini sana na tunahakika inaisaidia sana nchi yetu, nakuombeni Watanzania hasa Wanasheria tumpe ushirikiano mkubwa akiwa ni *Attorney General* na kama kuna cheo kikubwa zaidi ambacho kinaitwa *Principal Attorney General* basi apewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Sheria hii inahitaji marekebisho makubwa na haya yaliyoletwa ni kidogo, yapo mambo muhimu ambayo kimsingi yatafanya Sheria hii iwe ngumu kutekelezeka. Pia yataweza kupigiwa kelele na wadau mbalimbali vikiwemo Vyama vya Siasa na Wabunge. Ni imani ya Kambi ya Upinzani baada ya uchaguzi wa mwaka 2010, Sheria hii itatazamwa upya na kufanyiwa marekebisho makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Tisa, *amendment of Local Government (District Authorities) Act.* katika Kifungu cha 32(1), kinachorekebisha Kifungu cha 178A, Kambi ya Upinzani, inapenda kueleza masikitiko yake kuwa Kifungu hiki leo kinajadiliwa hapa Bungeni, lakini wakati huo huo Waziri mwenye dhamana amekwisha kuvunja Halmashauri za Miji, Manispaa na Halmashauri za Wilaya kwa Waraka. Hili ni jambo la kusikitisha, kwani Serikali inaanini kuwa jambo lolote linaloletwa na Serikali ni lazima likubalike na Bunge. Au kwa maana nyiningine Serikali inaona Bunge kuwa ni *Rubber Stamp* tu, kama ilivyokuwa chini ya Serikali ya Chama kimoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inafahamu hata kabla ya rekebisho hili, Waziri alikuwa anavunja Halmashauri hizo kwa mujibu wa Sheria zilizokuwepo yaani Sheria na 7 na Sheria na 8 ya mwaka 1982 kama ilivyokuwa ikirekeblishwa mara kwa mara. Hivyo hapakuwa na sababu kabisa kuleta rekebisho hili sasa isipokuwa kuthibitisha kuwa Bunge ni *Rubber Stamp* tu. Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali kueleza kwa kina kama Halmashauri hizo zimeshavunjwa, kama hivyo ndio rekebisho hili lina maana gani hasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo, Kambi ya Upinzani inapenda kutoa masikitiko yake kuwa Waziri mwenye dhamana amevunja Halmashauri hizo bila hata kuwalipa kiinua mgongo Madiwani waliomaliza muda wao. Tunataka kuwa na uhakika, Madiwani hao watalipwa lini na kwa utaratibu gani? Pia tunataka kujua ni kwa nini Serikali inachelewesha malipo wakati inafahamu kipindi cha Madiwani ni miaka mitano kama ilivyo kwa Mbunge, ni kwa nini hawakuandaa malipo yao kama ilivyo kwa Wabunge? Aidha, Wajumbe wa Mabaraza ya Miji Midogo, nao utaratibu wa malipo yao ukoje? Kama bado haujaandaliwa, ni vyema utaratibu wa malipo yao uandaliwe kuanzia leo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo huo, kuna tafsiri kuwa kuvunjwa Halmashauri za Wilaya, Manispaa na Majiji, Serikali pia imevunja Uongozi wa Miji Midogo. Kambi ya Upinzani, inafahamu kuwa ni kweli Halmashauri za Miji Midogo

inategemea Halmashauri ya Wilaya, Manispaa na Majiji, kwa maamuzi ya Kisheria. Lakini Pia ni kweli kuwa katika utekelezaji wa shughuli za Serikali za Mitaa, kuna mambo ambayo hayahitaji maamuzi ya kisheria yanayoamuliwa na Baraza la Madiwani, yako ndani ya Sheria yenyele iliyounda Miji Midogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inauliza, je, ni kwa nini Mamlaka hizo za Miji Midogo zimevunjwa pamoja na Mabaraza ya Madiwani, wakati kipindi chao cha uongozi kinaelezwa na Sheria kuwa ni miaka mitano? Je, hii si kuvunja Sheria? Muda huo unaopotea katika kipindi cha uchaguzi utafidiwa vipi? Kambi ya Upinzani, inataka Serikali kutoa majibu ya kina katika eneo hili kuondoa utata ambaa tayari umejitokeza katika maeneo yote ya Miji Midogo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Kumi, *amendment of the Local Government (Urban Authorities) Act*, Kifungu cha 34 cha Muswada kinachorekebisha Kifungu cha 16 cha Sheria, kinaeleza kuwa Msajili wa Vijiji atakuwa na uwezo wa kukubali au kukataa mtaa wowote utakaokuwa umeanzishwa na Mamlaka ya Mji. Kambi ya Upinzani inauliza, je, kuna Msajili wa Mitaa au Msajili wa Vitongoji? Kama itakuwa ni mtu huyo huyo itakuwa ni vyema cheo hicho kiwekwe vizuri ili kuondoa utata unaoweza kujitokeza. Pia tunauliza Msajili wa Vijiji atakuwa na uwezo gani wa kufuta Mitaa ambayo iko chini ya mamlaka tofauti na Sheria tofauti (*District and Urban Authority*)? Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri atoe utaratibu unaotumiwa kwa sasa katika kujasili Mtaa, Kitongoji na Kijiji. Je, hivi vyote viko chini ya mamlaka zipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, zile zote ambazo hatukuzitaja basi ichukuliwe kwamba tumekubaliana nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini kwa umuhimu, naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba Mheshimiwa Lubeleje, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria ni kifaa muhimu katika Bunge lako Tukufu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba CCM impitishe katika kura za maoni ili angojee kupambana na upinzani mwezi Oktoba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani naomba kuwasilisha. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Fatma Maghimbii kwa uwasilishaji na kwa dua kwa Mheshimiwa Lubeleje, nadhani na mwenyewe atakuwa amenyanya mikono kuitikia dua lako. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, tuna wachangiaji watano ambaa nitawataja kama ifuatavyo, nadhani wengine pia ambaa wanahitaji kuchangia wanaweza wakaendelea kuleta kama wapo. Kwanza kabisa, ni Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto ambaye atafutiwa na Mheshimiwa Anna Abdallah, baadaye atafutiwa na Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, ambaye pia atafutiwa na Raynald Alfonce Mrope na kwa orodha niliyonayo

Mheshimiwa James Philipo Musalika naye atakuja baada ya hapo. Kwa heshima na tahadhima, Mheshimiwa Zitto tafadhali.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii, kukushukuru kwa kunipa fursa ya kuwa mchangiaji wa kwanza katika Muswada huu wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali. Napenda pia kumshukuru na kumpongeza sana Mwanasheria Mkoo wa Serikali, kwa kazi nzuri ambayo anaifanya ya kuhakikisha kwamba Sheria zetu zinatungwa vizuri na timu yake akiwemo Mwandishi Mkoo wa Sheria (*CPD*) na vijana wenzangu ambao wako pale ofisi ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali kwa kuhakikisha kwamba tunaenda vizuri. Inawezekana kabisa leo ikawa ni siku yangu ya mwisho kuchangia katika Bunge hili la Tisa, kwa hiyo, nimeona kwamba nipate fursa hii kuweza kumshukuru sana Mwanasheria Mkoo wa Serikali na watu wake kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunafanya mabadiliko ya Sheria kumi na nne, sheria mbalimbali ambazo tumeletewa hapa, mabadiliko mengi yana nia njema na nitapenda kuchangia tu kwa baadhi ya mambo. La kwanza, napenda kuishukuru Serikali kwa kusikia kilio cha Wabunge wanaotoka maeneo ambayo hayana umeme, kwa kufanya mabadiliko ya Sheria ya Umeme kwa kufuta Vifungu namba 7, 8 na 9 na kumwezesha Waziri kuweza kutoa Kanuni, kuhakikisha kwamba Kifungu namba 41(6) kinafanyiwa utekelezaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mchakato ambao ulikuwa mrefu lakini nashukuru sana kwamba Serikali na Mwanasheria Mkoo wa Serikali wameweza kusikia na kuweza kuleta mabadiliko hayo na tutayaunga mkono, tunaelewa mazingira ya kwa nini vifungu vile vililetwa. Nilihudhuria mimi vikao vyote vya Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusiana na kuweka vipengele vile, mazingira ya wakati ule yalihitaji vipengele vile na mazingira ya sasa yameonyesha kabisa kwamba vipengele vinazuia uwekezaji wa sekta binafsi katika sekta ya umeme. Kwa hiyo, napenda niwashukuru sana kwa kuwa wasikivu katika hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nitaleta jedwali la mabadiliko kuhusiana na Sheria ya Serikali za Mitaa na hasa nafasi za Madiwani wa Viti Maalum. Wabunge wa Viti Maalum kwa mujibu wa Sheria ya sasa na kwa mujibu wa Katiba kabla ya mwaka 2005, Wabunge wa Viti Maalum walikuwa wanapatikana kutokana na idadi ya Wabunge ambao kila Chama kimepata. Mwaka 2005 tukafanya marekebisho, tukabadilisha Katiba tukasema kwamba Wabunge watapatikana kutokana na uwiano wa kura ambazo kila Chama cha Siasa kimepata katika Uchaguzi Mkoo wa Wabunge na matokeo yake hayo yameongeza idadi kubwa sana hasa kwa sisi upande wa Upinzani, kura zimekuwa na thamani na umeona tumeleta Wabunge wazuri kabisa hapa maana yake katika hali ya zamani vyama kama vyetu vingekuwa na Mbunge mmoja ama wawili, kwa hiyo, haya mabadiliko yalikuwa ni muhimu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika mabadiliko yale tulisahau kufanya mabadiliko kwenye Sheria ya *Local Government* kwa ajili ya Madiwani wa Viti Maalum, wanapatikana namna gani? Kwa hiyo, sasa hivi Madiwani wa Viti Maalum wanapatikana

kwa mtindo ule wa zamani ambao Wabunge wa Viti Maalum walikuwa wanapatikana, kutokana na idadi ya Madiwani ambao kila Chama kinao kwenye Baraza La Madiwani. Kwa hiyo, ni suala la ku-reconcile tu ile *proportionality* ambayo tumeianzisha kuanzia kwenye ngazi ya Ubunge, tuishushe mpaka kwenye ngazi ya Madiwani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimeandika *Schedule of Amendment* kwa msaada mkubwa wa Wanasheria wa Bunge ili tuweze kufanya hiyo *reconciliation*. Nilishazungumzia suala hili muda mrefu na Serikali ikaahidi kwamba italfanyia marekebisho. Hiyo *amendment* inakuja, Mwanasheria Mkuu inakuja usiwe na wasiwasi imeshaingizwa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda mrefu sana nimezungumzia suala hili, kila wakati nilikuwa najaribu kuleta marekebisho hayo, Serikali ikaahidi kwamba italeta, lakini nadhani labda imeghafilika tu, kwa hiyo, ni muhimu sana kufanyika wakati huu tunafanya marekebisho ya Sheria ya Uchaguzi ili kura inayopigwa iwe na thamani. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, utaangalia hayo marekebisho, utaangalia kama yanakidhi haja za kisheria ili tuweze kuboresha demokrasia yetu katika nchi na kuhakikisha kwamba tunawapata Madiwani wa Viti Maalum kutokana na uwiano wa kura ambayo Chama cha Siasa kimepata katika ile ngazi ya Halmashauri husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, kama nilivyosema, inawezekana kabisa kwamba leo nikawa nachangia mchango wangu wa mwisho katika Bunge hili la Tisa. Napenda nitoe pongezi zangu za dhati kwa Wazee ambao wameamua kutogombea mwaka huu. Wamefanya utumishi wao kwa nchi hii, wameitumikia nchi yetu kwa uzalendo wa hali ya juu sana na sasa wameamua kutoa fursa na kutoa kijiti kwa vijana ambao wataingia katika Majimbo yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana Maseneta wawili wamezungumza, Mheshimiwa Juma N'hunga na Mheshimiwa Kimiti, Mheshimiwa Mzindakaya hakuzungumza, naye pia ametangaza rasmi kwamba hatagombea na Mheshimiwa Keenja naye pia ametangaza hatagombea. Kwa kweli mimi binafsi kipindi hiki ambacho nimekaa ndani ya Bunge, nimefanya nao kazi kwa karibu sana, wamekuwa washauri wangu wazuri sana, wote kwa pamoa na hasa Mzee Kimiti, mara nyingi yanapotokea matatizo mbalimbali, tumekuwa tukishauriana naye. Lakini la msingi ni kwamba wametekeleza wajibu wao kwa nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo ningependa nitoe salamu kwa watu ambao wameitumikia nchi yetu kwa muda mrefu ni kwamba wametuachia nchi ambayo ina imani, ina umoja, nchi *stable*, nchi ya kujivunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ifahamike ya kwamba watoto waliozaliwa mwaka 1992 mwaka huu wanapiga kura kwa mara ya kwanza. Kuna wapigakura wapya milioni tano na laki sita wanaopiga kura, yaani *first time voters* mwaka huu 72% ya Watanzania ni vijana wa umri wa chini ya miaka 29. Kuna haja kubwa sana ya kuangalia *demographic* zetu na kuweza kuona ni jinsi gani Jeshi hili ambalo linatengenezwa kwenye nchi kutokana na wazazi wetu kutuzaa na kutuingiza nchini linaongezewa uwakilishi wake.

Natoa wito kwa vijana wenzangu kwamba kazi ambayo tumeifanya, vijana tulio ndani ya Bunge hili wa pande zote mbili, yaani wa Chama Tawala na sisi wa Vyama vya Upinzani ni chachu ya vijana wengine zaidi waingie ndani ya Bunge ili tuweze kufanya kazi ya kuendesha nchi yetu. Kuna kikomo ambacho watu wanafikia, kikomo hiki sasa *generation* nyininge ipewe fursa ili tuweze kuipeleka nchi yetu mbele.

Mambo mengi sana mazuri na mabaya yametokea ndani ya Bunge hili la Tisa, napenda kusema kwamba mtu ye yeyote katika utendaji wangu wa kazi ndani ya Bunge hili ambaye kwa njia moja ama nyininge tulikwaruzana ninaomba radhi anisamehe, na mtu ye yeyote ambaye kwa njia moja ama nyininge wakiwemo Wabunge kwa ujumla ambapo wao tarehe 14 Agosti, 2007 walinisimamisha Ubunge ilikuwa ni hali ya kisiasa na mchakato wa kidemokrasia, nawasamehe wote ambao kwa njia moja ama nyininge waliweza kunikosea kwani tumefanya kazi yetu na tumetekeleza wajibu wetu.

Nawaombea kila la kheri Wabunge wote huko muendako. Kama nilivyosema kwenye mchango wangu kwa Wizara ya Miundombinu, ninapenda Bunge letu lijalo liwe na Wabunge wengi zaidi wa Kambi ya Upinzani kwa sababu kazi ambayo Kambi ya Upinzani tumeifanya katika kipindi cha miaka mitano iliyopita ni kazi kubwa sana, tumewaelimisha sana wananchi lakini pia tumewasaidia watawala kwa kuwaonyesha maeneo ambayo tunaona siyo sahihi na kuna mambo mengi sana ambayo tumeyafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko mengi sana ambayo tumeyafanya yametokana na *initiatives* za Kambi ya Upinzani ndani ya Bunge. Nawaomba Watanzania kwamba Bunge lijalo angalau theluthi ya Wabunge wawe Wabunge wa Kambi ya Upinzani. Vyovyote itakavyokuwa kama, Kambi ya Upinzani ikiwa CCM, wasiwe chini ya theluthi na kama Kambi ya Upinzani tukiendelea kuwa sisi wasiwe chini ya theluthi. Kuna umuhimu mkubwa sana wa kuimarisha demokrasia katika nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda niyaseme hayo na nitaleta *schedule of amendments* kuhusu hii ya Madiwani na nitaomba Wabunge wenzangu tukubaliane tufanye *reconciliation* kati ya Katiba yetu na Sheria ya *Local Government* ili kuimarisha demokrasia yetu. Naipongeza Serikali kwa mabadiliko ya Sheria mbalimbali ambazo wamezileta na mabadiliko ya Sheria ya Umeme ambayo Wabunge wa Kusini wamezunguzia sana na sisi ambao hatukuwa na bahati ya kupata umeme mapema tunajua madhara ya yale mambo ambayo yalikuwa yamefanyika kutokana na kutokuwa na umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na ninawashukuru Wabunge wote, Mungu atawapa kila la kheri, awajaalie, awalinde, awaepushe na mabalaa yote *inshaalah*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto. Nami naomba nichukue nafasi hii kukuhimiza tu umsaidie Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kumpatia hiyo *schedule of amendments* ambayo umekuwa unaizungumza sasa hivi.

Sasa naomba nimpe nafasi mchangiaji wetu anayefuata Mheshimiwa Anna Abdallah ambaye atafuatiwa na Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha na Mheshimiwa Raynald A. Mrope ajiandae.

MHE. ANNA N. ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi, lakini na mimi nichukue fursa hii kwanza kabisa kumpongeza Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa mabadiliko haya ambayo yameletwa mbele yetu. Mabadiliko yana faida kubwa na ninafikiri tutakuwa tumepiga hatua kabisa katika maendeleo hasa katika lile suala la umeme.

Sisi tunaotoka Mkoa wa Mtwara tunajua yaliyotukuta kwa sababu tu ya vipengele hivi ambavyo vilikuwepo katika hii Sheria, lakini sasa nina hakika baada ya kupitisha Sheria hii, matatizo yetu yatapungua kwa sababu wale wawekezaji wa umeme kwetu Mtwara wamepata vikwazo vyta kutisha kabisa. Huwezi kuamini kabisa kwamba Serikali ilipitisha Sheria ya kuwakaribisha wawekezaji kwa nia njema lakini utendaji haukuftutana na ile nia njema ilivyokuwa.

La pili, ninapenda kuzungumzia hii Sheria ya *Election Expense*, lakini nakubali zile nydingine zote. Hii Sheria ya *Election Expense* ni nzuri, lakini mimi naomba niseme kwamba kuna mambo humu hayahusiani na *Election Expense*. Ninaomba tukimaliza, watakaorudi katika Bunge lijalo wahakikishe kwamba wanaondoa utatanishi uliopo katika Sheria hii. Lakini nafurahia sana lile la 24(1) iliyofutwa ambayo sasa hivi ni 24(a). Ninaomba kusema kwamba kwanza ile 24 ya sasa inasema *Disqualification of Candidates*, nashukuru hiyo imefutwa, lakini una-disqualify candidate.

Kwanza hii *statement* iliyokuwa ni ya kushangaza tu kwamba kama chama hakita-under take and complete the nomination process within 21 days before the nomination day halafu inakuwaje? Huku kwenye marginal notes inasema: “*disqualification of candidates*”. Mimi nafikiri Sheria hii ina mambo mengi ambayo kwa mfano ku-disqualify candidate mwenyewe hii ni kazi ya Msajili wa Vyama vyta Siasa, tunagawanaje madaraka na Tume ya Uchaguzi? Tume ya Uchaguzi ndiyo kwa kweli ina haki ya kusema kwa kweli *Candidate* huyu anafaa au hafai. Lakini Msajili! Mimi nafikiri tunafanya makosa, hiyo ni kazi ya Tume.

Kwa hiyo, maudhui ya Sheria yalikuwa mazuri sana lakini tuhakikishe kwamba huko tunakokwenda hebu tuikalie vizuri tuondoe mkanganyiko isije baadaye tukapata matatizo makubwa kati ya Tume ya Uchaguzi na *Registrar of Political Parties*. Sasa kama tulikuwa tunatafuta Sheria ya kumpa yeze kazi hii inasaidia, lakini tuondoe zile closes ambazo zitatuletea mgogoro huko tunakokwenda. Lakini nishukuru hizi amendments ambazo zimebekwa pamoja na kazi nzuri iliyofanywa na Kamati yetu ya Sheria na Katiba. Kwa kweli wamefanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba tu niseme hivi, kazi ya kuboresha na kukosa Serikali humu ndani tumefanya wote wa CCM na wa Upinzani, yaani wote tumeifanya. Hakuna anayetoka humu kifua mbele kwamba yeze ndiye champion aliyeboresha kila kitu, hapana! Wote tunaondoka vifua mbele tumeifanya kazi hiyo kwa pamoja. Hata

tulipokuwa tunazungumza habari za ufisadi, wapo Wabunge wa CCM waliopiga kelele kwelikweli tena sana.

Kwa hiyo, nasema mimi nafurahi na ninashukuru lakini wapinzani watakuwa wangapi na CCM wangapi, inategemea na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM na jinsi watu wanavyoolewa siasa ya nchi. Kwa hiyo, mimi nina hakika kwamba Chama cha Mapinduzi kitashinda tena kwa kishindo, tena sio ajabu zaidi kuliko tulikotokea.

Lakini mimi linanikera sana hili la watu *ku-mention* wazee. Nashukuru, lakini pengine hawa watu wazima watafutiwe chombo ambacho kitawasaidia pia kutoa maoni yao kwa maana hiyo wasiachwe tu. Sisi tunasema wastaafu wasiachwe wakiozea tu nyumbani na mawazo yao mazuri kichwani. Lakini naomba vijana muelewe kwamba hakuna mzee aliyekwaa kisiki akaanguka akastukia yuko mzee. Uzee ni *process* unakuwa mwaka wa kwanza, wa pili mpaka unafika sabini. Kwa hiyo, lazima tuwe na *balance*, hakuna nchi itaendeshwa na vijana peke yao, kwani tunahitaji wazee. (*Makofi*)

Mimi nasikitika sana baadhi ya vyombo vya habari wanaandika kwamba wazee wang'atuke, hao wanaosema hivyo wamezaliwa na wazee hao hao. Wewe utakapokuja kuwa mzee *uta-feel* namna gani mwanao atakaposema mzee sasa toka nikurithi mimi. Sasa utamrithi na mama yako?

Kwa hiyo, mimi nasema hivi hili jambo la utu uzima ni *process*, watu wamefika utu uzima, wanaosema sisi tuondoke waondoke wao. Lakini naomba vijana msilifanye ndiyo ngoma ya kupiga wazee waondoke, mtachimba makaburi tu ya wazee. Mimi ninaona nchi hii tunahitajika wote, mimi ni mmojawapo katika hao wazee lakini tunahitajika wote. Kila mtu kwa namna yake.

Mnawaona akina Mzee Ngombale hapa, Mzee Ngombale anashindana na kijana yeoyote kwa busara na kila kitu au akina mzee Malecela. Kwa hiyo, mimi nasema hivi, wewe kagombane kwenye Jimbo, kama wewe unataka kwenda kusema usimchague huyu ni mzee, kaseme wewe kwenye Jimbo lako na watu wataamua.

Kwa hiyo, naomba hili tungeliacha. Mimi linanikera kweli kweli, inakuwa kama wazee walikosa vile kuwa wazee kumbe na ninyi mtakuja huku huku.

Lakini namshukuru sana Mheshimiwa Zitto Kabwe yeye amesema kwamba wale wanaong'atuka ahsante. Ni kweli tulikuwa tunapeana vijiti, lakini nasema hivi tafadhalini kama mzee amesema mimi nitakuja, nataka kwenda kujaribu ama niendelee. Mwachenii kwa sababu ni haki yake ya kikatiba, Katiba haijasema ukishafika miaka 60 basi, huyo sio mfanyakazi wa kuajiriwa. Kwa hiyo, mimi ndiyo nilikuwa nataka kuchangia katika hilo.

Mwisho, nasema tumefanya kazi nzuri na mimi naomba niwaombeenii wote mtakaoingia katika mchakato, kila la kheri, mrudi na ningependa idadi ikabaki vile vile na ipungue zaidi kule, huku izidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Kicheko /Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Anna Abdallah na ahsante kwa somo lako kwa Mheshimiwa Zitto na umri. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha atafuatiwa na Mheshimiwa Raynald A. Mrope na Mheshimiwa James P. Musalika ajiandae.

MHE. MWADINI ABBAS JECHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii nami kuchangia Muswada uliopo mbele yetu wa marekebisho ya Sheria mbalimbali za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimpongeze na kumshukuru Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kusikiliza kilio cha Wabunge na wadau wengine na hatimaye kufanya maarifa ya kitaalamu anayoyafahamu yeye na wenzake kutuletea marekebisho ya Sheria mbalimbali za Serikali.

Lakini kadhalika, nimpongeze kwamba mara nyingi amekuwa anajitangaza kwamba yeye sio mwanachama wa chama chochote katika nchi hii, lakini tulishangazwa juzi wakati anawapongeza wagombea wa chama kimoja tu ambacho kimefanya uteuzi wa wagombea ilhali kuna baadhi ya vyama tayari vimeshachagua wagombea. Sasa kwa kuwathibitishia hilo, kwamba yeye sio mwanachama wa chama chochote, basi atakapokuwa anakuja kufanya *winding up* ya hoja yake, basi awapongeze pia wale ambao wameshateuliwa na vyama vyao kuwa wagombea wa nafasi za Urais, Makamu wa Rais na Rais wa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichangie kidogo kuhusu suala zima la Sheria ya Umeme ya mwaka 2008. Nashukuru kwamba kuna marekebisho yameletwa katika Bunge kako Tukufu.

Wiki iliyopita wakati nachangia katika hotuba ya Mheshimiwa William Ngeleja Waziri wa Nishati na Madini, nilikuwa nazungumzia suala zima la upatikanaji wa umeme katika nchi hii, na nikasema haipendezi hata kidogo kuona katika nchi hii kuna baadhi ya sehemu wanapata umeme wa uhakika, baadhi ya sehemu wanapata umeme wa wasiwasi, lakini kuna baadhi ya sehemu katika nchi hii hawapati umeme kabisa. Nikasema ni jinsi gani juhudhi iliyochochukuliwa na Serikali kuhakikisha kwamba sehemu kadhaa au sehemu zote za nchi hii zinapata umeme wa uhakika, na kama tulitunga Sheria hapa Bungeni za kusaidia mchakato mzima wa kusambaza umeme katika nchi hii. Ila nikasema kuwa kuna baadhi ya vifungu katika Sheria tulizotunga sisi wenye kwamba zilikuwa zinakwaza juhudhi nzima ya kuiruhusu sekta binafsi kuwekeza katika suala zima la kuzalisha na kusambaza umeme katika nchi hii.

Ni dhahiri kwamba Serikali imesikia, na kwamba vifungu vile na hasa kifungu hiki cha 41(7), (8) na (9) ndiyo vilikuwa ni gumzo kubwa katika Bunge hili Tukufu kwamba ni kikwazo kinachozuia sekta binafsi kuwekeza katika suala zima la kuzalisha na kusambaza umeme. Sasa nashukuru sana kwamba leo hii imeletwa hapa tufanye marekebisho na kama alivyosema mama yangu Mheshimiwa Anna kwamba angalau watu wa Mikoa ya Kusini mwa Tanzania na sehemu nyingine za Tanzania ambazo bado

umeme ni tatizo, basi sekta binafsi itakuwa na nafasi kubwa ya kuweza kuzalisha na kusambaza umeme katika sehemu hizo sambamba na hatua za kiserikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie pia hili suala la *Election Expense Act* ya mwaka huu. Watu wengi wamezungumzia Sheria hii. Sheria hii imetungwa na madhumuni yake makubwa ni kuweka hali iliyo sawa katika uchaguzi wa nchi hii ili uwe huru na wa haki kwa mwananchi yejote katika nchi hii ambaye ana nia ya kugombea katika chaguzi za Serikali basi awe na haki sawa na mtu yejote katika kugombea na kwamba ana uwezo au wananchi watakapomkubali basi anaweza kuchaguliwa bila kujali kwamba ni mtu mwenye fedha au mwenye akili sana na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na umuhimu wa Sheria hii, Sheria hii ikafanywa haraka haraka ikaletwa Bungeni, ikajadiliwa na tukaipitisha. Lakini muda mfupi tu baada ya kusainiwa Sheria hii makosa kadhaa yaligundulika, wadau wameyaona makosa hayo, vyama vya siasa ambavyo ndiyo wadau wakubwa wakagundua makosa hayo, sisi Wabunge pia tukagundua makosa mengi tu. Kwa hiyo, tukajadili tena Sheria hii na hata Kanuni zake ambazo zilikuwa zimetungwa za Sheria hii zikaonekana kuna makosa mengi ambayo kwa kweli yasingeweza kufanya Sheria hii itekelezeke kirahisi na kuweza kutoa haki kwa kila mtu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, pamoja na kwamba marekebisho haya ambayo yameletwa hayatoshelezi hasa kuiweka sawa Sheria yenewe, ni dhahiri kwamba wakati inatumika Sheria hii kutajitokeza makosa mengine madogo madogo ambayo yatahitaji kufanyiwa marekebisho hapo mbeleni. Sasa nimiraharishe tu kaka yangu Mheshimiwa AG kwamba kadri tutakavyoitumia Sheria hii kutajitokeza mengi na kwa hiyo, Serikali iwe tayari kurekebisha Sheria za nchi ili chaguzi zetu ziwe za huru na haki na iwe ni mfano kwa Afrika na kwa dunia.

Ila pia naomba Serikali kwamba Kanuni zenyewe zinazoongoza matumizi ya Sheria hii na kwa sababu uchaguzi wenye hauko mbali, basi zitengenezwe haraka haraka zichapishwe kwa wingi na tusambaziwe wadau wote ili tuweze kuitumia na isije ikawa ni kikwazo kwa watu wengine kwamba wanakwazwa na Sheria yenewe kutokana na kutopatikana kwa Kanuni za Sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa najaribu kupitia *Schedule of Amendments* aliyoiwasilisha Mheshimiwa Zitto Kabwe. Kwa haraka haraka nimeiona na kuilewa kwa kiasi fulani na nimeona kwa kweli ni marekebisho ambayo yanahitaji kila mmoja wetu ayape msisitizo. Ni marekebisho ambayo kwa kweli yanatoa haki kwa wadau wote wa siasa na wote ambao wataingia katika chaguzi hizi ambazo tunaelekea hapo mbeleni. Hivi viti maalum ambavyo alikuwa anavizungumzia, kwa kweli kwa sasa hivi uteuzi wake naweza kusema bado haujaka sawa na kwa mapendekezo ambayo yameletwa na Mheshimiwa Zitto ni mapendekezo mazuri na Serikali iangalie vizuri ili tuweze kuya-adopt mapendekezo hayo iwe ni sehemu ya mawasilisho ya leo.

Sasa baada ya kusema hayo nichukue nafasi hii kuwapongeza sana wananchi wa Jimbo langu la Wete, nimekaa nao miaka karibu saba na nusu katika ubunge, nusu ya

Bunge la 2000-2005 na miaka miaka mitano ya Bunge la 2005-2010. Nimekaa nao na nimewatumikia kwa kadri Mwenyezi Mungu alivyonijaalia. Ni matumaini yangu kwamba sikuwaangusha katika kuwawakilisha katika Bunge hili na kwa hiyo, niwatakie kila la kheri na *inshaalah* Mwenyezi Mungu awajaalie atakayojaalia ili maendeleo ya Jimbo letu yasonge mbele kulingana na matakwa ya chama changu, lakini pia matakwa ya wananchi wenyewe.

Aidha, nichukue nafasi hii kwa sababu binadamu kama binadamu kama alivyotangulia kusema Mheshimiwa Zitto, ni kwamba binadamu wanapokaa sio kama vikombe, hata vikombe vinagongana. Tumekaa huu muda mrefu sana, mimi nasema kwamba siku zote nimejifunza mengi kutoka kwenu Wabunge wenzangu, nilikuwa najihisi kama nimo katika familia ya watu tuliozaliwa tumbo moja kwa muda wote. Niwashukuru sana kwa msaada wenu, kwa maarifa yenu, na kwa uelekezi wenu. Yeyote ambaye katika uhai wa utumishi wa Bunge letu nimemkosea, mimi ni binadamu ama kwa kukusudia au kwa bahati mbaya, tunakokwenda sio mbali, ni mahali pa nyanda moja tu, naomba yeyote ambaye nimemkera au nimemuudhi basi anisamehe na yeyote ambaye nahisi labda ameniudhi ingawa sifirkiri kama kuna mtu ameniudhi, basi naye pia kwa moyo safi kabisa nimemsamehe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kuwapongeza Spika - Mheshimiwa Samuel Sitta, Naibu Spika - Mheshimiwa Anne Makinda, Wenyeviti - Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Zubeir Maulid na Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa kweli kwa juhudi kubwa ambayo wameichukua katika kuliendesha Bunge hili Tukufu na ninasema kwa kweli ile azma ya Mheshimiwa Spika ya kuendesha Bunge hili kwa viwango kwa kweli tumeiona na Bunge la Tisa. Niwe muwazi kabisa, ni Bunge ambalo limeonesha viwango vikubwa, na limekuwa ni Bunge la mfano katika nchi za *East Africa*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache ninaomba nikushukuru na kwa sababu pengine leo ndiyo itakuwa mwisho wa mimi kuzungumza, niwatakieni kila la kheri nyote, na kila ambaye Mwenyezi Mungu aliywandikia kurudi katika Bunge hili, basi amjalie kurudi kwa salama na amani. Nashukuru. (*Makofii*)

MHE. RAYNALD A. MROPE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia katika hoja hii iliyo mbele yetu. Kwanza, ninataka kutoa hongera nyingi sana kwa Mwenyekiti wetu wa Chama, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa na wanachama wenzake wa CCM kwa kura nyingi mno, nampa hongera nyingi sana. (*Makofii*)

Wakati huo huo nimpe hongera nyingi sana Mheshimiwa Makamu wa Rais, Dr. Shein, naye amefanya kazi kubwa sana hapa na wana-CCM kwa kweli wakarudisha shukurani zao kwa kumpa kura nyingi ili aweze kutuwakilisha kule Zanzibar.

Mwisho pia nimpe hongera Dr. Bilal ambaye ndiye amechaguliwa kuwa Mwenyekiti mwenza.

MBUNGE FULANI: Ni mgombea mwenza, siyo Mwenyekiti mwenza.

MHE. RAYNALD A. MROPE: Mheshimiwa Mwenyekiti, mgombea mwenza. Ukiangalia safu hii ya CCM unaona moja kwa moja kwamba, ni timu ya ushindi. Ninaamini kabisa kwa jinsi watakavyotuongoza, kwanza ni wasomi tupu! Hii inatuweka katika mahali pazuri sana na kwa kweli tunataka watu wenye taaluma mbalimbali ndiyo waweze kutufikisha kule tunakotaka kufika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hii inawezekana ikawa mara yangu ya mwisho kuzungumzia hoja katika Bunge letu hili, ninaomba nitoe shukurani zangu za dhati kwa wapigakura wangu wa Masasi. Wamenilea kwa miaka hii mitano na tumefanya mambo mengi mazito. Kwa hiyo, ninachukua nafasi hii kuwashukuru sana wapigakura wa Masasi. Ninawashukuru kwa sababu kuna mambo mengi tumeyafanya pamoja. Tulikuwa na tatizo la umeme, hivi sasa umeme Masasi ni saa 24. Hayo ni mafanikio yetu sote pamoja na mimi kama Mbunge wao.

Halafu leo asubuhi mmemsikia Waziri wa Maji akisema kwamba nikahudhurie sherehe maalum za utiaji sahihi mradi wa kuleta maji kutoka Mbwinji kuja Masasi, maji ya uhakika kabisa. Kwa hiyo, mkataba ule tunaokwenda kutia sahihi, hili ni jambo kubwa na siku kuu kubwa kabisa kwa watu wa Masasi kwa sababu tulikuwa na shida ya maji, lakini sasa kutakuwa kuchele kabisa! Umeme upo, maji yapo na hayo ndiyo mafanikio makubwa ya Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete na Mbunge Raynald A. Mrope. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukurani hizi, sasa niingie katika hayo marekebisho. Mimi ninaishukuru sana Serikali kwa kusikia kilio cha Wabunge kilichohusiana na Sheria ya umeme ambayo haikukaa vizuri. Nashukuru kwamba, sheria hii inabadilishwa kwa kumpa Waziri mamlaka ya kusimamia masharti ya kifungu hiki cha Na. 41.6 na kukifuta kabisa. Kwa kweli kwa hali ya sasa hakifai. (*Makofi*)

Kifungu hiki ndicho kilichowapa masikio na nguvu kubwa *EWURA*. *EWURA* walikuwa miungu mtu kutokana na kifungu hiki. Uungu mtu huo umetuumiza sana sisi watu wa Kusini kwa sababu kule Kusini kulikuwa na mradi mkubwa wa *ORET* unaotoka Serikali ya Uholanzi. Waholanzi wametoa shilingi bilioni 45 (dola milioni 30) ili kusaidia masikini ambao hawawezi kuunganisha umeme katika majumba yao. Kwa hivi sasa *TANESCO* inatoza shilingi 475,000 kwa kuunganisha kati ya nguzo na nyumba, wakati mpango wa *ORET* ulikuwa unalenga kuwawezesha wale masikini watoe shilingi 60,000 au 80,000 tu ili kuunganishiwa umeme katika majumba yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa *EWURA* akasimama katikati akafunga breki kubwa kiasi kwamba sisi tumekosa. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, nitaomba utuhakikishie: Je, hizi fedha zilizokuwa zimepangwa zamani ili ziwanufaishe watu wa Kusini zitafika? Kwa sababu kutokana na danadana walizochezewa Waholanzi wameamua kujitoa pamoja na fedha zao, sasa tutafanyaje? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu kama ninavyofahamu mimi haina fedha za kutosha kuweza kutekeleza mradi huu kama tulivyokuwa tumepanga mwanzo. Kwa

hiyo, ninaomba sana Mwanasheria Mkuu ongeeni huko Serikalini mradi wa kuleta umeme katika mikoa ya Kusini uende kama vile ulivyokuwa umepangwa. Wakati huo huo kwa sababu *EWURA* ndio waliotukosesha mambo haya: Je, Serikali itachukua hatua gani kwa uzandiki huu wa *EWURA*? Kwa sababu zinatakiwa zipatikane shilingi bilioni 45 ambazo zilikuwa tayari zimetolewa?

Sasa danadana zao zimefanya fedha hizi tukazikosa. Naomba Serikali iwavajibishe *EWURA* kabisa kwa sababu sisi hatuwezi kukosa umeme kwa sababu ya Taasisi hii kutokuelewa wajibu wake. Mimi ninaomba Mwanasheria Mkuu wa Serikali azungumze na Serikalini ili sisi tuhakikishiwe kupata umeme kwa shilingi 60,000 mpaka 80,000. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi Waziri mwenye dhamana ya umeme ndiye atakayekuwa anatoa masharti ya mwisho. Hili ni jambo kubwa na zuri kabisa. Hizi taasisi ambazo baadaye zinaanza kuwa na mapembe hazifai na mimi ninasema katika Bunge lijalo lazima hii *EWURA* iangaliwe.

Mimi ninasema katika Bunge lijalo lazima *EWURA* ifutwe ili kuwepo na Taasisi mbili; itakayoshughulikia mamlaka ya maji, na nydingine itakayoshughulikia mambo ya umeme na madini, kwa sababu ukiunganisha zote ndiyo haya matatizo tunayoyapata. Hawa sasa hivi wako chini ya Waziri wa Maji, lakini inapofika kwenye masuala ya umeme na madini, mara nydingi wanakuwa wagumu kweli kweli kwa sababu hawahusiki moja kwa moja kwa Waziri wa Nishati na Madini.

Kwa hiyo, ninachosema ni kwamba matatizo haya tumeyaona, *EWURA* ivunjwe ili kuwe na taasisi mbili za *Regulatory Authority*. Sijui tutaziitaje, lakini mimi hili jina la *EWURA* naona life kabisa wala halitusaidii kwa kitu chochote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, nami nilitaka kusema kwamba, kwa kweli ninashukuru nimekuwa katika Bunge hili kwa miaka mitano iliyopita na nimejifunza mambo mengi na nimebobea katika mambo mengi. Mama Anna pale amekwishasema vizuri sana, ameelezea na mimi nataka kuwashakikishia wananchi wangu wa Masasi, wale ambao wanani pigia simu: Je, unasimama au vipi?

Sasa ninataka kusema kuitia hapa Bungeni kwamba, mimi ninatetea kiti changu cha Ubunge kwa pale Masasi. Afya ninayo safi sana, nguvu ninazo, sina wasiwasi, nimeyapata mambo mengi ninayoyaelewa na nimekutana na kufanya urafiki na watu wengi tu ambao wanaweza kutusaidia katika kuendeleza Masasi yetu, na kama mnavyoona hivi leo haya mambo niliyoyazungumza sasa hivi yanatokana na kuelewana na wahusika mbalimbali ili tuweze kuondoa vikwazo vile vitakavyowafanya wananchi wasiendelee.

Kwa hiyo, kwa kuitia kwangu nafikiri inakuwa ni rahisi zaidi kwa sababu unavyojenga nyumba na kuifikisha kwenye lenta, kazi inayobaki si kuezeka tu? Sasa ni nani aezeke? Yule aliyeanza kuijenga au aje tu mtu mpya asiyefahamu lolote? Hata msingi hajui namna ya kuujenga, aje tu achukue! Haiwezekani! Nyumba itajengwa, na yule aliyeanza na ndiye atawezu kuimaliza vizuri. Huyu mpya hajui lolote kwamba,

msingi utakuaje, madirisha uweke wapi na nini, kwanini tuiweke katika hatua ya namna hiyo?

Mimi ninaomba haya wananchi wa Masasi tuweze kuyasahihisha sisi wenyewe wakati tunapiga kura na nina hakika kwamba, kwa ushirikiano tulionao bila shaka mtanirudisha tena hapa ili niendelee kuwahudumia.

Hivi sasa kuna wanaopitapita huko, tunawaita wapita njia, wanasema nichagueni mimi nitaleta maji, utaleta maji kwa namna gani? Waziri hapa leo ameshasema tunakwenda kutia sahihi. Anayeweza kuleta maji pale ni Jakaya Kikwete na Raynald Mrope tu, basi. (*Kicheko/ Makofi*)

Kwa hiyo, ninawashukuruni sana wenzangu, tumekwenda vizuri, tumekaa vizuri na tuombeane kila la kheri ili mwezi Novemba tuweze kurudi tena. Nawashukuruni sana kwa kunisikiliza. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mrope. Sasa ninamwita mchangaiji wetu ambaye atakuwa ni wa mwisho sasa hivi, Mheshimiwa James P. Musalika. Simwoni. Tuendelee.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. PROF. PHILEMON. M. SARUNGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuungana na Waheshimiwa Wabunge, kumpongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa kazi nzuri waliyoifanya kwa kufanya marekebisho katika sheria mbalimbali zinazohusu fedha na kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutamka kuwa naunga mkono hoja na napenda kutoa ushauri katika maeneo yafuatayo katika muswada:-

Katika Muswada, sehemu ya tatu, marekebisho kufungu cha 8 cha Muswada ukurasa wa nne, marekebisho kifungu kidogo 124(3), nashauri kuwa Serikali iangalie tena marekebisho haya ili wananchi watumiaji simu wasibebeshwe ushuru huu kupitia makampuni kupandisha gharama ya muda wa maongezi badala ya kupunguza ukizingatia gharama ya maongezi ni kubwa ikilinganishwa na nchi jirani.

MHE. HAWA ABDULRAHMAN GHASIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshauri Waziri wa Fedha kuhusu suala la uchakachuaji mafuta. Kwa kuwa suala hili limejadiliwa sana na kwa kuwa athari zinazotokana na uchanganyaji mafuta ni kubwa sana kibashara na kiuchumi, Wizara ione uwezekano wa kuanzisha utaratibu wa vocha kwa matumizi/ununuzi wa mafuta ya taa kwa wananchi ili mafuta ya taa na *petrol* iwe sawa na hivyo kukomesha kabisa uchanganyaji wa mafuta. Ni imani yangu kuwa Serikali itatoa ruzuku kiasi kidogo sana kwenye vocha za mafuta ya taa kuliko kiasi kinachopotea kupitia uchakachuaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. SALIM H. KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Manaibu Mawaziri wake wawili, Katibu Mkuu na Watendaji wake wote kwa kazi kubwa za kuandaa bajeti ya mwaka 2010/2011. Pamoja na mapungufu yaliyojitekeza, lazima tukiri kuwa Wizara hii ni nyeti sana na sote tunahitaji kutoa msaada na ushirikiano wa hali na mali ili kuhakikisha kuwa bajeti yetu inaboreshwu mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mwaka Serikali inadai kuwa bajeti yetu ni finyu, hivyo inabidi kupunguza kwa kiasi kikubwa miradi ya maendeleo lakini tumegundua kuititia ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (*CAG*) kuwa makusanyo ya Serikali ni chini ya asilimia 50 na yale yaliyotarajiwa kukusanywa. Huu ni udhaifu mkubwa .

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwani itaifanya Serikali kushindwa kuhudumia elimu, afya, barabara na kadhalika na hili likitokea, Serikali itakosa imani na wananchi.

Pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri kukiri kuwa vianzio vyta mapato vilivyopo hawataweza kuvitumia vizuri, bado tunashauri waanze kuviangalia vyanzo vipyta vilivyopendekezwa na Kambi ya Upinzani ili kuongeza mapato na hivyo kutunisha bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha kuwa baada ya Bunge lako Tukufu kuitisha marekebisho ya Sheria ya Madini ya kuondoa misamaha ya madeni, leo Serikali inakuja na kauli ya kuendelea kuyasamehe makampuni ya madini ambayo yameweka sahihi na Serikali kabla ya Juni, 2009. Hiki bado ni kitendawili kingine. Kwa utaratibu huo, Serikali inawasaidiaje Watanzania ambao wamekosa mapato ya madini yao kwa miaka yote?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuongeza tija katika kilimo, hivyo ufanisi kwa wakulima Serikali ikazie kufufua viwanda vilivyokuwa au kubinafsishwa na ambavyo vinavyofanya kazi kinyume na ile ya asili. Haiwezekani tuzuie kusafirisha mazao ghali kama Korosho, wakati hapa nchini hakuna viwanda vyta kutosha vyta korosho vyta nguo na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MHE. SHOKA KHAMIS JUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uzima na baada ya shukrani hizi napenda nichangie muswada huu kama ifuatavyo:-

Kwanza nitazungumzia sehemu zilizosamehewa kodi. Kwa maoni yangu kutotoza ushuru katika kusafirisha maua kwa ndege kwenda nje ya nchi mimi naona faida yake ni ndogo sana kwani watu wanaofanya biashara hii ni kidogo sana. Lakini unapoongeza kodi kwenye vinywaji baridi unawaumiza wananchi wote nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu kila mwaka inaongeza kodi kwenye sigara, tumbaku, bia, vinywaji baridi na kadhalika. Ni kwa nini Serikali isitafute vyanzo vingine kila mwaka ikaleta kodi hizi hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia hivi karibuni tena Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi ameanza kuongeza kodi kwenye usajili wa magari pamoja na pikipiki na leseni za barabara, sasa Mheshimiwa Waziri aangalia sana isiwe kila mwaka ukawa unaongeza kodi kama vile unavyofanya kwenye vinywaji baridi, mvinyo, sigara na kadhalika ikawa kila mwaka unaongeza kodi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini basi Waziri hatafuti vyanzo vipyta mapema kama vile tunavyompatia Kambi ya Upinzani akavifanyia kazi mapema na ikifika wakati akawa yupo tayari badala ya utaratibu anaotumia sasa wa kutoa kodi vitu vile vile. Ahsante.

MHE. EUSTACE O. KATAGIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri wa Fedha na Uchumi na timu yake yote kwa maandalizi ya sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria ya korosho, imeendeleza na kuongeza *export levy* inayotozwa kwa usafirishaji korosho nje ambazo hazikubanguliwa, hii ni sawa na sahihi, ila hii inasaidia kidogo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka ifahamike kuwa huyu mnunuzi wa korosho, gharama ya *levy* hii anaipeleka kwa mkulima kwa kumpunguzia bei. Dawa ni kuweka masharti ya kuzuia na kushawishi uendeshaji wa viwanda hapa nchini kwa kuweka *incentives* nzuri.

MHE. MARTHA J. UMBULLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia maeneo machache ya Muswada huu wa Fedha (Sheria za Fedha).

Mheshimiwa Mwenyekiti, riba za benki kwa walipa kodi hailengi gharama za ukopaji (*cost of finance*) kwa wakopaji wenyewe kipato cha chini. Kwa mfano, haizingatii adha anayopata mkopaji tangu anapo jitayarisha kwenda benki kukopo yaani muda wake anaopoteza kupata taarifa na kufuatilia haujathaminishwa na riba inayowekwa kwenye *savings* zake anazoweka benki hailingani na riba inayowekwa kwenye mkopo anaokopa. Huu ni uonevu kwa wakopaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii iweke bayana kurekebisha mazingira hayo ili haki itendeke, mfano riba ya *savings* iongezwe na gharama za ukopaji ithaminishwe na sheria iseme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa mafuta ya kula, kwa kuwa nchi nyingi imeweka kwenye sheria za nchi zao kuwa mazao yote ya mafuta yenye kulinda afya za watu wake, hayaruhusiwi kuuzwa nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kuwa sheria hii iagize Serikali kusindika mbegu za mafuta ya kula yanayozalishwa hapa nchini ili kunusuru maisha ya

Watanzania. Baada ya kuzingatia haya, ndipo itawekwa kwenye sheria nyingine kupiga marufuku uagizaji wa mafuta yasiyofaa kwa afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naishauri Serikali kuhakikisha kuwa nishati ya kutosha hapa nchini inaelekezwa kwenye viwanda vyetu nya saruji ili Serikali iache kuagiza saruji kutoka nje. Hii ni aibu kwa nchi maskini kutoweka mikakati mizuri ya kuhakikisha viwanda vyake vinazalisha na hapo hapo tunalalamikia Pato la Taifa kuwa chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii ijikite vizuri kwenye uagizaji (*import licence*). Pia waagizaji wa mafuta ya taa wadhibitiwe vizuri ili kuagiza huko kuwe kwa manufaa ya Watanzania na siyo kwa kuhamasisha uhabiribu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kuwa leseni za waagizaji zihakikiwe kuonesha matumizi na soko la mafuta ya taa anayoagiza ni ipi.

MHE. JUMA H. KILLIMBAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkulo, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu, Naibu Makatibu Wakuu na watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Uchumi.

Meshimiwa Mwenyekiti, napongeze Serikali kwa kufanya marekebisho ya sheria mbalimbali ya kutoza ushuru wa bidhaa mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ushuru wa mazao, nakubaliana kabisa moja ya chanzo muhimu cha mapato ya halmashauri ni ushuru wa mazao, marekebisho ya sasa yanamwondolea kero mzalishaji (mkulima) kutozwa ushuru pale anapouza mazao yake, suala la sasa la kumtoza ushuru mnunuzi ni sahihi kwani yeze ndiye mtu wa kati anayepata bidhaa toka kwa mzalishaji na kutafuta soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuondoa ushuru wa uzalishaji wa saruji ili kuleta ushindani na saruji toka nje, pamoja na hayo umuhimu uongezwe kuvipa uwezo viwanda vya ndani nya uzalishaji saruji ili kudhibiti ushindani unaoweza kujitokeza kwa soko la pamoja la Jumuiya ya Afika Mashariki, kuondoa kwa ushuru kwa saruji kutaongeza ari ya wananch kufanya matumizi ya saruji ya ndani ya nchi na hivyo kuiondolea aibu Taifa kugeuzwa soko la bidhaa za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuondoa ushuru nasikitika Wizara kutokuona haja ya kuondoa ushuru wa uzalishaji wa magunia ya mkonge (*sisal bag*), yanayozalishwa na viwanda vya ndani, kuendelea kuacha ushuru kwa magunia haya kuua zao la mkonge na kudhoofisha juhudzi za kilimo ushindani wa matumizi ya magunia ya mkonge umefifishwa na magunia sasa (*duty bags*) toka ng'ambo ambayo yameingia bila ushuru na yanayo ruzuku kwa nchi zao, hivyo ingekuwa busara kwa Serikali kuzingatia suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiit, katika Bunge la Bajeti la mwaka 2009/2010 lililetwa azimio la kutaka Serikali iridhie uondoaji wa ushuru kwa magunia ya mkonge (*sisal bag*). Naomba Mheshimiwa Waziri wakati wa majumuisho anipe ufanuzi juu ya hatua hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuondoa kabisa ushuru wa bidhaa za mafuta mazito ya uzalishaji viwandani ili kuongeza ushindani katika uzalishaji wa bidhaa, suala hili ni zuri lakini lazima udhibiti uelekezwe katika kudhibiti msamaha huu maana unaweza kutumika visivyo hasa kwa viwanda dhaifu kuingiza mafuta bila kodi kwa kutumia jina la kiwanda lakini baadaye kutumika kwa biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia nafasi ya awali kabisa kutoa pongozi kwa Serikali kuitia Waziri wa Fedha na Uchumi Mheshimiwa Mustafa Mkulo, Naibu Waziri Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee, Naibu Waziri Mheshimiwa Jeremiah Sumari, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote walioshiriki kuandaa Muswada huu kwani ukitekelezwa ipasavyo utaleta tija kubwa katika kukuza uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ukusanyaji wa mapato kwenye halmashauri zote nchini, napenda kuiomba Serikali kuwa ukusanyaji wa mapato kwenye halmashauri kuitia vyanzo vyao wenye ni duni sana kwanza uwezo wa kuibua vyanzo vya mapato ni mdogo na juhudhi za ukusanyaji ni mdogo na uaminifu wa utunzaji wa mapato hayo ni mdogo. Naiomba Serikali kumtenganisha Mkaguzi wa Ndani na mwajiri wake yaani Afisa Mhasibu vile vile semina, kozi fupi na kozi ndefu zitolewe kwa wahasibu wote kwenye halmashauri ili kuongeza tija kwenye uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ukusanyaji mapato kwenye mashirika ya umma, napongeza mashirika ya umma ambayo yanajitahidi sana kuongeza makusanyo yao kwa kila mwaka. Pamoja na pongozi hizi pia napenda kutoa angalizo kuwa bado yapo mashirika ambayo makusanyo yao sio mazuri ama matumizi yao sio mazuri. Hivyo naiomba Serikali kuitia Muswada huu kutoa utaratibu upya wa kufuatwa na Mashirika ya Umma katika utumiaji wao kwani kumekuwa na taratibu tofauti tofauti za kufuata katika matumizi yao ya fedha, hii itasaidia kulinda fedha zisitumike ovyo ovyo. Sheria zifuatwe za fedha na manunuuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu matumizi ya mizani katika kuuza bidhaa, vile vile kumekuwepo na utaratibu mbaya wa uuzaaji wa bidhaa kwani wananchi wanauza mazao pasipo na bei ya pamoja na kudumu. Naishauri Serikali kuagiza halmashauri zote nchini kuhakikisha mazao yanauzwa kwa kutumia mizani ili kusaidia pia kuwepo kumbukumbu ambazo zitasaidia kupata tathimini ya kipato cha mwananchi wa chini kwa kila mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuondoa kodi kwa magari yenye *CC zero* mpaka *CC 2000*, kuwa na vyombo vya usafiri sasa hivi sio kwa ajili ya starehe tena bali

ni kwa ajili ya kuwawezesha wananchi katika kurahisisha shughuli zao mfano kubebea mazao, kwenda shambani, kuenda hospitali na kadhalika, hivyo naiomba Serikali kufuta ushuru kwa vyombo nya usafiri kuanzia *CC zero* hadi *CC 2000*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho napenda kumalizia mchango wangu kwa kuunga mkono hoja.

MHE. ZAYNAB M. VULU: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii, kuipongeza Serikali, kwa juhudhi zake za kuleta na kufanya marekebisho ya Sheria mbalimbali kwa maslahi ya nchi na wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, napenda kutoa pendekeso langu katika marekebisho ya Sheria, Sehemu ya Kumi na Mbili (*Part XII*). Sheria hii pia ingefanya marekebisho ya kutoa au kupunguza kodi katika vifungashio nya madawa ya binadamu. Serikali imetoa changamoto kwa Watanzania kuanzisha Viwanda nya Madawa ili kuleta unafuu wa bei kwa watumiaji. Tatizo dawa zinazozalishwa nchini zimekuwa ghali sana na hiyo inachangiwa pia na gharama za VAT katika vifungashio nya madawa, hatimaye mtumiaji ndiye anayeumia zaidi. Je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kwamba ni vyema kutoa VAT kwa vifungashio na kuingiza katika marekebisho haya tunayojadili leo?

MHE. FATUMA A. MIKIDADI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, ninapenda kuchukua nafasi hii, kuipongeza Wizara, kwa kuona kuwa kuna haja ya kuwa na Muswada wa Sheria ya Fedha na kufanya marekebisho kwa baadhi ya vipengele haswa sehemu ya Sheria ya Kososh, Sura 203, kwa kuongeza Kifungu cha 17A.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli mimi ninapongeza sana kukusanya ushuru kutoka kwenye korosho ghafi inayosafirishwa nje ya nchi kuitia *TRA*, pili kuongeza kiwango kutoka asilimia 10 ya sasa ya bei ya kosoro ghafi hadi asilimia 15. Vile vile kiwango cha asilimia 65 ya makusanyo yatapelekwa kwenye Mfuko wa Sekta ya Maendeleo ya Korosho (*Cashewnut Industry Development Fund*), ili yaweze kutumika kwa ajili ya kuendeleza sekta ya korosho na kuhamasisha ubanguaji wa korosho nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusipokuwa na mfuko maalumu wa kuendeleza korosho nchini, kwa kweli zao la korosho litafutika kabisa. Hivi sasa Tanzania tunakabiliwa na matatizo kadhaa ya kutoliendeleza zao la korosho kwa vile tu, halina mfuko maalumu wa kuisaidia. Mkulima wa korosho anahitaji pembejeo; miche mipya kwani hadi sasa mikorosho mingi ni mizee na haizai vizuri; kupalilia mikorosho yake ili korosho iangukie pazuri; kuendeleza zao hili kwa kuibangua korosho ili kuongeza thamani yake. Mpaka sasa, korosho yetu inasafirishwa nje nzima nzima kwani wakulima wengi hawana uwezo wa kuibangua kitaalamu hadi imfikie mlaji na mwisho wanahitaji vifaa, viwanda na maandalizi ya ubanguaji korosho kitaalamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote yanataka fedha, tunapata wapi? Njia pekee ya kupata fedha ni hiyo hiyo ya kuanzisdha mfuko. Hivi sasa, korosho yetu ya Tanzania inaanza kupandwa katika Mikoa mingine nchini, ukiachia Mtwara, Ruvuma na Lindi, kuna Mikoa mingine zaidi imeanza kupanda korosho, nao pia wanahitaji kujiendeleza.

Mikoa hiyo ni Pwani, Ruvuma, Tanga, Dar es Salaam, Mbeya, Morogoro, Iringa na Dodoma.

Mikoa hii yote inayoanza kupenda kulima zao hili, ni budi waendelezwe kwa kupatiwa pembejeo kwa wakati, watambuliwe na waelekezwe masuala mazima ya ubanguaji. Imeonekana kuwa Tanzania husafirisha korosho nje kwa asilimia 2.7% karibu nusu ya mazao mengine mfano tumbaku ni 4.8, pamba ni 4.2%, kahawa ni 4.2% na samaki ni 4.8%.

Kwa hiyo, mimi ninadhani, korosho ikiwekewa mikakati maalumu ya kuliboresha, basi tunaweza kusafirisha nje asilimia kubwa zaidi kama mazao mengine. Njia pekee ni kuwa na Mfuko Maalumu ambao utaingiziwa pesa kutokana na ushuru wa korosho ghafi inayosafirishwa nje ambayo imependekezwa katika Sheria ya Korosho, Sura 203, katika Kifungu cha 17 kwa kuongeza Kifungu kipywa cha 17A ili asilimia ya makusanyo ipelekwe kwenye Mfuko wa Sekta ya Maendeleo ya Korosho ili makusanyo hayo yaweze kuendeleza zao la korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

MHE. MOHAMED H. MISSANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkulo na Manaibu Mawaziri wote wawili pamoja na Katibu Mkuu, Mheshimiwa Khadija, kwa maandalizi mazuri ya bajeti na kupitishwa vizuri tarehe 14/6/2009 pamoja na maandalizi mazuri ya Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu, tumekuwa tukieleza tatizo la kuchanganya mafuta ya *diesel* na mafuta ya taa, maarufu kama ‘Chakachua’, lakini Serikali haijachukua hatua thabiti za kutatua tatizo hili.

Suala hili sasa limefikia mahali pabaya kwani magari ya mafuta zaidi ya 60 yamerejeshwa kutoka nchi jirani tena kwa *escort* ya Polisi. Hii ni aibu na fedheha kwa nchi yetu licha ya kwamba athari zake ni nyingi kwa uchumi wa nchi yetu. Nchi jirani zinategemea mafuta kupitia Bandari ya Dar es Salaam hivyo kwa mtindo huu wa Chakachua, mapato mengi ya nchi jirani tutayakosa kwani hivi sasa wameamua kupitisha mafuta na bidhaa nyingine katika Bandari za nchi nyingine.

Serikali inatakiwa kuchukua maamuzi mazito kurekebisha tatito hili. Suluhisho la kudumu ni kuoanisha kodi ya mafuta ya diseli na kodi ya mafuta ya taa, hakuna njia nyingine. Nafuu ya kodi ya mafuta ya taa inawasaidia wachache sana wakati nchi inapata hasara kubwa kuliko faida ya kutenganisha kodi hizi. Okoa nchi na ondoa fedheha kwa nchi kwa kuoanisha kodi ya mafuta ya taa na diseli na vilevile kuwachukulia hatua kali wote wanaojishughulisha na biashara ya Chakachua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa misamaha na nafuu ya kodi katika maeneo mbalimbali, tatizo ni kwamba watakaofaidika na misaada hii, ni makampuni na wafanyabiashara tu. Mwananchi wa kawaida, mlaji wa mwisho, hatafaidika kabisa. Miaka kadhaa misamaha ilitolewa lakini wananchi hawafaidiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kodi zilizoongezwa kwenye magari sawa lakini pikipiki tusiwatoze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. LUCAS L. SELELII: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Waziri kwa kuitisha bajeti ya 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sioni sababu ya kuweka kodi kwenye pikipiki (bodaboda) kutokana na usafiri huu kutumiwa na wananchi walio na kipato kidogo cha fedha. Itafutwe kodi sehemu nyininge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Serikali kuheshimu mikataba ya wamiliki wa migodi ya madini lakini kuendelea kuwasamehe kodi wachimbaji hawa, ni kujinyima vyanzo vya mapato. Mazungumzo yaendlee, napongeza hatua ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupunguza kodi kwenye mafuta mazito (*HMO*) ili kuwezesha viwanda kama cha cement kupunguza bei, naishauri Serikali iweke ruzuku (*subsidiary*) ili kushindana na bidhaa toka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nawatakia kazi njema.

MHE. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 4, kwa nini tutumie *US dollar* kwenye Sheria yetu? Endapo *dollar* imepanda au kushuka thamani hali itakuwaje? *US\$ one hundred sixty per metric tone, which ever is higher.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *export levy* itakusanywa na *TRA*, tutatumia *mechanism* (utaratibu upi) kujua kwamba pato hili limetokana na korosho za Wilaya X,Y,Z. ili fedha hizo zirudishwe kwenye Wilaya husika? *What if* korosho zinanunuliwa na *middlemen* wa hapa nchini, anakusanya toka Wilaya sita mbalimbali na baadaye yeeye ndio ana-export kwa pamoja, tutajuaje ili kodi ya 65% irudishwe Wilaya husika. Lakini nipongeze suala la kurudisha 65% kwa Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu marekebisho katika viwango cha kutoza ushuru wa mazao shambani kati ya 3% na 5%. Naomba kushauri kuwa ushuru huu wa mazao utozwe kwa mazao ambayo hununuliwa kwa ajili ya biashara na sio chakula. Kwa niaba ya akina mama wa Wilaya saba za Iringa, wanaomba mtu anaponunua debe moja la mahindi, mpunga kwa ajili ya kujikimu chakula, asitozwe ushuru wa mazao. Wale wanaonunua Fuso zima au lori, wanapopita getini ni halalli kulipa kodi. Hivyo, naomba Halmashauri na Wakala wa Ukusanyaji Mazao, walizingatie hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi ninakubaliana na wazo la kusamehe kodi ya majengo kwenye nyumba zinazomilikiwa na wazee lakini nina wasiwasi na maneno ya Kifungu 33 kinachosema:-

“A person ... has no other means of earning than residential ratable property may be exempted from payment of levy”

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inamaanisha kwanza, *it is not for granted* na pili ni *may be, how can you prove?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Section 22 1(b) or b Volume*, hii ‘b’ ina maanisha nini?

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkulo, (MB), Manaibu Mawaziri, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote, kwa kuleta marekebisho haya ya *Finance Act, 2010*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na marekebisho haya yaliyoletwa mbele ya Bunge lako Tukufu, nasikitishwa na wafanyabiashara wanaouza mali kwa kutumia *USD* badala ya shilingi ya Kitanzania. Muswada huu haujazungumzia kuwabana watu hao. Yapo maduka mengi ndani ya nchi yetu yanayouza bidhaa kwa *USD* na Serikali haijawahi kuwachukulia hatua kitu ambacho nchi zingine si ruhusa hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kupunguza ushuru wa bidhaa kwenye mafuta mazito ya kuendeshea mitambo na hasa Viwanda vya Simenti. Nashauri ushuru huo upunguzwe pia kwa Viwanda vya Mabati, pembejeo zote za kilimo kwa mfano magunia, *power tiller* na kadhalika ili wananchi wa hali ya chini waweze kumudu kununua/kufaidika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 98, ni ukweli usiopingika kuwa wafanyabiashara wengi hapa nchini hawatoi stakabadhi na wanaotoa stakabadhi wanatoa baada ya majadiliano na mnunuzi kwani mauzo kwa stakabadhi ni ghali kuliko mauzo pasipo stakabadhi. Kifungu kinachorekebishwa, kinatamka adhabu itakayotolewa.

Ninachoomba ni Serikali kusimamia kwa karibu sana na ikiwezekana viongozi wa Serikali za Mitaa watumike kuhakikisha kuwa stakabadhi zinatolewa kwa kila mauzo, hii itasaidia wakwepa kodi kulipa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sura 124, marekebisho aya ya 3 na ya 4, nashauri marekebisho hayo yaguse zaidi magari ya starehe kwa mfano, *Landcruiser, Lexus, Rangerover* na kadhalika na sio pikipiki au magari ya kusafirisha abiria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kuanzisha Idara ya Usimamizi wa Ukaguzi wa Ndani pamoja na uteuzi wa *CAG*, idara hii ndio jicho la Serikali katika kusimamia matumizi yenye tija. Ninashauri taarifa zitakazotolewa na *CAG* za matumizi mabaya ya fedha za umma, zifanywe kazi mapema na kwa haraka ili kujenga heshima ya matumizi kwa watumishi wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kusamehe kodi ya majengo kwenye nyumba zinazomilikiwa na wazee wenye umri wa miaka sitini na zaidi. Je, msamaha huo ni kwa jengo moja au majengo yote yanayomilikiwa na wazee hao? Ninaomba msamaha huo wapewe watoto yatima waliofiwa na wazazi wote na hawana kipato cha kuwawezesha kulipa kodi ya majengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naunga mkono Muswada huu kwa asilimia mia.

MWENYEKITI: Sasa nitampa Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, ili ye ye aanze kujibu hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezitoa.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru tena kwa kunipa nafasi hii na ninaomba niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge waliochangia Muswada huu. Bila shaka waliowasikiliza watakulaliana na mimi kwamba, kiwango na ueledi wa uchangiaji Bungeni kimeongezeka sana. Ninapokea pongezi kwa maneno mazuri yaliyosemwa na wachangiaji wote. Maneno mazuri yaliyosemwa juu yangu, najisikia mnyonge wakati fulani nikisifiwa kwa sababu kwa *profession* yangu huwa tunaanza kwa kukashifiwa kwanza.

Lakini ninawashukuru sana kwa kunipongeza, ninamshukuru sana Mheshimiwa George Malima Lubeleje, huyu mzee wetu ana uzoefu mkubwa, ni mlezi mzuri, anasikiliza, ana imani na binadamu wenzake, na amenisaidia sana kufafanua Muswada huu kwa lugha nyepesi na sura yenyeye ushawishi. Baba Mheshimiwa Lubeleje, Mungu wetu akunyooshee mikono yake na akujalie katika mahitaji yako. (*Makofî*)

Mchangiaji mama yangu, naona hayupo Mheshimiwa Fatma Maghimbî - Waziri Kivuli wa Katiba na Sheria - Kambi ya Upinzani, amesema maneno mazuri juu yangu lakini tulikuwa tumepatana kwamba kama nilivyokuwa *university; paper* yangu nilikuwa ninaiweka *notice board*, siweki kwenye kwapa. Mimi *paper* yangu nilimpa mapema sana kwamba asome na kama kuna kitu, basi akiseme kwa kufanya *research*, lakini ya kwake hakunipa, hata hivyo ninamshukuru sana.

Kuhusu kifungu cha 26 alichoelezea, nafikiri nimesema vizuri zaidi kwenye hotuba yangu na kwa kweli mabadiliko yanayofanyika katika Sheria hii ya Elektroniki ni kama yale ambayo yako kwenye Sheria ya Madini na tunayaainisha. Jamani Waheshimiwa Wabunge tusiwe na mawazo ya zamani sana, tukadhani kwamba tukiwa wakali Sheria zetu zitatekelezwa ipasavyo.

Nafikiri tuainishe, tuwape nafasi wawekezaji na Mawaziri ambao wana dhamana ya kufanya hizo kazi kusimamia sekta hizo. Itakuwa vizuri zaidi kuliko kuweka vitu vya jumla. Kwa hiyo, mimi jibu langu kwa Mheshimiwa Mama Maghimbî ni hilo, hayupo, lakini nitamtafuta mchana na tutaongea naye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchangiaji wa tatu, Mheshimiwa Kabwe Zitto ninamshukuru sana ndugu yangu. Ni kweli kabisa kwamba, vipengele vile vya Sheria ya Umeme vinazuia uwekezaji na haitakuwa na maana kama unawasikia binadamu wenzako wanalamika kwamba vifungu hivi vinazuia uwekezaji katika Kanda ya Kusini na wewe ukawa umekaa unang'ang'ania tu.

Kwa hiyo, ndiyo maana tumevileta hapa na mimi ninashukuru kwamba umeniunga mkono mara nyingi tu, ninakushukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Kabwe Zitto pia amezungumzia kuhusu viti vya vijana. Mimi ninaamini katika demokrasia, kweli kabisa katika demokrasia ya jumla ya kuanzia kwenye *grass root*. Kwa mfano, pale nyumbani mkeo na wewe mwenyewe na watoto wako ni lazima kuwe na demokrasia kidogo.

Kwa hiyo, ninaamini kwamba katika mambo mengine haya ya viti vya vijana nadhani yanaweza kuanzia pia kwenye Vyama vya Siasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema hivi kwa sababu ni vizuri tukaimarisha demokrasia katika Vyama vya Siasa na nitakuja kwa Mheshimiwa Mwadini, lakini nina taarifa ninyi hamkunikaribisha kwenye mkutano wenu. Wenzeni walinikaribisha katika mkutano wao ingawa sikwenda, na walinipa taarifa kwamba wametenga viti kumi kwa ajili ya vijana na ninajua hapa wengi wenu mlikuwa wanachama wa Chama cha Mapinduzi.

Nafikiri wengine walikuwa bado hawajazaliwa na mnajua jinsi chama hicho kilivyo na utaratibu wa kupanua demokrasia. Naomba muige tu, kwani ni vizuri kuiga, sisemi hivyo kwa sababu ya kuwakandia, bali ninasema hivyo kwa sababu mazungumzo niliyosikia leo na wiki nzima hii, na katika kikao hiki yanaonesha kwamba na ninyi mna mwelekeo wa demokrasia ya kitaifa. (*Makofi*)

Kuhusiana na hili la Madiwani wa Viti Maalum, nimesoma mapendekezo ambayo Mheshimiwa Kabwe Zitto ameyatoa, yameandikwa vizuri. Ukiangalia juu juu ni mazuri sana, lakini ukiangalia kwa undani utagundua kwamba yanadurufu Ibara ya 78(1) ya Katiba na kwa ajili hiyo basi Mheshimiwa Kabwe Zitto, kambale wa mambo haya ni kwenye mchakato kwenye vyama vyetu. Kambale wangu mimi kama Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni Baraza la Mawaziri. Hili ni suala kubwa sana, ni suala la sera kwa sababu unazungumzia sasa haki ya kushiriki ya wanawake katika maeneo haya. Nafikiri kwamba ni vizuri tulijadili kwa kina. Huu sio mwisho wa sheria nafikiri wakati utakapofika tutaandika kwa sababu karatasi za kuandika na kalamu tutakuwa nazo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nikwambie kwamba mantiki ya mapendekezo haya Mheshimiwa Kabwe Zitto yanapunguza fursa kwa vyama vya siasa kupata Madiwani kwa kuwa sasa kigezo kitakuwa kupata angalau asilimia tano ya kura zote zilizopigwa katika Kata. Nafikiri ni mambo ambayo yanahitaji kufikiriwa kwa siku za usoni. Lakini kwa wepesi, mimi kama mtaalamu wa mambo ya kutunga sheria lazima niseme kwamba na wewe unielewe kwamba huyu ni Mwanasheria makini kama ulivyosema, basi Baraza la Mawaziri ndilo lenye dhamana ya kushughulikia hili suala ambalo ni la sera, lakini haizuii mawazo mazuri kama hayo uliyotoa na nakupongeza kwa sababu umefanya *research* nzuri. *Thank you. Thank you again. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, kwanza napenda kuchukua nafasi hii kwa moyo mkunjufu kabisa kukipongeza Chama cha *CUF* kwa uchaguzi ingawa hamkunialika, lakini nilikuwa sifahamu kama mlifanya uchaguzi kwa sababu hata barua hamkuniandikia na *TLP* ambao pia wamefanya uchaguzi wa kumpata Mgombea wa Kiti cha Urais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na maneno kwamba mimi si mwanachama, ni kweli, si kwa hiyari yangu, lakini ni kwa mujibu wa Katiba. Naomba kufafanua hili jambo kwa sababu hata ndugu zangu kule kijijini wengine wanang'ung'unika, wanalamika huku kwamba wewe vipi? Ibara ya 113(a) inasema kwamba; "Itakuwa ni marufuku kwa Jaji wa Mahakama ya Rufani, Jaji wa Mahakama Kuu, Msajili wa Mahakama ngazi yoyote, Hakimu wa ngazi yoyote kujiunga na chama chochote cha siasa isipokuwa tu kwamba atakuwa na haki ya kupiga kura iliyotajwa katika Ibara ya 5 ya Katiba hii." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Jaji, sijajiuzulu bado. Kwa hiyo, ndiyo sababu inanifanya mimi niwe na nguvu ya kusema hivyo kwamba mimi hata mkinialika kwenye *congress I will come. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nakubaliana na wewe kwamba pengine Sheria ya Gharama za Uchaguzi inahitaji kufanyiwa kazi zaidi, tutafanya kila wakati tukipata nafasi, isipokuwa sasa mimi nimesoma Kiswahili kigumu lile neno ulilokuwa unatumia mbeleni si neno la kifasaha, unaweza kusema siku za usoni lakini sio mbeleni, mbeleni ni kitu kingine kabisa, nafikiri huyo alikuwa mchangiaji wa tano. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa mwengine alikuwa ni Mheshimiwa Raynald Mrope. Hili suala la kufuta *EWURA* nafikiri nitamwachia Mheshimiwa Adam Malima wakati wa kwenda kwenye vifungu atakuja alizungumzie, ingawa nina majibu lakini nitampa Waziri ambaye anahuksika nalo akujibu vizuri, sitaki kukujibu ovyo ovyo. *(Makofi)*

Kuhusiana na nadhani tukifika hapo tunakuwa na taabu. Hii Sheria ya Waziri amevunja mabaraza kinyume cha sheria. Hii si kweli kwa sababu sheria ambayo Mheshimiwa Waziri ametumia ni sheria iliyopo sasa ambayo haijafanyiwa marekebisho. Tunachofanya sasa kwenye marekebisho haya kitu kidogo tu ni kuweka muda. Sheria ya sasa haisemi ni kwa muda gani. Sasa tunaweka muda kwamba ni siku saba kabla ya

kuvunjwa kwa Bunge. Nafikiri ni vizuri kuweka *benchmark* kwa sababu unawenza kumpata Waziri mwingine kama mimi, sivunji. Lakini nakubaliana na maoni kwamba ni vizuri tuwe na usimamizi mzuri wa sheria hii. Lakini kwa kweli Waziri amefanya kazi hiyo sawa sawa. Tunaweka sharti la muda tu. Nafikiri alikuwa Mheshimiwa Fatma Maghimbii huyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tunaleta mabadiliko kwenye Sheria ya Uchaguzi, ni kwa sababu ya ukosefu wa umakini, kwa sababu ya ukosefu wa umahiri au uwezo? Ni swali zuri na tusingependa sisi kila wakati kuleta sheria ambayo hata haijaanza kutumika kwenye mabadiliko. Lakini Waheshimiwa Wabunge sheria inapotungwa huwezi kuwauzia watu wengine kuzungumza na watu wengine wakizungumza wakikupa mawazo mazuri ni vizuri kuyachukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa msingi huo tumechukua mawazo haya, kwa mfano tulipokuja na *scheme* ya kwanza tulikuwa tunafikiri kwamba kwa sababu ya kusimamia eneo moja la gharama za uchaguzi kwa mtu mmoja *then* ni vizuri kuweka zile siku tano kabla ya siku ya uteuzi ili kumpa nafasi yeze kuweka pingamizi. Sasa kwa sababu unaondoa hiyo na unaondoa kwa sababu umesikiliza maoni ya watu wengine basi inabidi ufanye marekebisho ya hiyo sheria. (*Makofii*)

Kwa msingi huo Mwenyekiti kwa mara nyingine tena niwashukuru Waheshimiwa Wabunge kama kuna kitu ambacho sikujibu si kwa sababu ya kunuia, lakini ni kwa sababu labda kimenipitia, lakini kama kuna Mbunge yejote ambaye anataka apate majibu zaidi basi tunaweza kuzungumza baadaye au wakati wa kuitisha kifungu kwa kifungu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Waheshimiwa Wabunge hoja imetolewa na imeungwa mkono sasa kwa hatua inayofuata.

WAZIRI WA NISHATI NAMADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki. (*Makofii*)

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

KAMATI YA BUNGE ZIMA

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2010, (The Written Laws (Miscellaneous Amendments) No. 3. Bill, 2010)

MWONGOZO WA MWENYEKITI

MHE. RAYNALD A. MROPE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo hii *Bill Supplement* lakini kuna suala hili katika hotuba ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

linalohusiana na mambo ya Sheria ya Umeme halipo hapa katika hii *main* sheria. Sasa nilitaka kuuliza kama nataka kupata maelezo zaidi nisimame katika kifungu gani hapa?

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la umeme kuna *schedule of amendment*. Naomba uangalie *schedule of amendment* pamoja na ule Muswada.

MWENYEKIDI: Ahsante Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali naona limeshakaa sawa.

Kifungu cha 1

Kifungu cha 2

Kifungu cha 3

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote*)

Kifungu cha 4

MHE. ANDREW J. CHENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama kwanza kuipongeza sana Serikali kwa marekebisho yanayoletwa sasa hivi kwani yana maana kubwa sana katika sekta hii muhimu ya mawasiliano, ila nina kitu kimoja tu cha kusaidia ukisoma kwenye kifungu cha 26(1) kina mtiririko mzuri mpaka unapofika sasa kwenye maneno; “*Approval and transfer of shares of electronic communications, postal, license and content service license.*” Sasa uhamishaji wa hisa ni kwenye Kampuni.

MWENYEKIDI: Samahani Mheshimiwa Chenge, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu simuoni na ndio anatakiwa aijibu hii hoja. Unamwakilisha? Yuko Mheshimiwa Chikawe haya tuendelee sasa. Anza upya Mheshimiwa Chenge.

MHE. ANDREW J. CHENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nilikuwa nasema hivi makampuni haya yana leseni, sasa unapohamisha wewe kama mwanaahisa.

MWENYEKIDI: Samahani ngojea tumsaidie Mheshimiwa Chikawe ni ukurasa wa 6, kifungu cha 26 (1) na 61. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu ameshaingia. Tuendelee.

MHE. ANDREW J. CHENGE: Nadhani hapa ni suala tu la *concept* kwamba tunaweka kiwango cha chini cha umiliki wa hisa katika makampuni yanayofanya biashara hii na utaratibu wa kuweza kuuza hisa kwa *local shareholders*. Hiyo dhana ni nzuri tu ila sasa ilivyokaa huwezi ukasema *transfer of shares* kwa leseni, leseni inashikiliwa na Kampuni na Kampuni hiyo ndani yake kuna wanahisa.

Mimi nilikuwa nashauri kwamba baada ya neno *shares pale tuseme in a company holding*, maana makampuni haya ndio yenye leseni hizi. Wewe ndani ya Kampuni hiyo

ndio unataka kuuza hisa zako kama mzawa au *local shareholder*. Sasa utaratibu huu ndio tunapendekeza utawekwa. Ukiacha namna hii inakuwa haina maana kidogo maana *shares of a licence of postal licence or content licence, service licence* haileti maana. Ndio nilikuwa naomba tu hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa katika kifungu kidogo cha 2 la *class licence C*, hapana. *Individual or class licence*, sio *licence C*. Huo ndio mchango wangu mdogo katika eneo hili. Sasa sijui kama Mwanasheria Mkoo...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwanasheria Mkoo umeuelewa mchango wa Mheshimiwa au akusaidie Mheshimiwa Chikawe.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Andrew Chenge kwenye hili la pili ninakubaliana naye kwamba kwenye kile kifungu cha 26(2) baada ya maneno “*in consultation with a company incorporated in the United Republic*” tuongeze neno “*and holding an individual or a class licence.*” Hiyo ni sawa sawa. Kwenye hili la *concept* ambalo liko kwenye 26(1) kama Mheshimiwa Chenge ana mapendekezo mahsusni vizuri angesema kusudi tuweze kuona kama yanakwenda na...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Chenge nitalazimika kukupa tena nafasi.

MHE. ANDREW J. CHENGE: Nashukuru Mwenyekiti, samahani sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkoo nilisema tu kwamba baada ya neno “*shares*” tufute neno “*of*” halafu tuingize maneno tunaanza kwa kusema “*for approval and transfer of shares in a company holding an electronic communication and postal licence and content service licence.*”

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru tena Mheshimiwa Chenge sina tatizo na mapendekezo aliyoyafanya na naomba yaingie kwenye Muswada huu. Ahsante sana.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake*)

Kifungu cha 5
Kifungu cha 6
Kifungu cha 7
Kifungu cha 8

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote*)

Kifungu cha 9

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)

Kifungu cha 10
Kifungu cha 11

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 12
Kifungu cha 13

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)

Kifungu cha 14

MHE. RAYNALD A. MROPE: Mheshimiwa Mwenyekiti, sielewi hapa kuna 14 mbili. Sasa mimi nilitaka hii ya 14 ya pili.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu sijui utakuwa umemwelewa au aseme tena? Hebu fafanua kidogo tatizo lako liko wapi?

MHE. RAYNALD A. MROPE: Tatizo langu ni kwamba kuna *Part 14* inasema; “*Amendment of Army’s and Ammunition Act.*” Halafu kuna *Part 14* tena inayosema; “*Amendment to the Electricity Act.*” Sasa kwa kuwa yote imetajwa 14 na nisije nikakosa nafasi yangu ndiyo nauliza hii.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hatujafika huko anakozungumzia. Tuko ukurasa wa 10 wa Muswada Kifungu cha 14 sio sehemu ya 14.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 15
Kifungu cha 16
Kifungu cha 17
Kifungu cha 18
Kifungu cha 19

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 20

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)

Kifungu cha 21
Kifungu cha 22

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 23
Kifungu cha 24

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)

Kifungu cha 25

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 26
Kifungu cha 27

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)

Kifungu cha 28

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 29
Kifungu cha 30

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)

Kifungu cha 31

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba asome kwamba Kifungu 31 kina marekebisho yangu.

MWENYEKITI: Ndiyo tayari Mheshimiwa Kabwe Zitto.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Hajasoma kwa sababu kuna marekebisho yangu kwa hiyo inabidi asome kwamba kuna marekebisho ya Mbunge ili ni *move motion* na Waheshimiwa Wabunge waunge mkono halafu tuweze kujadili. Ndiyo utaratibu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu tafadhali.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naepuka *confrontation* kwa sababu ya utaratibu kwamba Mheshimiwa Kabwe Zitto angeleta marekebisho hayo mapema zaidi kuliko alivyofanya ili kusudi tupate nafasi ya kuyaangalia kwa kina zaidi. Sasa kwa hivi walivyoyaleta hapa na wewe mwenyewe ulimwona nilipokuwa nafanya mikono hivi akasema yatakuja. Kwa hiyo, itakuwa vigumu sana ku-*deal* na hoja yake na sidhani kama iko kwenye utaratibu.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, sijatoa hoja ya marekebisho yangu.

MWENYEKITI: Alikukatalia.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Hana Mamlaka ya kukataa Hoja ya Mbunge. Natakiwa nitoe hoja baadaye tuijadili atatoa majibu *then* tutakubali au tutakataa. Bunge ndilo linalokubali au kukataa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kabwe Zitto naomba ukae. Hata na mimi nilikukumbusha kwamba ilionekana kabisa Mwanasheria Mkuu hana marekebisho yako na nikakwambia kwamba ungetumia wakati huu basi ukamfikishia *amendment* kwa wakati. Lakini sasa sijui ilikuwaje na ndiyo maana alipojibu hapa alikukatalia. Kwa hiyo, naomba tuendelee.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti Taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kabwe Zitto usisimame kwa sababu nimekunyima nafasi ya kuendelea kwa sababu hujafuata utaratibu. Tuendelee.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote*)

Kifungu cha 32

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sasa kuchukua fursa hii kutoa hoja ya marekebisho yangu ambayo nataka tufanyie mabadiliko kifungu hicho cha 32 haya mazungumzo ya awali yalikuwa si hoja yenye. Kwanza Kanuni za Bunge hazielezi ni muda gani amba Mheshimiwa Mbunge anapaswa kuleta marekebisho. Muda amba Mheshimiwa Mbunge anazungumza analeta *schedule*, *schedule* inajadiliwa, inakubaliwa au kukataliwa. Hilo ni la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, lazima tujifunze hii nchi imekua. Mwaka kesho nchi yetu inatimiza miaka 50 baada ya Uhuru lazima tujifunze kusikiliza na wengine hata kama hawatoki chama ambacho unatoka. (*Makofi*)

Ni suala la kukua tu, *next year half of the century*, miaka 50 baada ya Uhuru. Kuna *principle* ya *proportionality* kwa mujibu wa Katiba ambayo ipo ndani ya Katiba ambayo inawafanya Wabunge wa sasa wa Viti Maalum wawemo ndani ya Bunge hili kwa wingi huu tulionao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *principle* ile ya *proportionality* marekebisho haya ambayo naya-move sasa Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu ina-translate *principle* ya *proportionality* ndani ya Katiba. Kuyaweka sasa kwenye Serikali za Mitaa na maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba kila kura inayopigwa kwenye uchaguzi, mwananchi anapoenda kumchagua Diwani inakuwa na thamani. Sasa hivi kura ambazo wananchi wanapiga hazina thamani kwa sababu Madiwani wa Viti Maalum wanapatikana kutoka na idadi ya Madiwani ambayo kila chama kinao.

Sasa tunataka kama jinsi ambavyo iko kwenye Bunge hivi sasa kwamba Wabunge wa Viti Maalum watapatikana kutokana na idadi ya kura ambayo kila chama kimepata kwenye uchaguzi wa Wabunge. *Principle* hiyo hiyo tunaishusha sasa chini kwamba Madiwani wa Viti Maalum wapatikane kutokana na idadi ya kura ambayo kila chama kimepata kwenye uchaguzi wa Madiwani. Ndiyo maana nikasema kwenye mchango wangu kwamba katika hili tulighafilika, hatukufanya hayo mabadiliko, kwa sababu tulifanya kwenye Katiba. Kwa sababu uchaguzi wa Madiwani haumo ndani ya Katiba, *composition* ya Madiwani haimo ndani ya Katiba tukachelewa au tukasahau ku-reconcile kwenye Sheria ya Uchaguzi kwa maana ya Sheria Namba 7 na Namba 8 ya *Local Government*.

Kwa hiyo, anachokifanya Mbunge wa Kigoma Kaskazini sasa hivi ni hiyo *reconciliation* haihitaji chama chochote cha siasa kwenda kukaa ama Mkutano Mkuu au NEC au Baraza la Mawaziri kwa sababu tayari tumeweka *principle* ile ndani ya Katiba. Sasa inawezekana kabisa kwamba hoja kama hii angeleta Mbunge wa CCM labda pasingekuwa na mjadala. Lakini kwa sababu hoja hii anaileta Mbunge wa Kambi ya Upinzani inaonekana ni mjadala. Hakuna *in feeling*, hakuna nia mbaya ni nia tu ya kuhakikisha kwamba...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kabwe Zitto nenda kwenye hoja nafikiri Mheshimiwa Mwanasheria ameshaifahamu.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo nafafanua hoja, naomba unipe fursa. Nina muda kwa mujibu wa Kanuni hata kama maneno haya ninayosema hayakupendezi mnipe haki tu ya kuyasema, mkikataa, mmekataa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge umebakwa na dakika moja.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo basi kuna hoja ambayo Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu amesema kwamba mabadiliko haya yatapunguza fursa ya vyama kupata Wabunge, ni *contrary to that*. Mabadiliko haya yataongeza fursa ya vyama kupata Wabunge. Kwa mfano chama kimeweka Madiwani kwenye Halmashauri. Chama kile kimepata asilimia kumi kwa Kata zote zilizoko ndani ya Halmashauri, chukua ziko Kata 12, amepata asilimia kumi maana yake chama hiki...

KUHUSU UTARATIBU

MWANASHERIA MKUU: Kuhusu utaratibu.

MWENYEKITI: Kuhusu Utaratibu Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kulikwa na *objection* kwamba marekebisho haya yanayopendekezwa hayakuletwa kwa mujibu wa Kanuni. *Tui-solve* kwanza hiyo halafu twende kwenye *amendments*. Kanuni iko wazi na Mheshimiwa Kabwe Zitto ameleta mapendekezo haya chini ya Kanuni ya 86(10). Kanuni hiyo inasomeka kama ifuatavyo:-

“Katika hatua hii iwapo Mtoa Hoja anataka kufanya Marekebisho au Mabadiliko katika Muswada wa Sheria kutokana na ushauri uliotolewa ama katika Kamati au wakati wa Muswada wa Sheria Kusomwa Mara ya Pili au kwa sababu nyingine yoyote iwapo Muswada huo ni wa Serikali atamjulisha Mwandishi wa Mkuu wa Sheria na iwapo Muswada husika ni wa Kamati au binafsi atamjulisha Mshauri Mkuu wa Bunge wa Mambo ya Sheria ili atayariske na kumkabidhi Katibu ambaye atagawa kwa kila Bunge nakala ya:

(a) Muswada wa Sheria uliochapishwa upya ukiwa na Marekebisho au Mabadiliko yanayokusudiwa kufanyika au Jedwali la Marekebisho au Mabadiliko yanayokusudiwa kufanyika.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii si Kanuni ambayo Mheshimiwa Kabwe Zitto angeitumia. Kanuni ambayo angeitumia ni Kanuni ndogo ya 11 ambayo inasema; “Kamati au Mbunge anaweza kuwasilisha kwa Katibu kwa maandishi mabadiliko anayoyakusudia kuyafanya katika Muswada huo wakati wa Kamati ya Bunge Zima akionesha bayana mabadiliko yanayokusudiwa kufanyika katika kila Ibara inayohusika.”

Sasa hapa huu mstari hujauvuka, huwezi kwenda mbele. Kwa hiyo, *objection* hii ni kwamba mabadiliko haya hayajaletwa chini ya utaratibu. Mimi nilijifunza kwamba palipo na wazee wanaonizidi umri huwa sipazi sauti. (*Kicheko*)

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)

TAARIFA

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kabwe Zitto, taarifa.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tu kutoa taarifa kwamba taratibu zote zinazotakiwa zilifuatwa, Mshauri wa Sheria wa Bunge ndiye ambaye ameandika mabadiliko haya, Katibu amejulishwa, Wabunge wamegawiwa lakini pale ambapo watu wanaamua kutumia hoja za nguvu kukataa au kupinga jambo ambalo wanalitaka ndivyo inavyokuwa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kabwe Zitto, naona unatupoteza wakati, kaa chini tuendelee.

Kifungu cha 33

Kifungu cha 34

Kifungu cha 35

(Vifungu villivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 36

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi niulize kwamba hiki kifungu sasa kitatumika kwenye muhula huu? Kwa sababu tayari Mabaraza yameshavunjwa au itatumika baadaye na kama ni baadaye mimi nashangaa kwa nini imekuja wakati huu.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu hiki kitatumika siku za usoni na sasa hivi kimeletwa kwa sababu Sheria ilivyo sasa haisemi huo muda na sasa tunasema kwamba Waziri atakapofanya mambo yake afanye siku saba kabla ya Bunge kuvunjwa ni siku za usoni. Lakini hakuna hila wala hila.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 37

Kifungu cha 38

Kifungu cha 39

Kifungu cha 40

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)

Sehemu Mpya ya 12

(Sehemu mpya iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 41

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake*)

Kifungu cha 42

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote*)

Sehemu Mpya ya 13

(*Sehemu Mpya iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu cha 43

Kifungu cha 44

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote*)

Sehemu Mpya ya 14

(*Sehemu Mpya iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu cha 45

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote*)

Kifungu cha 46

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake*)

Sehemu Mpya ya 15

(*Sehemu Mpya iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu cha 47

MHE. RAYNALD A. MROPE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kupata maelezo ya ziada. Katika kifungu hiki *EWURA* kwa bahati mbaya imechelewesha suala la *Artamus* na katika kuchelewesha Serikali ya Uhlanzi ambayo ilitaka kutoa karibu shilingi bilioni 45 ili kusaidia katika suala zima la

umeme vijijini. Wao kutokana na hilo *EWURA* waliweka bei ya senti 40 kwa *KWH* badala ya mapendekezo ya *Artamus* ya senti 26. Wao waliamua kwamba sasa hawataisaidia tena Tanzania. Sasa kwa kitendo hiki tumekosa shilingi bilioni 45. Sasa nataka kuhakikishiwa na Serikali je, kuna mpango mbadala wa kupata fedha hizi ili umeme vijijini uweze kutozwa kwa shilingi 60,000/= mpaka 80,000/= kama ilivyo katika mradi wa awali au sasa tufanye nini na kwa nini *EWURA* yenewe iliyosababisha mambo haya isiwajibishwe kwa kosa hili kwa sababu hili litawaumiza sana watumiaji wa umeme wa Mikoa ya Kusini ya Lindi na Mtwara?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba niseme tu kwamba labda katika hili ambalo Mzee Mrope amelileta precisely mabadiliko haya ya Sheria yaliyofanywa hapa yamelenga kukabiliana na tatizo hili. Tatizo lililokuwepo baina ya *Olet* ni jambo la mwekezaji *Artumas* aliyekuwepo pale ambaye kama kawaida unapokuja kufanya utaratibu wa kuja kuwekeza kwenye umeme ni lazima uje na maelezo ambayo huyu *regulator* anatakiwa ayafanyie kazi na abaini kama kweli katika utoaji wako wa huduma hiyo unayokusudia utafikia yale malengo ambayo yanakusudiwa na sekta yetu ya umeme.

Sasa tulijiwekea hivi vipengele mwaka 2008 mwezi wa nne wakati Sheria hii ilipokuja Bungeni kwa lengo la kutarajia kwamba litaboresha masuala ya usambazaji lakini pia uzalishaji wa umeme na pia kuwezesha sekta binafsi kuwa na ushiriki mkubwa zaidi. Lakini kadri siku zilivyokwenda na utekelezaji na mifano kama hii ya *Olet* imeonesha wazi kwamba vipengele hivi badala ya kutusaidia kujenga na kuendeleza sekta yetu vilikuwa vinatukwaza. Kwa hiyo, mapendekezo yalipokuwa yanakuja ya kuleta mabadiliko haya ndiyo maana tumefuta Sheria hizi.

Lakini katika maelezo yake alikuwa anataka kujua mambo makubwa matatu, moja ni hili la kuchukua hatua gani kuhusu suala la *EWURA* na la pili ni kukamilika kwa mradi wenyewe na haya masuala ya *tariff methodology* na la tatu lilikuwa ni *structure* ya *EWURA*. Sasa niseme tu kwamba tumemaliza suala la kisheria hili suala la *tariff methodology* na kwa nini limekwaza mradi huu kutekelezeka na kufikia hatua kwamba hizo pesa zimepotea kusema kweli kilichofuata hapo kulikuwa na utaratibu wa kufuata ambao kulikuwa na pande zote mbili zilikuwa zinashindwa kuelewana.

Sasa katika misingi hiyo mimi nilisema juzi labda busara haikutumika kuweka msimamo wa taratibu. Kwa hiyo, sisi kama Serikali naamini tutafanya tathimini juu ya hali hii lakini kwa kuwa ule mradi ni ahadi ya Serikali utekelezwe kwa manufaa ya wananchi wa Mtwara na Lindi na maeneo ya mpaka wa Mangaka na kwa sababu gesi iko pale ya kutosha na uwezo wa kuzalisha mpaka *Megawatt* 30 upo pale unatarajiwu kwamba *ka-mini grid* haka kanaweza kufika mpaka Tunduru na maeneo yote yale yakapata umeme kuitia maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naamini kwamba kwa kuwa mradi wenyewe ulikuwa ni mradi unaoendelea zile shilingi bilioni 41 zilizokwuwa zitoke *Olet* zingesaidia sana kufanya wepesi kwenye ule mradi. Lakini kwa sababu haya matatizo ya kiutaratibu yametokea hapo mimi naomba hapo niseme kama alivyosema Waziri wa Nishati na

Madini kwamba bado mradi huu lazima utekelezwe katika hatua zake zote mpaka tufike maeneo ya Nachingwea kwa Mheshimiwa Chikawe mpaka Mangaka kwa Mheshimiwa Mkapa mpaka Tunduru. Kwa hiyo, utekelezaji wa mradi huo bado unaendelea na utekelezwa kulingana na mipango ya Serikali na ahadi zake kwa wananchi wa Lindi na Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili lingine la *structure* ya *EWURA* kwa sasa hivi *EWURA* imeanzishwa Kisheria kwamba ni Mamlaka ya Maji na Nishati. Lakini kwa nchi zingine kuna Mamlaka ya Maji, kuna Mamlaka ya Nishati zikiwa tofauti. Kwa hiyo, mimi naamua hilo, nafikiri hilo ni suala ambalo linaweza likaja Bungeni likajadiliwa. Lakini kwa sasa hivi kwa kuridhia Bunge hili kuondoa vipengele hivi vyta kisheria ninaamini kwamba sekta ya umeme itapata unafuu mkubwa katika malengo yake ya awali ya usambazaji na uzalishaji wa sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Adam Malima. Naomba kufanya mabadiliko kwenye *part* ambayo imeandikwa kwa makosa kama *Part 14* isomeke kama *roman fifteen*.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Ilishafanya huku mezani ilikuwa tayari imeshakaa sawa hiyo.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote*)

Kifungu cha 48

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge pamoja na marekebisho yake*)

(*Bunge lilirudia*)

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa mwaka 2010 (The Written Laws (Miscellaneous Amendments) No. 3, 2010)

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kuwa Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Sheria Mbalimbali Na. 3 wa mwaka 2010 yaani *The Written Laws Miscellaneous Amendments No. 3 of 2010* kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na mabadiliko yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Sheria Mbalimbali Na. 3 wa mwaka 2010 yaani *The Written Laws Miscellaneous Amendments Na. 3 of 2010* kama ulivyorekebishwa sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki. (*Makofi*)

Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, Muswada huu sasa utawasilishwa kwa Mheshimiwa Rais ili sasa ukamilike kwa hatua ya kusainiwa na Mheshimiwa Rais. Ahsante sana Katibu. (*Makofi*)

Kwa hiyo, sasa utaratibu umekamilika rasmi kwa kuwa Muswada umeshasomwa kwa mara ya tatu. Napenda nichukue nafasi hii kukupongeza Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa namna uliviyowasilisha na namna ulivyweweza kujibu masuala ya Waheshimiwa Wabunge mbalimbali ambayo yamejitokeza katika mabadiliko haya ya Sheria Ndogo Ndogo. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, nina matangazo mawili, tangazo la mwanzo ni kukujuisheni kwamba kesho siku ya Alhamisi hatutakuwa na maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu ingawa naona Mheshimiwa Waziri Mkuu mnambona hapo, lakini kuna mawasiliano ambayo Spika tayari ameshayafanya pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu, hakutakuwa na kipindi cha maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa hiyo, tutaendelea na utaratibu tu wa kawaida.

Tangazo lingine, ni kwamba kuna uzinduzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma ambao ulikuwa umepangwa ufanyike tarehe 15 Julai, 2010 na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alitarajiw akuwa mgeni rasmi. Napenda kuwatangazia kuwa uzinduzi huo umeahirishwa mpaka tarehe 16 Novemba, 2010.

Naomba Waheshimiwa Wabunge nikupeni taarifa hiyo ili muweze kujipanga kuhudhuria. Mtajulishwa muda na saa, mimi nimeambiwa niahirishe ile tarehe tu kutoka 15 Julai, kwenda 16 Novemba, 2010 lakini Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundı atakujulisheni muda unaohusika. Ni mwezi wa kumi na moja imeandikwa hapa Waheshimiwa Wabunge. Ndiyo mambo mengine yote mtajulishwa na mwenyewe, Mheshimiwa Waziri wa Elimu.

Napenda pia kuchukua nafasi hii kuwajulisha Waheshimiwa Wajumbe wote wa CCM kwamba kuna kikao leo tarehe 14 Julai, 2010 mara baada ya kuahirishwa kwa kikao hiki cha sasa hivi na kikao hicho kiko katika Ukumbi wa Pius Msekwa. (*Makofit*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa shughuli ambazo zimepangwa kwenye *Order Paper* ya leo zimekamilika, napenda sasa kuchukua nafasi hii kwa kuwa hatutakuwa na kikao cha Bunge cha jioni saa 11.00, niahirishe Bunge mpaka kesho saa tatu barabara asubuhi. (*Makofit*)

(*Saa 6.45 mchana Bunge lilahirishwa mpaka siku ya Alhamisi,
Tarehe 15 Julai, 2010 saa tatu asubuhi*)